

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

MAOMBOLEZO

التعزية

MSIBA WA BWANA WA MASHAHIDI (A.S.)

慈悲ية سيد الشهداء

Lamentations

Part II

The Tragedy of The Lord of the Martyrs

Mtunzi:

Mohammed Ishtihardi

Mtarjuma:

Al-hajj Ramadhani S.K. Shemahimbo

Kimehaririwa na:

Al-Hajj Hemedi Lubumba Selemani (Abu Batul)

Kimepitwa na:

Mbarak A. Nkanatila

ترجمة

التعزية

مصيبة سيد الشهداء

تأليف

محمد إشتهردي

من اللغة الإنجليزية إلى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION**

ISBN: 978 - 9987 - 17 – 031 - 9

Mtunzi:
Mohammed Ishtihardi

Mtarjuma:
Al-Hajj Ramadhani S. K. Shemahimbo

Kimehaririwa na:
Al-Hajj Hemedi Lubumba Selemani (Abu Batul)

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Agosti, 2014
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: www.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la Mchapishaji	1
Dibaji.....	3
Utangulizi.....	4

MLANGO WA KWANZA.....6

YALIYOJIRI KWA KIFO CHA MU'AWIYYAH6

Hali ya wakati wa kifo cha Mu'awiyah	6
Wosia wa mwisho wa Mu'awiyah kwa Yaziid	7
Barua ya Yaziid kwa Gavana wa Madina	7
Mazungumzo ya Imam Husein na Walid	8
Mazungumzo ya Marwan na Walid	9
Safari ya usiku ya Imam na wasaidizi wake	10
Barua za watu wa Kufah	10

MLANGO WA PILI.....12

KUWASILI KWA MUSLIM BIN AQIL MJINI KUFAH12

Kuwasili kwa Muslim bin Aqil mjini Kufah na kusoma barua ya Imam Husein	12
Maelezo ya namna ya kifo cha Muslim bin Aqil	13

Udanganyifu wa Ibn Ziyad na onyo lake kwa watu wa Kufah	14
Mpiga mbiu wa ibn Ziyad	15
Usaliti na kukosa uaminifu kwa watu wa Kufah	16
Makabiliano ya Muslim bin Aqil na ibn Ziyad	20
Wosia wa mwisho na ombi lake Muslim bin Aqil	22
Shahada ya Hani ibn Urwah	24
Msiba wa wale watoto wawili wa Muslim bin Aqil	28

MLANGO WA TATU35

SAFARI YA KUTOKA MAKKA KWENDA KARBALA.....35

Kuondoka Makka kwa Imam Husein (a.s.)	35
Wosia wa Imam (a.s.) katika kuondoka kwake Makka	36
Hotuba ya Imam Husein wakati wa kuondoka kwake Makka	36
Nyoyo na Panga za watu wa Kufah	37
Shahada ya Qais ibn Mushir al-Saydawi –	
Mjumbe wa Imam Husein.....	38
Mazungumzo ya Ali al-Akbar ibn Husein na Imam	40
Maombi ya Imam ya kutaka msaada	41
1. Ubaidullah bin Hurr al-Ju’fi	41
2. Zuheir ibn Qayn al-Bajali	43
3. Wahb	45
Taarifa za kuuawa Shahidi kwa Muslim bin Aqil	46

Vilio na machozi kwa taarifa za Shahada ya Muslim bin Aqil	47
Kuzuiwa njiani Imam na majeshi ya Hurr ibn Yazid Riyahi	49
Swala ya Jamaa	51
Mazungumzo ya Imam na Hurr	52
Hotuba iliyotolewa na Imam hapo Bidah	54
Kuwasili kwa Imam Karbala	55

MLANGO WA NNE58

MATUKIO YA KARBALA KABLA YA SIKU

YA ASHURA.....58

Kuwasili kwa Habib ibn Mudhahir hapo Karbala	58
Kuwasili kwa Umar bin Sa'd hapo Karbala	61
Mazungumzo ya mjumbe wa Imam na Umar bin Sa'd	63
Mazungumzo ya Imam na Umar bin Sa'd	64
Barua danganyifu ya Umar bin Sa'd kwa Ibn Ziyad na majibu yake	66
Habib ibn Mudhahir anajaribu kupata kuungwa mkono na Bani Asad	67
Matukio ya mwezi 9 Muharram	68
Kukataliwa kwa hati ya usalama	70
Matukio ya mkesha wa Ashura	71
Tangazo la Imam juu ya kudhihiri kwa Imam Mahdi (a.t.f.s.)	73

Machungu makali ya Bibi Zainab katika usiku wa Ashura	74
Kujizatiti kwa Imam na wafuasi wake katika usiku wa Ashura	76
Tukio la Nafi'i ibn Hilal kwenye usiku wa Ashura	77
Kuleta maji.....	79
Kuchimba mtaro	80
Majadiliano yaliyofanyika usiku wa manane	80
Tukio pamoja na Barayr ibn Hudayr	81
Ndoto aliyoita Imam	82

MLANGO WA TANO.....83

VIFO VYA KISHAHIDI VYA WAFUASI WA IMAM	83
---	-----------

Kuanza kwa siku ya Ashura	83
Idadi ya wafuasi wa Imam ambao waliuawa	85
Hurr bin Yazid Riyahi anarejea kutoka kwenye jeshi la Umar bin Sa'd	87
Shahada za ndugu na watoto wawili wa Hurr bin Yazid Riyahi	90
Shahada ya Hurr ibn Yazid Riyahi	91
Maneno ya Imam Ali ibn Husein juu ya mwili wa Hurr	93
Uingiliaji kati wa mapema wa Abbas ibn Ali katika mapambano	93

Maelezo juu ya Shahada ya Muslim ibn Awsajah	95
Shahada ya Habib ibn Mudhahir	96
Swala ya mwisho ya Imam (a.s.)	98
Shahada ya Zuheir ibn Qayn	99
Shahada ya Anas ibn Harith Kahili	100
Shahada ya Junadah ibn Harith Ansari na mwanawе Umar	101
Shahada ya Wahb na mke wake Haniyah aliyemuoa karibuni ..	103
Shahada ya Juwayn	105
Shahada ya Hajjaj ibn Masruq	107
Shahada ya Hafhaf ibn Muhammad	107
Shahada ya Suwayd ibn Umar	109
MLANGO WA SITA	110
KUULIWA KISHAHIDI KWA FAMILIA YA	
IMAM HUSEIN	110
Bani Hashim wajiandaa kwa mapambano	110
Kizazi cha Imam (a.s.)	110
Watoto wa Imam al-Hasan waliopigana hapo Karbala	111
Shahada ya Ali ibn Husein – Ali Akbar (a.s.)	113
Shahada ya Abdallah ibn Muslim ibn Aqil (a.s.)	119
Shahada za Awn na Muhammad, watoto wa Bibi Zainab (a.s.)	121

Taarifa za Shahada za Awn na Muhammad zamfikia Abdallah ibn Ja'far	123
Shahada ya Qasim ibn al-Hasan (a.s.)	124
Kujeruhija kwa Hasan ibn Muthanna	127
Shahada za Abdallah, Ja'far na Uthman – ndugu zake Abbas ibn Ali (a.s.)	129
Shahada ya Abbas ibn Ali (a.s.) – Kuzaliwa na hadhi tukufu ya Abbas ibn Ali	130
Vyeo vya Abbas ibn Ali	132
Kifo cha Abbas ibn Ali wakati akienda Furati kujaribu kupata maji	134
Maneno ya mwisho kati ya Abbas na Imam (a.s.)	138
Kurejea kwa huzuni kwa Imam (a.s.) kutoka mto Furati	139
Vilio na maombolezo ya Bibi Zainab kwa kifo cha Abbas	140
Maelezo mengine ya kifo cha kishahidi cha Abbas	141
Baadhi ya maelezo ya baadaye ya huzuni na uvutiwaji juu ya Abbas ibn Ali (a.s.).....	142
Maamkuzi ya Imam wa kumi na mbili kwa Abbas ibn Ali (a.s.)	143
Sababu zaidi na maelezo juu ya huzuni kubwa juu ya Abbas ibn Ali (a.s.)	144
Vifo vya huzuni vya Abdallah ibn Husein na Ali Asghar ibn Husein – watoto wachanga wa Imam Husein (a.s.)	147
Mauwaji ya Abdallah ibn Husein (a.s.)	149

Kifo cha msiba mkubwa cha Ali Asghar ibn Ali (a.s.)	150
Huzuni ya Imam kwa kifo cha Ali Asghar (a.s.)	150
Sakina akabiliana ghafla na mwili ulioloana damu wa Ali Asghar	150
Kifo kinachopenya moyoni cha mtoto kando ya mahema	152
Msiba wa Abdallah Asghar ibn al-Hasan (a.s.)	152
Ujasiri wa masahaba wa Imam (a.s.) kama unavyoiezwa na maadui	154

MLANGO WA SABA155

MSIBA MKUBWA WA BWANA WA MASHAHIDI IMAM HUSEIN IBN ALI (A.S.)155

Kuagana kwa mwanzo	155
Kuagana kwa mwisho kwa Imam na Imam Ali ibn Husein Zainul-Abidin (a.s.)	156
Majonzi ya kuaga kwa mara ya mwisho kwa Imam (a.s.)	160
Kuagana kunakovunja moyo kwa Imam na bintiye kipenzi Sakinah (a.s.)	162
Mtoto mwenye kiu anamkimbilia Imam (a.s.)	163
Kuagana na Bibi Zainab (a.s.)	164
Kukumbuka wosia wa mwisho wa Bibi Fatimah (a.s.)	165
Tukio la kutisha wakati wa kuagana kwa mara ya mwisho	166
Uchangamfu mkubwa na hamasa ya Imam (a.s.)	167

Imam anajitambulisha na kutoa hoja ya kuvunja nguvu kwa adui	170
Kuvitazama vita vya mwisho vya Imam (a.s.)	172
IMAM KWENYE KINGO ZA MTO FURATI	173
Mapigano ya mtu mmoja mmoja	174
Du'a ya mnong'ono ya Imam (a.s.)	176
Bibi Zainab katika kukatwa kichwa kikatili kwa Imam (a.s.) ...	177
Imam (a.s.) Kurushiwa jiwe na mkuki wenyencha tatu	178
Shahada ya kuchoma moyo ya Imam (a.s.)	179
Imam anaomba maji	181
Msiba wa Dhul-Janah – yule farasi mwaminifu wa Imam (a.s.)	182
Sakina pale anapomuona Dhul-Janah	184
Baadhi ya misiba isiyovumilika iliyompata Imam ile siku ya kupata Shahada yake	185

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni tarjumi ya Kiswahili ya kitabu cha Kiingereza kitiwacho, *Lamentations – The Tragedy of the Lord of the Martyrs*, kilichoandikwa na Muhammad Muhammadi Ishtihardi. Sisi tumekiita, *Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi*.

Kitabu hiki ni moja ya mfululizo wa vitabu vinavyochapishwa na Taasisi ya al-Mahdi kwa ajili ya kuelimisha Umma wa Waislamu.

Kitabu hiki ni cha maombolezi ya masaibu ya Karbala, ambapo mwandishi anaelezea matukio mbalimbali muhimu yaliyotokea pale Karbala kuanzia mwanzo mpaka Siku ya Ashura, siku ambayo Imam Husain (a.s) alipigana kishujaa na kuutoa uhai wake kwa ajili Uislamu; kama alivyosema mwenyewe kwamba hatoki (kupigana) kwa ajili ya kupata maslahi ya kidunia bali anatoka kwenda kupigana kwa ajili ya Uislamu na kuurudisha katika maadili yake ya awali kama yalivyowekwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w).

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote; ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Kutoka na ukweli huu, taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwashudumia Waislamu hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru ndugu yetu al-Haj Ramadhani S. K. Shemahimbo kwa kazi kubwa aliyofanya ya kukitarjumi kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili. Pia tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na kesho Akhera – Amin.

**Mchapishaji
Al-Itrah Foundation**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

DIBAJI

Hiki ni kitabu cha kwanza kati ya vitabu vingi ambavyo inata-rajiwa kwamba Taasisi ya al-Mahdi itavichapisha. Lengo la *al-Mahdi Publications* ni la namna tatu. La kwanza kati ya haya ni kufanya upatikanaji, kwa lugha ya Kiingereza wa vitabu juu ya dhamira za Kiislamu vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiarabu, Kiajemi na Urdu. Kwa njia hii inatarajiwa kutoa muendelezo wa kupatikana fasihi ya Kiroho kwa Waislam na wasiokuwa Waislam, wanaoongea lugha ya Kiingereza. Lengo la pili ni kuwapatia jamii ya Kiislam na wengineo fasili za Kiingereza za du'a na ziyarat muhimu katika vijarida ama vitabu vidogo vidogo. Lengo la tatu ni kuchapisha kikamilifu tafsiri zilizofafanuliwa za vitabu muhimu vikubwa vya wanachuoni wa Ki-Shi'ah na monografia – makala za mada moja moja muhimu juu ya mas'ala ya Kiislam.

Kitabu hiki kinaangukia kwenye kundi la kwanza. Ni kazi ya fasihi ya kiroho, kuadhimisha na kukumbuka ule msiba wa Imam al-Husein (a.s.) pale Karbala. Inatarajiwa kwamba kwenye mfululizo huu vitabu vingine viwili vya wanachuoni maarufu wa Iran vitachapishwa katika siku za baadaye.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

UTANGULIZI

Kitabu hiki ni cha pili katika mfululizo wa mijaladi mitatu ya Maombolezo. Mjaladi wa pili umetengwa kwenye madhumuni ya Kifo cha Imam Husein (a.s.) huko Karbala. Inatarajiwa kwamba tarjuma ya hiyo mijaladi mingine miwili itachapishwa baadaye.

Kitabu cha asili kiliandikwa kwa lugha ya Kiajemi (Kifursi). Hata hivyo, mwandishi ametumia sana vyanzo vya Kiarabu, kutoka kwenye vyanzo vya kihistoria vya mwanzoni kabisa vinavyopatikana hadi leo hii mpaka kwenye vitabu vya kisasa zaidi. Amenukuu vilevile kutoka kwenye vitabu vya Kiajemi vya hivi karibuni tu. Alipotumia vyanzo vya Kiarabu, mwandishi ametafsiri wakati mwingine moja kwa moja kutoka kwenye lugha ya Kiarabu na wakati mwingine amefafanua matini ya Kiarabu. Hivyo tafsiri ya Kiingereza imelichukulia maanani hili. Kwa hiyo wakati mwingine hakikupewa tafsiri ya moja kwa moja kutoka kwenye Kiajemi bali wakati mwingine alirejea kwenye vyanzo vya Kiarabu na mara kwa mara akafanya fasili kwenye Kiajemi.

Kitabu hiki sio kitabu cha historia bali ni mkusanyiko wa vipande vya fasihi kutoka Karbala ambavyo vinakazia ule msiba mkuu wa tukio lile. Kinatoa visa vifupi ambavyo vinatumika kutilia mkazo ule muhanga mkubwa uliofanywa na Imam Husein (a.s.), familia yake na wafuasi wake. Kimekusudiwa kuwa kama tafakari akisi ya kiroho juu ya safari ya huzuni na maafa ambayo yalifikia kilele hapo Karbala. Ili kuwasilisha kazi hii kwenye ulimwengu uzungumzao

Kiingereza, ilionekana ni muhimu kufanya uhariri kiasi fulani na kupangilia upya yale yaliyomo ili kwamba tukio lifuatue tukio kwa utaratibu wake. Kwa nyongeza, baadhi ya majina yamesahihishwa kulingana na vyanzo vya uhakika vya awali kabisa, yaani at-Tabari, al-Baladhuri na al-Shaykh al-Mufid.

Majina yamesababisha matatizo kiasi kwa vile kibainishi kilichotumika kama kiambishi awali kwenye jina, kwa mfano al-Husein hakitumiki sana katika maandishi ya Kiajemi, kwani Kiajemi hakina hili kama sehemu ya muundo wa lugha yake yenye. Kwa hiyo imeamuliwa kutumia mtindo wa al- kwenye majina ya Maimam tu. Majina yote ambayo yanakuwa na mtindo huu katika Kiarabu yameondolewa ile al- kabla yao. Kwa namna hii, yale majina ya Maimam ambayo yana kiambishi al- yanatofautiana na majina mengine.

Mwishiuni mwa kitabu kuna mapendekezo ya vitabu vilivyoandikwa kwa Kiingereza ambavyo vinaweza kuwa na msaada kwa wale wanaotaka kufanya uchunguzi zaidi wa historia na fasihi juu ya Kifo cha Imam al-Husein (a.s.).

بسم الله الرحمن الرحيم

MLANGO WA KWANZA

YALIYOJIRI KWA KIFO CHA MU'AWIYYAH

HALI YA WAKATI WA KIFO CHA MU'AWIYYAH

Imam Husein (a.s.) aliupata Uimam mnamo mwaka wa 50 A.H. baada ya kifo cha kaka yake Imam al-Hasan (a.s.). Uimam wa Imam Husein (a.s.) uliendelea kwa miaka kumi, ambapo miaka tisa na miezi minne kati ya hiyo ilisadifiana na Ukhalfa wa Mu'awiyyah bin Abi Sufyan na takriban miezi sita na ukhalifa wa mwanawewe Yazid.

Mu'awiyyah alifariki mwaka wa 60 A.H. baada ya miaka ishirini kama khalifa. Kinyume na masharti ya mkataba aliofanya na Imam Hasan, ambamo aliahidi kutoteua mrithi, Mu'awiyyah alimtaja rasmi Yazid kama mrithi wa Ukhalfa. Mu'awiyyah alikuwa amechukua viapo vya utii kwa Yazid kutoka kwa wengi wa Waislam mbali na watu maarufu wachache wa wakati huo, mionganoni mwao akiwemo Imam Husein (a.s.), Abdallah ibn Umar, Abdallah ibn Zubeir na Abdur-Rahman ibn Abi Bakr. Hata hivyo, huyu Abdur-Rahman ibn Abi Bakr alifariki kabla ya Mu'awiyyah.

WOSIA WA MWISHO WA MU'AWIYYAH KWA YAZID

Hofu na wasiwasi aliokuwa nao Mu'awiyyah kwa sababu watu hawa hawakutoa kiapo cha utii kwa Yazid unajionyesha katika wasia wake wa mwisho kwa Yazid, ulioandikwa wakati kilipokaribia kifo chake. Alimwambia Yazid: "Nimepokea viapo vya utii kwa ajili yako kutoka kwa Waislam wote isipokuwa hawa watu watatu: Husein ibn Ali, Abdallah ibn Umar na Abdallah ibn Zubeir. Kuhusu Abdallah ibn Umar nenda naye vizuri na utamkuta akiwa rafiki msaidizi. Na kuhusu Abdallah ibn Zubeir, huyu umtafute, umuue na umkatekate vipande kwa sababu wakati wowote wa fursa ya mwanzo yeye atakutafuta na kukuchana vipande kama simba mwenye njaa, ama atakufanya mitego na hila kama mbwamwitu. Na kuhusu Husein ibn Ali, watu wa Iraq wataunga mkono madai yake tu kama wataweza kumshawishi ajitokeze na kuasi. Kama atatoka na kuasi dhidi yako, basi umshinde katika mapambano. Hata hivyo, usiwe na uhasama juu yake kwa sababu ya uhusiano wake wa karibu wa kifamilia na wewe na kwa haki zake kubwa maarufu.

BARUA YA YAZIID KWA GAVANA WA MADINA

Baada ya kifo cha Mu'awiyyah, Yazid alituma barua kwa gavana wake wa Madina, ambaye ni Walid bin Utbah ibn Abi Sufyan, ambaye pia alikuwa ni binamu yake. Katika barua hiyo aliandika hivi: "Oh Walid! chukua kiapo cha utii kutoka kwa al-Husein ibn Ali bila ya kuchelewa na usimpe nafasi ya kukawiza kwa hali yoyote ile."

Walid, akitenda kwa mujibu wa maelekezo hayo, alituma akaitwe Imam Husein (a.s.) katikati ya usiku. Imam Husein (a.s.) akikisia

makusudio ya Walid, alikusanya kikundi cha watu wa familia yake na akawapa maelekezo yao ya kufuata: “Walid ameniita mimi na ninahofia kwamba anaweza akanilazimisha jambo ambalo huenda siridhiki nalo. Hatimae ninahofia juu ya maisha yangu. Hivyo kusanyeni silaha zenu na msubiri nje ya mlango wa Walid. Mtaka-posikia sauti yangu ikija juu, basi njoni upesi sana kunilinda.”

MAZUNGUMZO YA IMAM HUSEIN NA WALID

Imam Husein (a.s.) alikwenda kwa Walid usiku huo na akamkuta Marwan akiwa amekaa karibu naye. Walid akamjulisha Imam juu ya kifo cha Mu’awiyyah. Katika hili, Imam kama ilivyokuwa desturi yake ya kawaida akasoma ile aya: “*Inna lillahi wa inna ilayhi raiju-un* – sote tunatoka kwa Mwenyezi Mungu, na kwake sote tutarejea.”

Walid akasoma ile barua ya Yazid mbele ya Imam ambayo ilitaka kiapo cha utii kutoka kwake Imam (a.s.). Baada ya kusikia yaliyokuwemo ndani ya barua, Imam Husein akamwambia Walid: “Mimi sifirkirii kwamba utaridhika mimi nitoe kiapo cha utii kwa siri. Unaonaje badala yake nikatoa kiapo hicho kwenye mwanga wa mchana kweupe na mbele ya kadarnasi ya watu?” Walid akajibu akasema: “Hilo ni sawa.” Imam Husein (a.s.) akasema: “Kwa hali hiyo, ngoja suala hili libakie hadi kesho.” Kwa hili, Walid akasema: “Wallahi rudi nyumbani kwako na unijie kesho ili kutoa kiapo hicho cha utii mbele ya watu.”

Kufikia hapa mazungumzo yakawa yamekwisha. Marwan akamwambia Walid: “Kama ukimruhusu Husein kuondoka hapa kwako, hutampata tena mpaka damu nyingi sana iwe imemwagika kati yako na yeze! Chukua kiapo chake sasa hivi. Vinginevyo basi mkate kichwa chake.” Imam Husein (a.s.) mara moja akaondoka

pale alipokuwa na akasema kwa hasira: “Ewe mwana wa mwanamke mwenye macho ya buluu! Utaniua wewe au yeye. Wallahi umeongopa na umetenda dhambi.”

Waliposikia ile sauti ya Imam iliyopanda juu, wale watu wa familia yake haraka sana wakaingia ili kumsaidia wakiwa wamechomoa panga zao tayari. Imam (a.s.) akawatuliza na kuwaamuru warudi wakae naye.

MAZUNGUMZO YA MARWAN NA WALID

Baada ya Imam (a.s.) kuondoka, Marwan alimwambia Walid: “Hukuzingatia yale niliyokwambia. Wallahi hutamuona tena! Kwa hili Walid akajibu: “Huzuni na iwe bahati mbaya ya wengine! Hicho ulichonitaka mimi nikifanye kinalazimisha uvunjifu wa imani yangu. Wallahi kama ufalme wa ulimwengu wote ningepewa mimi, nisingemuua Husein. Alhamdu Lillahi! Mimi niweze kumuua Hussein, ati kwa sababu hakutoa kiapo cha utii? Mimi sidhani kama mizani ya muuaji wa Husein itakuwa nyepesi hiyo Siku ya Hukumu.” Marwan akajibu: “Kama hiyo ndio ilikuwa nia yako katika kumwacha Husein aondoke basi umefanya jambo la kupongezwa.” Hili ni jambo alilolisema Marwan kinafiki ili kumpendeza Walid. (*Kitab al-Irshaad*)

Asubuhi iliyofuata, wakati Marwan alipokutana na Imam (a.s.) alisema: “Ni maoni yangu kwamba kama utatoa kiapo cha utii kwa Amirul Muminiin Yazid, itakuwa ni vyema kwako katika dunia hii na kesho Akhera.” Kuyasikia haya Imam akasema: “Mimi natoa muago wangu wa mwisho kwa Uislam ambao umeteswa na mtawala kama Yazid. Nimemsikia babu yangu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) akisema kwamba Ukhaliifa umeharamishwa kwa watoto wa Abu Sufyan.” (*Muthir al-Ahzan*)

SAFARI YA USIKU YA IMAM NA WASAIDIZI WAKE

Mkutano wa Imam (a.s.) na Walid ulifanyika katika usiku wa Jumamosi, 27 Rajab ya mwaka wa 60 A.H. Usiku huu Imam aliupitisha akiwa nyumbani kwake huko Madina. Mnamo jioni ya siku iliyofuata, Walid alituma kikundi cha watu wake nyumbani kwa Imam kwenda kumleta aje kutoa kiapo cha utii kwa Yazid. Imam (a.s.) aliwataka wawakilishi wa Walid wampe muda mpaka kesho yake asubuhi ili pande zote mbili zilitazame jambo hilo kwa makini na uangalifu. Wakati Walid aliposikia ombi la Imam (a.s.), yeye akalikubali. Ndani ya usiku ule ule, usiku wa Jumapili 28 Rajab, Imam pamoja na wanawe, ndugu zake, wapwa zake na wengi wa watu wa familia yake, isipokuwa mmoja wa kaka zake, Muhammad ibn al-Hanafiyah, waliondoka kuelekea Makka.

Imam (a.s.) na watu wa familia yake waliwasili mjini Makka mnamo mwezi wa Shabani mwezi 3, mwaka wa 60 A.H. (*Kitab al-Irshaad*)

BARUA ZA WATU WA KUFAH

Taarifa za kifo cha Mu'awiyah, kujizua kutoa kiapo cha utii kwa Imam Husein (a.s.) na kuwasili kwake Makka zote ziliwafikia watu wa al-Kufah. Shi'ah wa mji wa al-Kufah wakajikusanya katika nyumba ya Suleiman ibn Surad al-Khuza'i. Baada ya kusikia maelezo ya hali hiyo, wao waliamua kuandika barua kwa Imam (a.s.) kumwalika aje al-Kufah. Miogoni mwa watu waliotia saini kwenye barua hiyo walikuwa ni Sulaiman Ibn Surad, Musayyib ibn Najabah, Rifa'ah ibn Shaddad na Habib ibn Mudhahir pamoja na wafuasi wengine waaminifu wa Shi'ah.

Barua hiyo ilitumwa kwa Imam (a.s.) na ikamfikia mnamo mwezi 10 Ramadhan. Kisha barua za baadaye kutoka kwa watu mbalimbali wa mjini al-Kufah pia zikatumwa kwa Imam (a.s.). Kulikuwepo na barua zaidi ya mia moja na hamsini zikimwita Imam kuja kuwaongoza dhidi ya Yazid. Yafuatayo ni maneno ya barua moja kama ilivyonukuliwa kutoka kwenye *Kitab al-Irshaad*: “Kwa Jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Hii ni barua kwa al-Husein ibn Ali kutoka kwa Waislam waaminifu wa Shi’ah wa al-Kufah. Baada ya kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumsifu, O Husein, elekea kwetu kwani tunakusubiri, na hatuna mwingine kuliko wewe. Kwa hiyo harakisha, harakisha na tena harakisha. Amani iwe juu yako.” (*Kitab al-Irshaad*)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, barua moja ilieleza hivi: “Kuna panga elfu moja ndani ya al-Kufah zinazongojea kukulinda wewe. Usicheleweshe kufika kwako al-Kufah.” (*A yan al-Shi’ah*).

MLANGO WA PILI

KUWASILI KWA MUSLIM BIN AQIL MJINI KUFAH

KUWASILI KWA MUSLIM BIN AQIL MJINI KUFAH NA USOMA BARUA YA IMAM HUSEIN (A.S.)

Imam al-Husein (a.s.) alimchagua Muslim ibn Aqil, mtoto wa ami yake na mume wa dada yake Ruqayyah kurudisha majibu kwa barua za watu wa Kufah.

Muslim ibn Aqil pamoja na wafuasi wake waliondoka kuelekea Kufah na wakawasili hapo mnamo mwezi 8 Shawwal, mwaka 60 A.H. Muslim ibn Aqil alifikia kwenye nyumba ya Mukhtar ibn Abi Ubaydah Thaqafi, iliyojulikana zaidi kama nyumba ya Salim ibn Musayyib. Katika maelezo mengine yaliyotolewa na Tabari, yeche aliaka katika nyumba ya Muslim ibn Awsajah. Idadi kubwa ya Shi'ah walikusanyika katika nyumba hiyo, na Muslim ibn Aqil akawasomea ile barua kutoka kwa Imam Husein (a.s.). Walipoyasikia yaliyokuwemo ndani ya barua hiyo walilia machozi. Barua ilisomeka hivi: "Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Kutoka kwa al-Husein ibn Ali kwenda kwa waumini wa Kiislam. Hani na Sa'id wamewasilisha barua zenu kwangu. Hawa ndio waliokuwa wajumbe wenu wa mwisho kuja kwangu. Baada ya kuzisoma barua zenu zinazoniomba kuja kwenu ili Mwenyezi

Mungu aweze kuwaongoza, nimechagua kumtuma kwenu kaka yangu na binamu yangu, Muslim ibn Aqil, ambaye anashiriki siri zangu na uaminifu. Kama Muslim atanishauri kwamba maoni na mawazo ya watu wenu wenye hekima na wasomi yanalingana na kile mllichokieleza kwenye barua zenu, basi kwa Mapenzi ya Mwenyezi Mungu mimi nitakuwa pamoja nanyi hivi karibuni tu. Naapa kwa uhai wangu! Imam ni yule tu anayetawala kwa Kitabu, anayesimama katika haki, anayeshikamana na dini ya kweli na anayejizua mwenyewe ndani ya yale yanayomridhisha Mwenyezi Mungu.” (*Kitab al-Irshaad*).

MAELEZO YA NAMNA YA KIFO CHA MUSLIM BIN AQIL

Pole pole watu wakaanza kumtembelea Muslim ibn Aqil na kutoa viapo vya utii kwake kwa niaba ya Imam Husein (a.s.). Watu elfu kumi na nane walitoa viapo vya utii kwa Muslim ibn Aqil. Kisha yeeye akatuma taarifa juu ya hili kwa Imam ndani ya barua.

Wakati huo, Nu'man ibn Bashir alikuwa ndiye Gavana wa al-Kufah. Wafuasi wa Yazid walikuwa na wasiwasi kwamba Nu'man hakuwa mwangalifu vya kutosha na wakamwandikia Yazid wakimjulisha hali ilivyokuwa hapo Kufah. Yazid alipoipokea taarifa hii, aliwaona washauri wake. Baada ya kuchukua ushauri wao, Yazid aliamua kumteua Ubaydullah ibn Ziyad, ambaye tayari alikuwa gavana wa Basrah, kuwa gavana wa al-Kufah vilevile. Yazid aliandika barua kwa Ubaydullah akimfahamisha juu ya matukio ya huko Kufah na kumpa mamlaka kamili ili aweze kuchukua udhibiti kamili wa mji huo na kuzima huo uasi wa Muslim ibn Aqil na wafuasi wake.

UDANGANYIFU WA IBN ZIYAD NA ONYO LAKE KWA WATU WA KUFAH

Ibn Ziyad mara tu baada ya kupokea barua hiyo, alimteua ndugu yake Uthman ibn Ziyad kama makamu wake hapo Basra wakati yeye mwenyewe alipoondoka kuelekea Kufah. Alipokuwa anakaribia mji wa Kufah alivaa kilemba cheusi kichwani mwake na akafunika uso wake ili kwamba afanane na mwana wa Ki-Bani Hashim. Aliingia katika mji wa Kufah kwa hali hii pamoja na msafara wake. Wakazi wa Kufah wakiwa wanatarajia ujio wa Imam, walimdhania Ibn Ziyad kuwa ni Imam kutokana na namna alivyokuwa amevaa. Matokeo yake wakamkaribisha kwa mkarara wa, “Karibu! Ewe mtoto wa Mtume! Sisi tuko pamoja nawe, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa!” Watu waliodhani kwamba aliyewasili ni Imam walizidi kuongezeka kwa idadi mpaka wakafikia elfu arobaini. Muslim ibn Amr, mmoja wa wale waliokuja pamoja na ibn Ziyad, aliwaamuru watu watawanyike na akawajulisha kwamba alikuwa ni Ibn Ziyad, gavana mpya wa Kufah ndiye ambaye amewasili na wala sio Imam. Kwa kulisikia hili, baadhi ya watu ambao walikuwa wamekusanyaika walitawanyika ambapo wengine walibakia wakifikiria bado kwamba aliyewasili ni Imam. Wakati jioni ilipokuwa inakaribia, Ibn Ziyad aliwasili kwenye kasiri la gavana. Nu’man ibn Bashir, yule gavana wa Kufah alifunga milango akidhania kwamba ni Imam ambaye amekuja kuchukua udhibiti wa kasiri hilo. Alipoamriwa kufungua, yeye alitokeza kichwa chake kutoka juu kabisa ya kasiri na akasema: “Ewe mtoto wa Mtukufu Mtume! Mimi sitakabidhi ofisi hii, ambayo imeaminishwa kwangu, kwako wewe, na hakuna haja ya vita kutokea kati yetu.” Hapa ibn Ziyad alisogea karibu zaidi na kasiri hilo na kujitambulisha kwa Nu’man na akaamuru milango ifungulilwe. Waliposikia sauti ya ibn Ziyad, watu wote wa Kufah hatimae

wakatambua kwamba huyu ni mtoto wa Marjanah (yaani ibn Ziyad) na sio Imam mwenyewe. Ibn Ziyad aliingia ndani ya jengo hilo na akafunga milango kwenye nyuso za watu waliokuwa pale nje. Kufikia hatua hii, ule mkusanyiko ukatawanyika.

Asubuhi iliyofuata, Ubaydullah ibn Ziyad alizungumza na watu akisema: “Damu na mali ya yeote atakayetupinga sisi itakuwa ni halali juu yetu. Ninawataarifu wakuu na machifu wa jumuiya zote kwamba yeote anayefahamu mahali gani walipo maadui wa Yazid na asitujulishe sisi huyo atasulubiwa kwenye mlango wake mwenyewe na malipo yao ya kila mwezi yatasimamishwa. (*Kitab al-Irshaad*)

Imesimuliwa pia kwamba wakati Ibn Ziyad alipoingia Kufah, watu walidhania kwamba alikuwa ni Imam na wakakusanyika kwake wakipiga makelele ya “Tuko pamoja na wewe.” Idadi yao ilisemekana kuwa zaidi ya elfu arobaini. Mwanamke mmoja aliguta kwa sauti: Allah Akbar, Mwenyezi Mungu ni Mkubwa! Ewe mwana wa Mjumbe wa Allah!” Na watu wakaitika kwa mkarara huo huo. (*A’yan al-Shi’ah*)

MPIGA MBIU WA IBN ZIYAD

Wakati taarifa za kuwasili kwa ibn Ziyad na maonyo yake vilipomfikia Muslim ibn Aqil, aliondoka kwenye nyumba ya Mukhtar na kwenda kwenye nyumba ya Hani ibn Urwah ambaye alikuwa kiongozi mashuhuri wa kabile la Madhhij. Hapo Mashi’ah wakaenda kumuona kwa siri.

Ibn Ziyad alimwita mtumishi wake Ma’qal na akampa dirham elfu tatu. Alimwambia amtafute Muslim ibn Aqil na kwenda karibu naye na wafuasi wake, na ili wapate kumuamini katika siri zao, alikuwa awape fedha hizo na awaambie kwamba hizo ni kwa ajili ya

kupigana na maadui zao. Ma'qal aliambiwa amjulishe ibn Ziyad juu ya nyendo zote za Muslim ibn Aqil na watu aliokutana nao. Ma'qal akafanya kama alivyoambiwa kwa kiasi kwamba alikuwa ndiye wa kwanza kufika kwa Muslim ibn Aqil na wa mwisho kuondoka kwenye mkusanyiko wao. Alimuarifu Ibn Ziyad juu ya mambo yote ya Muslim ibn Aqil na wafuasi wake. (*Kitab al-Irshaad*).

USALITI NA KUKOSA UAMINIFU KWA WATU WA KUFAH

Baada ya Ibn Ziyad kuwa amekwisha kupokea taarifa hizo kuhusu Muslim Ibn Aqil, alimwita Hani. Alidai kwamba Hani amkabidhi Muslim kwake. Hani akakataa kufanya hivyo na ibn Ziyad akamtupa gerezani. Pale Muslim alipopata taarifa za kile kilichomkuta Hani, alitambua kwamba hali yake sasa imeingia matatani. Aliwataka watu kumshambulia ibn Ziyad. Watu elfu nne walikusanyika nje ya kasiri la gavana. Ibn Ziyad na msafara wake walibakia ndani na akawaita wakuu wa makabila kuungana naye, kwani tayari alikuwa amekwisha kufanikiwa kuwateka upande wake kwa njia ya hongo. Walianza kujipenyeza mionganoni mwa watu na kuwaambia wajitoe kwa sababu watu wa Syria wangewasili baada ya muda mchache. Baadhi ya jamaa zao wa kikabila waliwaamini na wakajitoa. Wengine walishawishiwa na wake zao na mama zao wenye hofu katika kujitoa.

Kidogo kidogo idadi ya watu waliokuwa kwa Muslim Ibn Aqil ikaanza kupungua. Ilipokuwa ni wakati wa swala ya jioni, Muslim Ibn Aqil alikwenda msikitini na kukuta kwamba kulikuwa na kikundi kidogo tu cha watu wa kuswali pamoja naye. Huu ulikuwa ni msikiti ambao jamaa yake ilikuwa ikififikia idadi ya watu elfu kumi. Wakati Muslim ibn Aqil alipoondoka hapo msikitini, ni watu

kumi tu waliofuatana naye. Kufikia wakati alipowasili kwenye lango la makazi walipoishi kabila la Kindah, kulikuwa hakuna hata mtu mmoja aliyekuwa pamoja naye. Muslim ibn Aqil alifanywa mgeni kabisa katika mji wa Kufah. Alihangaika mitaani akiangalia kulia na kushoto. Alikuwa katika hali ya kuchanganyikiwa kwa kutisha asijue wapi kwa kwenda. Aliingia kwenye uchochoro ambao alikuwa haujui kabisa. Hapo akamkuta mwanamke mzee kwa jina la Taw'ah akiwa amesimama nje ya nyumba yake akimsubiri mwanawe. Muslim ibn Aqil akamuomba mwanamke huyo maji. Alimpatia maji na baada ya kuyanya, Muslim alikaa karibu na mlango wake kwa kuchoka. Ingawa Taw'ah alikuwa ni Shi'ah na mpenzi wa nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hakuweza kumtambua Muslim ibn Aqil. Wakati Muslim alipoketi chini, yeze akamwambia kwamba ilikuwa haifai kwake yeze kukaa pale. Aliposikia hivyo, Muslim ibn Aqil akasema: "Ewe mtumishi wa Mwenyezi Mungu! Mimi sina mahali pa kuishi. Je, utaniruhusu nikae ndani ya nyumba yako kwa usiku huu? Mwenyezi Mungu akipenda mimi nitalipa deni hilo." "Wewe ni nani?" Taw'ah aksauliza. "Mimi ni Muslim ibn Aqil, watu hawa waliniita na kunikaribisha mimi hapa. Sasa wamenitelekeza na kunifukuzilia mbali." Alipojua kwamba bwana yule ndiye Muslim ibn Aqil, Taw'ah akamkaribisha ndani ya nyumba.

Aliporudi nyumbani Bilal mtoto wa Taw'ah, aliulizia kuhusu mgeni huyo. Taw'ah alimtaka achukue kiapo kwamba hatamwambia yoyote kuhusu mgeni wao huyo wala kuhusu mahali alipo. Kisha bila kuhiarri na kwa moyo mzito kabisa akamwambia kwamba huyo alikuwa ni Muslim ibn Aqil. Bilal alikaa ndani ya nyumba hiyo usiku huo lakini asubuhi iliyofuatia alikwenda kwa Abdur-Rahman ibn Muhammad ibn Ash'ath na kumfahamisha mahali alipokuwepo Muslim ibn Aqil. Abdur--Rahman alikwenda kumjulisha baba yake Muhammad ibn Ash'ath juu ya habari hizi. Huyu Muhammad ibn

Ash'ath, mkuu wa kabilia la Kindah alikuwa ni mshirika wa karibu sana wa Ibn Ziyad na ambaye alikwenda moja kwa moja kwa Ibn Ziyad na kumjulisha juu ya mahali alipokuwepo Muslim ibn Aqil.

Mara moja tu Ibn Ziyad akamuamuru Muhammad ibn Ash'ath kumkamata Muslim ibn Aqil na kumleta kutoka kwenye nyumba ya Taw'ah. Muhammad ibn Ash'ath akatoka kwenda nyumbani kwa Taw'ah pamoja na Amr Ubaydullah ibn Abbas al-Sulami wakiwa na askari sabini.

Wakati wa usiku huo, Taw'ah alikuwa ameleta chakula cha usiku kwa ajili ya Muslim ibn Aqil, lakini alikuwa amekataa kula kitu chochote kile. Alikuwa amelala kwa muda mdogo tu na kisha akawa ameamka kuupitisha usiku uliobakia katika swala na maombi. Alfajiri ilipokuwa inakaribia, Taw'ah alileta maji kwa ajili ya Muslim kuchukulia Udhuu kwa ajili ya swala. Akamwambia: “Bwana wangu! Wewe hukulala usiku mzima wote.” Muslim ibn Aqil akajibu, “Nililala kidogo na katika usingizi wangu nilimuona ami yangu Amirul-Mu’minin. Alikuwa ananiambia, ‘O Muslim! Harakisha na uje kwetu haraka sana.’ Nahofia kwamba siku ya mwisho ya uhai wangu imekaribia.” Kisha Muslim akachukua udhuu.

Baada ya kuwa amemaliza swala na alikuwa akiomba du'a, alisikia sauti za askari wanaokuja. Muslim ibn Aqil haraka sana akamalizia du'a zake na akaanza kuvaa nguo zake za kivita huku akisema: “Nenda ukakabiliane na kifo ambacho hakina namna ya kukwepa.” Taw'ah akamuuliza, “O Bwana! Je umejitolea kufa?” “Sina namna ya kutoroka isipokuwa kifo tu. Mtume wa Mwenyezi Mungu akuombee shufaa kwa fadhila ambazo umeonyesha,” alijibu Muslim ibn Aqil.

Kundi la kufikia hadi askari mia tatu lililazimisha kuingia ndani ya nyumba hiyo ya Taw'ah ili kumkamata Muslim ibn Aqil, ambaye

alikamata upanga wake mkononi na akawarudisha nyuma hadi mtaani. Alipotazama juu, Muslim aliona kwamba baadhi ya askari wamepandajuu ya mapaa ya nyumba za jirani na walikuwa wanarussha mawe na mienge ya moto kwenye nyumba hiyo. Akiogopea kwamba wapiganaji hao wataichoma nyumba hiyo, alijitokeza nje na kwenda kupigana nao. Muslim ibn Aqil alipigana peke yake ingawa alikuwa amezungukwa na alikuwa anabanwa kutoka kila upande. Inasimuliwa kwamba wakati alipokuwa anapigana, Muslim ibn Aqil aling'oa mlango wa nyumba hiyo na kuutumia kama ngao yake. Alipigana kwa ukali na bidii sana kiasi kwamba aliwaua wapiganaji mia moja na themanini katika wale waliokuwa wamepanda farasi.

Katika nyakati mbili, Muhammad ibn Ash'ath alilazimika kutuma ujumbe kwa ibn Ziyad ili kupata msaada wa nyongeza. Katika nyakati zote hizo, Ibn Ziyad aliitikia kwa kutuma askari. Katika ombi la mara ya tatu, Ibn Ziyad alijibu: "Mama yako alie kwa huzuni ya kifo chako! Yaani huwezi kumshinda mtu mmoja tu? Kitatokea nini iwapo utakabiliana na adui mwenye nguvu kushinda yeye?" Kwa usemi huu yeye alimaanisha Imam (a.s.). Hapa Muhammad ibn Ash'ath akajibu, "Wewe hutambui kwamba bwana huyu ni upanga wa Mtume, simba jasiri na mpiganaji, na wala sio mkulima au muuza duka wa Kufah?" Ibn Ziyad akatuma wapiganaji wengine mia tatu pamoja na maagizo kwamba Muhammad ibn Ash'ath atoe kibali cha ahadi ya salama kwa Muslim ibn Aqil ili kuweza kusalinisha uhai na maisha ya watu wake.

(Maqtal al-Husayn Abu Mikhnaif)

Muslim ibn Aqil alikuwa anaendelea kupigana kishujaa katikati ya mapambano makali, Muhammad ibn Ash'ath akamuuta tena kwa sauti, Ewe Muslim! Usijiangamize mwenyewe. Sisi tunakupa kibali cha usalama. Simamisha mapigano. Muslim ibn Aqil hakushawishika

na akaendelea kupigana. Muhammad ibn Ash'ath akaita tena, “Ewe Muslim! huu sio uongo au mtego wa kijanja. Huyu ni mwana wa ami yako (akimaanisha ibn Ziyad) na ametoa ahadi yake kwamba hakuna madhara yatakayokufika wewe.”

Muslim ibn Aqil sasa akawa amefunikwa na majeraha kutokana na urushwaji wa mawe wa mishale mfululizo. Kutokana na kuchoka sana alisitisha ili kupumzika na akaka chini mgongo wake ukielekea kwenye ukuta wa nyumba ya Taw'ah. Kwa mara nyingine tena Muhammad ibn Ash'ath alimgutia na kumtaka Muslim aache kupigana na achukue lile pendekezo la kibali cha usalama. Hapo Muslim ibn Aqil akauliza: “Ni kweli mtayaacha maisha yangu?” “Ndio, maisha yako yatahifadhiwa,” lilikuja jibu kutoka kwa wenyeji waliokuwa wamemzunguka.

Muslim ibn Aqil alikuwa hana nguvu tena za kupigana na akalazimika kukubali lile pendekezo la kibali cha usalama. Akale twa nyumbu kwa ajili yake. Haikuchukua muda baada ya kumpanda nyumbu huyo, wale askari wakamzingira na kuchukua upanga wake na wakamfanya kuwa mateka wao. Machozi yalitiririka kwenye mashavu yake matukufu wakati akisema: “Huu ndio udanganyifu wa kwanza.”

(*A 'lam al-wara'*)

MAKABILIANO YA MUSLIM BIN AQIL NA IBN ZIYAD

Wakati Muslim ibn Aqil alipoletwa pale kwenye kasri kama mateka, hakumsalimia Ibn Ziyad kwa yale maamkizi ya amani. Yule mlinzi aliye kuwa amesimama hapo langoni akamwambia Muslim ibn Aqil:

“Msalimie kamanda na mkuu.” Muslim ibn Aqil akajibu: “Kimya! Huzuni na iwe juu yako! Huyu sio kamanda wangu mimi.”

Hapo ibn Ziyad akasema: “Yote ni mamoja, unisalimie au usinisalimie. Wewe utaadhibiwa kifo.” Muslim ibn Aqil akarudisha maneno makali: “Haitakuwa mara ya kwanza, yule muovu zaidi yako ameua mbora kuliko mimi.” Ibn Ziyad akaguta: “Ewe mpinzani sugu! Umeasi dhidi ya mtawala na ukasababisha vurugu na mfarakano ndani ya jamii.” Muslim ibn Aqil akajibu: “O Ibn Ziyad! Alikuwa ni Mu’awiyyah na mwanawe Yazid ambao wameleta mfarakano ndani ya jamii na ilikuwa ni wewe na baba yako ambao mmeeneza dhulma ndani yake. Ni matarajio yangu kwamba Mwenyezi Mungu atanijaalia kifo cha Shahada kwa mikono ya muovu kabisa kati ya viumbe Wake.” Ibn Ziyad alimuasa akasema: “Mlikuwa mkitamani jambo (yaani Ukhilifa) ambalo Mwenyezi Mungu hakulikamilisha kwenu bali akaliweka kwa watu wanaostahiki hilo.” Muslim ibn Aqil akauliza, “Ewe ibn Ziyad! Na ni nani anayelistahiki hilo?” Ibn Ziyad akajibu: “Yazid bin Mu’awiyyah.” Muslim akasema: “Sifa zimwendee Mwenyezi Mungu! Sisi tumeridhika na radhi Zake! Yeye na atuamulie kati yenu na sisi!” Ibn Ziyad akiwa katika hali ya kukasirika sasa, alimtukana Muslim ibn Aqil, Imam Ali, Imam Hasan na Imam Husein. Kwa hili Muslim ibn Aqil akajibu: “Ewe adui wa Mwenyezi Mungu! Fanya utakalo. Wewe na baba yako ndio mnaostahiki matusi haya.”

Ibn Ziyad akamuamuru Bukayr ibn Humran ampeleke Muslim ibn Aqil hadi juu kabisa ya kasri hilo na amkate kichwa chake. Wakati Muslim ibn Aqil alipokuwa anaongozwa kuelekea kwenye kuuliwa kwake, alimsifu na kumtukaza Mwenyezi Mungu na akaomba rehema na amani Yake juu ya Mtume na kizazi chake (a.s.) akisema: “Ewe Allah! Wewe uwe ndiye hakimu wa mwisho kati yetu na watu hawa ambao wametuita sisi, wakatudanganya na kutusaliti sisi.”

Mapema kabla siku ile Bukayr ibn Humran aliwahi kuwa mmoja wa watu waliopigana dhidi ya Muslim Ibn Aqil. Katika mapambano hayo, Muslim alikuwa amemshambulia kwa pigo kali sana na akamjeruhi. Hivyo alikuwa amejawa na chuki sana juu ya Muslim na akaonyesha kutokuwa na huruma kabisa vile alipokuwa akitekeleza amri za ibn Ziyad. Alimchukua hadi kwenye paa la kasiri hilo na akamuamuru apige magoti na achomoze kichwa chake kwenye ukingo wa ukuta wa kasiri hilo. Kisha bila ya huruma japo kidogo akamkata kichwa chake. Pale shoka ilipogawa shingo yake, kichwa cha Muslim ibn Aqil kikadondoka kutoka juu ya kasri hilo hadi chini ardhini. Baada ya tukio hili, askari waliamrishwa kuutupa mwili wake chini ardhini. Kwa njia hii roho iliyobarikiwa ya Muslim ibn Aqil ikatoka kwenye kiwiliwili chake kilichojeruhiwa na kwenda kwenye Furaha isiyo na Kifani ya Milele na kwenye makazi ya Akhera.

(Al-Luhuf & A'lam al-Wara')

WOSIA WA MWISHO NA OMBI LAKE MUSLIM BIN AQIL

Yafuatayo ni maelezo ya makabiliano ya mwisho ya Muslim ibn Aqil na ibn Ziyad kama yalivyoelezwa ndani ya *Kitab al-Irshaad*: Muslim ibn Aqil alikuwa na kiu kali kabisa wakati alipoletwa kwenye kasri hilo. Kundi la watu lilikuwa limesimama nje ya mlango likisubiri kuingia ndani. Akiwa amesimama pamoja nao ni Amr ibn Hurayth na karibu na mlango lilikuwa limewekwa gudulia la maji. Muslim ibn Aqil alimuomba Amr ibn Hurayth maji kidogo wakati alipokaa chini akiegemeza mgongo wake kwenye ukuta. Amr ibn Hurayth alimuamuru mtumishi wake ampatie Muslim maji. Maji yaliletwa kwake lakini wakati alipajaribu kuyanywa, ile damu iliyokuwa ina-

tona kutoka kinywani na kwenye midomo yake ilijojeruhiwa ilim-wagikia kwenye maji hayo. Maji mapya yaliletwa na yakatokea yale yale. Mara ya tatu wakati Muslim alipojaribu kunywa maji hayo, meno yake ya mbele yalidondokea ndani ya chombo. Muslim Ibn Aqil aliyatema maji hayo na akasema: “Sifa zote zinamstahiki Allah! Kama riziki ingekuwa imetengwa kwa ajili yangu, basi kwa hakika ningeweza kuyanya maji haya.”

Watu wa Ibn Ziyad walimpeleka Muslim kwake na baada ya kutupiana maneno ibn Ziyad kwa ukatili na ufidhuli akasema: “Kwa hakika wewe utauliwa tu.” Muslim ibn Aqil akajibu akasema: “Kama umedhamiria kuniua basi niruhusu nitengeneze wasia wangu wa mwisho.” Ibn Ziyad akakubali kwamba Muslim ibn Aqil anaweza kufanya hivyo.

Muslim ibn Aqil alimwita Amr Sa’d ambaye alikuwa amesimama karibu naye akamwambia: “O Ibn Sa’d! kuna udugu kati yetu sisi. Kwa sababu hiyo nakuomba unipe kiapo cha usiri na uheshimu wasia wangu wa mwisho.” Ibn Sa’d akakataa kumsikiliza. Kuona hivi Ibn Ziyad akamuamuru ibn Sa’d: Msikilize binamu yako anachotaka kukisema.”

Chini ya uangalizi wa macho ya Ibn Ziyad, Ibn Sa’d akamwendea Muslim ibn Aqil na wote wawili wakajitenga pembeni ambako walikaa chini. Muslim ibn Aqil akamwambia: “Nilikopa dirham mia saba ndani ya Kufah. Uza deraya yangu ya vita na upanga wangu na ulilipe deni hilo. Baada nikisha kuuawa, tafadhali chukua mwili wangu kutoka kwa Ibn Ziyad na ukanzike. Mtumie habari Imam Husein kwamba asije tena mjini Kufah. Nimetuma barua kwake kumfahamisha ye ye kuhusu uaminifu wa watu wa Kufah na shauku yao ya kuongozwa na ye ye. Nahofia kwamba atakuwa ameanza safari yake ya kuja Kufah.”

Akiogopa kwamba ibn Ziyad atamtilia shaka kuhusu jambo fulani, alimwendea na kumjulisha yeye kuhusu wasia wa mwisho wa Muslim ibn Aqil. Ibn Ziyad akamsuta ibn Sa'd kwa vitendo vyake na akasema mdhamana haisaliti siri wakati inapodhaminiwa kwake. Kwa hili alimaanisha kwamba kama ibn Sa'd angekuwa mtu wa kuaminika, kamwe asingefichua kile Muslim alichokuwa amemwambia yeye kwa siri na kumuamini. Hata hivyo, licha ya hayo alimuamuru ibn Sa'd: “Na juu ya deni hilo, ulilipe baada ya kufa kwake kama ukitaka. Na kuhusu mazishi yake, hayo pia nitakuruhusu kama utapenda kumzika. Lakini kwa kiasi anachohusika al-Husein, sisi hatuna ugomvi naye kama tu hatatuingilia.

Kisha ibn Ziyad akamgeukia Muslim ibn Aqil na akaanza kumtukana. Baada ya kurushiana maneno makali ambamo Muslim alishutumiwa kwa kufarakanisha watu, Ibn Ziyad akamwambia Muslim: “Unahusika nini umoja wa watu na wewe. Kwa nini hukujishughulisha nao wakati ulipokuwa unakunywa pombe na watu huko Madina?” Kwa hili Muslim akamjibu kwa maneno makali: “Wallahi unadanganya! Wewe, ambaye unalalamba damu ya Waislam na kuwauwa wale ambao maisha yao Mwenyezi Mungu ameyachukulia kuwa matakatifu ndiye unayeelezeka vizuri zaidi kama mlevi wa pombe na sio mimi.” Ibn Ziyad hakuweza tena kujizua mwenyewe na akaamuru Muslim Ibn Aqil akatwe kichwa chake na mwili wake utupwe kutokea pale juu kwenye ghorofa ya kasri hadi chini ardhini. (*Kitab al-Irshaad*)

SHAHADA YA HANI IBN URWAH

Hani ibn Urwah amekwishatajwa hapo kabla kwamba ndiye mtu ambaye Muslim ibn Aqil alikwenda kukaa kwake baada ya kuwasili kwake mjini Kufah. Alikuwa mmoja wa watu mashuhuri mionganii

mwa Shi'ah na alikuwa anatokana na kabilia la Madhhij. Kwa mujibu wa riwaya moja, Hani Ibn Urwah alishuhudia zama za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na anahesabiwa kama mmoja mionganini mwa masahaba zake. Wakati wa kuuliwa kwake, alikuwa na umri wa miaka themanini na tisa. Kwa mujibu wa Ya'qubi, Hani alikuwa na hadhi kubwa sana kijamii na alikuwa na wapiganaji elfu nne wa vipando na wapiganaji wa miguu elfu nane chini ya udhibiti wake. (*Muntaha al-Amal*).

Kama ilivyoelezwa, Hani alitoa nyumba yake ipate kutumiwa na Muslim na alimuunga mkono na kumsaidia. Hani alikamatwa na ibn Ziyad na akawekwa kizuizini wakati alipokataa kumkabidhi Muslim Ibn Aqil. Baada ya kifo cha Muslim ibn Aqil, Ibn Ziyad alimwamuru mtumishi wake Rashid kwenda kumkata kichwa chake Hani ndani ya soko. Kwa mujibu wa Muthir al-Ahzan, mzee huyo wa miaka themanini na tisa aliburuzwa hadi Uwanja wa Kunasah ambako aliuliwa na baadaye akatundikwa kwenye mlango.

Kwa mujibu wa riwaya iliyosimuliwa na Sayyid Ibn Tawus, Hani aliburuzwa kutoka gerezani hadi sokoni ili akauliwe. Alirudia rudia kupiga ukelele, “Enyi kabilia la Madhhij! Kwa nini hamji kunisaidia?” Hapa muuaji wake, Rashid, Mturuki ambaye ni mtumishi wa nyumbani wa ibn Ziyad alimuamuru Hani kujipanga sawa mwenyewe kwa ajili ya kuuliwa kwake. Hani akamjibu kwa ukali: “Wallahi sitakusaidia katika kuniuwa kwako mimi.” Rashid alimpiga Hani dharuba kichwani mwake lakini haikuweza kumuua. Hani alipiga ukelele wakati alipokuwa anaanguka kuelekea ardhini.

Kwa Mwenyezi Mungu ndiko marejeo ya mwisho! Ewe Allah! mimi ninarejea kwenye rehema na radhi Yako.” Rashid akamkata tena Hani na kichwa chake kilichobarikiwa kikatenganishwa na pingili la mwili wake.

Ibn Ziyad alivipeleka vile vichwa vya Muslim ibn Aqil na Hani ibn Urwah vilivyokatwa kwenda kwa Yazid pamoja na barua ikielezea hali halisi ya Kufah. Yazid aliandika kumjibu Ibn Ziyad akimshukuru na akimuagiza ajiandae kwa ajili ya kufika kwa Imam Husein (a.s.). Yazid vile vile akaagiza vichwa hivyo vitundikwe kwenye lango la mji wa Damascus.

Abdallah ibn Zubeir aliandika beti zifuatazo kuhusu Muslim ibn Aqil na Hani ibn Urwah:

“Kama hujui kifo ni kitu gani,

basi muangalie Hani na Ibn Aqil ndani ya soko.

“Mwangalie shujaa ambaye uso wake upanga umeufunika na majeraha,

na mwingine ambaye alianguka akiwa mfu kutoka mahali pa juu mno.

“Amri ya gavana imewaangusha chini,

na wamekuwa ni hadith ya kale kwa wanaotembea katika kila barabara.

Unaiона maiti ambayo rangi yake, kifo kimeibadilisha,

na mtapanyo wa damu ambayo imemwagika kwa wingi.

(*Kitab al-Irshaad*)

Watu wawili, Aradil na Awbash waliifunga ile miili miwili isiyo na vichwa ya Muslim Ibn Aqil na Hani Ibn Urwah nyuma ya farasi wao kwa kamba na kuiburaza kwenye mitaa ya Kufah. Kabilia la Madhhaj, baada ya kutambua kuhusu kifo cha Hani Ibn Urwah na Muslim Ibn Aqil walipanda farasi wao na wakapigana na Aradil

na Awbash mpaka wakaipata ile miili miwili. Kisha wakaiosha, wakaikafini na kuizika miili yao hiyo.

(*Ma 'ali al-Sibtayn*)

Mshairi wa Kiarabu anaghani katika maombolezo ya Muslim Ibn Aqil:

“Waliutupa mwili wako kutoka kwenye kasri baada ya kukufunga.

Je, kuna kiungo chochote kilichobakia kamili?

“Ulfungwa na kuburutwa mitaani kwao.

Hukuwa wewe ni jemedari wao hadi jana?

“Utakufa wewe bila ya wanawake wapigao mayoe kulia kwa ajili yako?

Hivi huna mtu wa kukulilia katika mji huu?

“Hata kama umeuliwa kikatili, vilio vyta huzuni vilisikika.

Wakati taarifa za kifo chako zilipowafikia (watu wa) Zarud.

Imesimuliwa vilevile kwamba Ibn Ziyad aliamuru miili hiyo ya Muslim na Hani isiyo na vichwa ifungwe kwenye miguu yao na kuburuzwa kupitia kwenye mitaa. Kisha miili yao ilitundikwa juu chini kwenye lango la Kunasah na vichwa vyao vilipelekwa kwa Yazid. Yazid aliamuru vichwa hivyo vitundikwe kwenye malango ya Damascus.

(*Maqtal al-Husein al-Muqarram*)

MSIBA WA WALE WATOTO WAWILI WA MUSLIM BIN AQIL

Muslim Ibn Aqil aliondoka pamoja na watoto wake wawili wa kiume kwenda Kufah. Mtoto mkubwa aliitwa Muhammad na yule mdogo aliitwa Ibrahim. Wote walikuwa na umri chini ya miaka kumi. Wakati Muslim alipotambua jinsi ibn Ziyad alivyokuwa mtu hatari na tishio kubwa, alimwita Qadhi Shurayh na kumkabidhi watoto wake wawili hawa. Qadhi Shurayh aliwaweka vijana hao wawili nyumbani kwake mpaka siku ya kuuliwa kishahidi kwa Muslim ibn Aqil.

Baada ya kifo cha Muslim ibn Aqil, ibn Ziyad alitoa onyo akisema kwamba yejote yule anayejua mahali walipo watoto wa Muslim ibn Aqil na akawa hakumfahamisha yeye, basi atamuua. Katika kulisikia hili, Qadhi Shurayh aliwaenda watoto hao wa Muslim ibn Aqil. Aliwaonyesha upendo na huruma wakati yakimtoka machozi. Watoto hao wakamuuliza: “Kwa nini unalia?”

Shurayh akajibu, “Baba yenu ameuliwa kikatili mno.” Watoto wale wakalia kwa huzuni sana. “Ewe baba! Oh uhamisho! Baada ya Shurayh kuwaliwaza, aliwajulisha juu ya tishio la ibn Ziyad dhidi yao. Waliposikia hili, wale watoto wakanyamaza kulia kwa kuhofu. Alipoona hivi, Shurayh akasema: “Msiwe na hofu. Ninyi ni matufaha ya macho yangu. Sintaruhusu hatari yoyote kuwafikeni ninyi. Mimi nimeandaa kwa ajili yenu kuwa chini ya uangalizi wa mtu mwaminifu sana ambaye atahakikisha kwamba mnarudishwa Madina.”

Shurayh alimwita mwanawe Asad na kumpa maelekezo yafuatayo, “Zimenifikia habari kwamba kuna msafara unaojiandaa kwenda Madina. Wachukue watoto hawa na ukawakabidhi kwa mtu mwaminifu ambaye atahakikisha kwamba wanafika Madina salama

salimin.” Shurayh akawabusu vijana hawa na akawapa kila mmoja wao dinari 50. Kisha akaagana nao na akawakabidhi kwa mwanawe Asad.

Katika giza la usiku, Asad aliwabeba vijana hawa wawili mikononi mwake mpaka alipokuwa yuko kilomita chache nje ya mji wa Kufa ili kukutana na msafara huo. Hata hivyo ikawa kwamba msafara huo ulikwisha kuondoka kabla wao hawajafika pale. Maumbo meusi ya msafara huo yalikuwa yanaonekana kwa mbali kidogo. Asad aliwaaga vijana mayatima hao wa Muslim Ibn Aqil na akawaambia waukimbilie ule msafara mpaka waukute. Kwa mazingira yoyote yale wao wasisimame mpaka watakapokuwa wamekutana na msafara huo.

Katika giza hilo la usiku, watoto hao yatima walianza kukimbia kukatisha ndani ya jangwa kuulekea msafara huo. Hata hivyo uchovu uliwazidi na wakapumzika kwa kitambo kidogo. Ilikuwa ni wakati huu ambapo mkazi mmoja wa Kufah alitokea kupita eneo hilo. Aliwaona watoto hao na akawatambua kwamba ni wale mayatima wa Muslim ibn Aqil. Aliwakamata na kuwachukua hadi kwa ibn Ziyad.

Ibn Ziyad alimwita bwana jela na akawakabidhi watoto hao kwake. Bwana jela huyo alikuwa ni mtu anayeitwa Mashkur na alikuwa ni mmoja mionganini mwa wapenzi wa Ahlul-Bayt (a.s.), nyumba ya Mtume (s.a.w.w.). Wakati Mashkur alipouelewa utambulisho wa vijana hawa wawili, aliwashughulikia kwa upole na upendo mwingi mno na akawaletea chakula na maji. Hatimae katikati ya usiku huo Mashkur aliamua kuwaachia huru vijana hao. Aliwapa pete yake na akawaelekeza waende Qadisiyyah ambako watamkuta ndugu yake. Aliwaambia kwamba wampe huyo kaka yake pete hiyo ambaye baada ya hapo atawasaidia namna ya kufika Madina. Habari za Mashkur kuwaachia watoto hao zilipomfikia ibn

Ziyad, aliamuru achapwe mijeledi hamsini. Mashkur alifariki wakati adhabu hiyo ilipokuwa ikitekelezwa juu yake.

Katika usiku huo huo, Ibrahim na Muhammad, wale watoto wa Muslim Ibn Aqil waliondoka mjini Kufah na kuanza safari ya kuelekea Qadisiyyah. Walitembea usiku kucha. Hata hivyo kutokana na giza la usiku na ule ukweli kwamba hawakuwa wakijua njia, walijikuta bado wakiwa kwenye viunga vya mji wa Kufah wakati wa asubuhi yake. Vijana hao wenyе hofu waliona shamba la mitende na wakaliendea. Hapo walijificha juu ya mti wa mtende.

Mtumishi wa Kihabeshi aliingia kwenye shamba hilo la mitende kwenda kunywa maji kutoka kwenye dimbwi chini ya mtende ambamo vijana hao walikuwa wamejificha. Pale mtumishi huyo alipoinama karibu na dimbwi hilo aliona vivuli vya vijana hao wawili ndani ya maji hayo. Mtumishi huyo haraka sana alitazama juu ya mti huo na akawaona vijana hao wadogo wakiwa wamejificha humo. Aliwatendea kwa huruma na upole na akawapeleka kwa bibi mmiliki wake ambaye alikuwa ni mke wa Harith ibn Urwah. Mara tu mwanamke huyu alipowaona aliweka mikono yake kuwazunguka na akawaauliza wao walikuwa ni akina nani. Wao wakajibu wakasema: “Sisi tunatoka kwenye familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ni watoto wa Muslim Ibn Aqil.” Pale alipogundua utambulisho wao halisi aliwaonyesha upendo mkubwa sana na bibi huyu akamkumbatia yule mtumishi wake kwa furaha. Hata hivyo alimuonya kwamba asije akamjulisha mume wake Harith kuhusu vijana hao kwa sababu ye ye aliujua vizuri uovu wa mume wake.

Baada ya watoto hao kuwa wamekwisha kula na kwenda kulala, Harith alirudi nyumbani akiwa katika hali ya kukasirika. Wakati mke wake Harith alipomuuliza ye ye sababu ya hasira zake, ye ye alijibu kwamba alikuwa katika msako wa watoto wawili wa Muslim Ibn Aqil ambao wameachiwa huru na Mashkur ambaye ni bwana

jela. Alisema kwamba ilikuwa imetangazwa ndani ya kasri kwamba atakayewakamata watoto hao atalipwa unono kabisa. Hata hivyo licha ya katika kipindi kirefu cha usakaji wake ambamo farasi wake alikufa kwa uchovu na ambamo yeye binafsi amechoka kabisa, bado hakuweza kuwaona vijana hao. Kwa haya, mkewe Harith akasema: “Huzuni naiwe juu yako! Muogope Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho ambamo Muhammad mjambe wa Mwenyezi Mungu atakuwa adui yako. Usiwadhuru watoto wale.” Harith akajibu: “Kimya! Ewe mwanamke! Kama ningekuwa niwaone hao watoto, ningezawadiwa kwa kiwango kikubwa cha dhahabu na fedha kutoka kwa ibn Ziyad. Hebu nyanyuka uandae chakula changu cha jioni.”

Baada ya kula chakula chake, Harith alikwenda kitandani kwake. Muhammad na Ibrahim walikuwa wamelala katika moja ya vyumba humo. Ghafla Muhammad, yule kijana mkubwa kati ya wawili hao aliamka kutoka usingizini. Alipata ndoto ambayo ilimsumbia. Alimwambia Ibrahim: “Amka! Ewe ndugu yangu! Ni punde tu nimeota ndoto na nahofia kwamba tutauawa hivi karibuni. Nimemuona Mtukufu Mtume pamoja na Imam Ali, al-Hasan, al-Husein na Bibi Fatima wakiwa wamekaa huko Peponi pamoja na baba yetu. Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alitutazama sisi kisha akalia. Halafu akamgeukia baba yetu na akasema: “Oh Muslim! Umewezaje kuwaacha wanao miongoni mwa maadui?” Kwa hili baba yetu akasema kwamba wataungana nasi kesho.”” Ibrahim akajibu, “Na mimi nimekuwa na ndoto hiyo hiyo.” Watoto hao wakakumbatiana wenyewe katika giza hilo la usiku, wakiwa na hofu na wasijue ni lipi litakalowatokea.

Harith aliamshwa kutoka usingizini na sauti za watoto hao. Akishikilia taa aliingia ndani ya chumba hicho na akawaona watoto hao wawili wenye hofu wakiwa wamekaa kwenye pembe ya chumba wakiwa wameng’ang’niana. Yeye akauliza: “Ninyi ni akina nani?”

Wao wakajibu: “Sisi ni wageni wako, familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Sisi ni watoto wa Muslim Ibn Aqil.” Harith akapiga kelele kwa hasira, “Nimejiangamiza mimi mwenyewe na farasi wangu katika msako wenu wakati ninyi mmekaa ndani ya nyumba yangu mwenyewe?”

Harith akaanza kuwapiga makofi watoto hao kwa ukali na nguvu kabisa. Kisha akawafunga mikono yao na miguu na akawasukumiza kwenye pembe ya chumba. Mkewe Harith alimjia na akambusu mikono yake na miguu akimsihi na kumuomba asiwadhuru watoto hao ambao walikuwa ni mayatima na kutoka kwenye familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na ni wageni wao. Hata hivyo bwana huyu mwenye roho ngumu alikuwa hana huruma hata kidogo na hakujali maombi yake. Hivyo watoto hao waliachwa katika hali hiyo mpaka asubuhi yake.

Hapo asubuhi, Harith akiwa na upanga wake mkononi na akifuatana na mwanawe wa kiume na mtumishi wake, aliwachukua watoto hao wa Muslim ibn Aqil hadi kwenye kingo za mto Furati. Mke wa Harith alikuwa analia huku akimsihi wakati akiwafuata nyuma yao. Hata hivyo, kila alipowafikia karibu Harith alimsukuma kwa upanga wake. Hapo kwenye mto Furati Harith alimpa mtumishi wake ule upanga wake na akamuamuru kuwakata vichwa watoto hao. Mtumishi wake akakataa kutekeleza amri yake na Harith akamuua yeye. Baada ya hili Harith alimkabidhi mwanawe upanga huo na kumwambia awakate vichwa vijana hao wawili. Hapo mwanawe akajibu: “Najikinga kwa Mwenyezi Mungu! Kamwe sitatenda jinai kama hiyo na sitakuruhusu kuwauwa vijana hawa.” Mke wa Harith akaguta, “Ni dhambi gani wamefanya watoto hawa? Wapeleke kwa gavana wakiwa hai.” Harith akajibu: “Mimi sina uchaguzi bali kuwauwa hawa, sina uhakika kwamba Mash’ah hawatawaokoa kutoka kwangu wakati nikitafuta njia yangu kuelekea kwa gavana.”

Hapa Harith akachukua upanga wake kwa madhumuni ya kumuua mwanawe mwenyewe. Mke wake akapiga kelele na kumuomba awe na huruma lakini bila mafanikio yoyote. Harith akatoa uhai wa mwanawe mwenyewe. Kisha akawageukia wale vijana wawili ambaao walikuwa wanalia huku wakitetemeka kwa hofu ya kile walichokishuhudia. Watoto hao wakaomba wapate muda kidogo ili wafanye swala zao za mwisho lakini Harith hakuwakubalia matakwa yao. Harith akamkamata Muhammad lakini Ibrahim akajirusha mwenyewe juu ya Muhammad katika jaribio la kumuokoa yeye. Muhammad naye akafanya vivyo hivyo ili kuokoa maisha ya ndugu yake. Kwa kukosa subira Harith akampiga upanga Muhammad na kumkata kichwa chake. Ibrahim akakidaka kichwa cha kaka yake mapajani mwake. Alivyokuwa anaulilia mwili wa kaka yake, Harith alipiga upanga shingo ya Ibrahim na kukata kichwa cha yatima huyo.

Harith akaitupa ile miili isiyo na vichwa ya mayatima wa Muslim ibn Aqil ndani ya mto Furati na akaweka vichwa vyao kwenye kiguzo na akaondoka kuelekea kwenye kasri la ibn Ziyad.

Vichwa hivyo vya yatima wa Muslim Ibn Aqil vililetwa na kuwekwa mbele ya Ibn Ziyad. Yeye Ibn Ziyad akauliza: “Hivi ni vichwa vya akina nani?” Harith akajibu: “Hivi ni vichwa vya wale maadui zako ambaao mimi niliwakamata na kuwakata vichwa kwa ajili ya malipo ya zawadi ambayo umeahidi kutoa.” Ibn Ziyad akauliza: “Maadui zangu gani hao?” Harith akajibu: “Wale watoto wawili wa Muslim Ibn Aqil.” Ibn Ziyad akaagiza vichwa hivyo visafishwe na viletwe ndani ya sinia. Kisha akavitazama na akamwambia Harith: “Huzuni iwe ndio malipo yako! Ni kosa gani walilokutendea watoto hawa?

Ibn Ziyad akamwita mcheshi wake binafsi Muqatil ambaye alikuwa ni mpenzi mwaminifu wa Familia hiyo Tukufu na kukataa kifo cha muuaji huyo kuwa mikononi mwa askari wake akasema:

“Mtu huyu aliyelaaniwa amewauwa watoto hawa bila ruksa yangu. Mchukue hadi kwenye kingo za mto Furati ambako aliwauwa watoto hawa na umhukumu kifo kama utakavyopenda.” Muqatil alimkamata Harith mabegani na akampitisha kwenye mitaa ya Kufah bila viatu na kichwa wazi huku akiwa anavionyesha vichwa vyta mayatima wawili wa Muslim Ibn Aqil kwa watazamaji huku akiguta: “Enyi watu! Huyu ndiye muuaji wa mayatima wawili wa Muslim Ibn Aqil.” Watu wakalia sana kwa kuona vichwa vyta yatima hao na kumlaani Harith. Vile Muqatil alivyokuwa akielekea kwenye mto Furati, watu walikusanyika pamoja naye kwenda kushuhudia kuuliwa kwa Harith. Walipowasili pale mahali ambapo aliwauwa watoto hao, walikuta maiti ya mtoto wake Harith na mtumwa wake na mkewe mwenye michubuko akilia karibu na mwili wa mwanawe. Watu walichanganyikiwa sana kwa mandhari haya.

Harith alimuomba Muqatil amwache huru kwa thamani ya dinari elfu kumi.

Juu ya hili, Muqatil akajibu: “Wallahi! Kama utajiri wote wa dunia nzima ungekuwa ni wako na ukautoa kunipa mimi, wala nisingekubali. Natamani kuipata Pepo ya Mwenyezi Mungu kwa kukuuwa wewe.” Muqatil akamkata mikono yake na miguu. Kisha akamkata masikio na pua yake na akapasua matumbo yake. Baada ya hayo watu wakauchoma mwili wake. (*Ma’ali al-Sibtayn*)

MLANGO WA TATU

SAFARI YA KUTOKA MAKKA KWENDA KARBALA

KUONDOKA MAKKA KWA IMAM HUSEIN (A.S.)

Kama ilivyoelezwa mapema, Imam Husein (a.s.) na wafiasi wake waaminifu waliondoka Madina mnamo mwezi 28 Rajab, 60 A.H. na kuwasili Makka mnamo mwezi 3 Shaaban mwaka huo huo. Imam na wafiasi wake walikuwa wakati wote wakikutana na watu hapo mjini Makka na kuwajulisha juu ya upinzani wao dhidi ya serikali dhalimu ya Yazid. Baada ya kutambua kuhusu hatari ya kuuliwa au kutekwa na majasusi waliotumwa na Yazid kama mahujaji kwenye Nyumba ya Allah swt. ye ye alibadilisha nia yake ya kufanya hijja kubwa (*hajj*) na kufanya hija ndogo (*umrah*) na akaamua kuondoka Makka na kuelekea Kufah pamoja na familia yake na wafiasi wake. Imam aliondoka kuelekea Iraq mnamo mwezi 8 Dhul-Hijjah, 60 A.H. Siku ya Tarwiyyah, siku ileile ambayo Muslim Ibn Aqil aliuliwa kikatili na ibn Ziyad. Hivyo Imam alikuwa ametumia takriban siku 95 hapo mjini Makka. (*Kitab al-Irshaad*).

Katika kuondoka kwake Makka, Imam aliomba karatasi ambamo aliandika ujumbe ufuatao kwa ajili ya Bani Hashim: “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Kutoka kwa Husein Ibn Ali kwenda kwa kizazi cha Hashim, jueni kwamba ye yeyote atakayeandamana na mimi ataulliwa, ambapo yule

atakayejizuia kwenda pamoja nami kunisaidia hatapata mafanikio! Amani iwe juu yenu.” (*Al-Luhuf*).

WOSIA WA IMAM (A.S.) KATIKA KUONDOKA KWAKE MAKKA

Katika kuondoka kwake Makka, Imam aliandika wosia na kuukabidihi kwa ndugu yake Muhammad ibn al-Hanafiyyah. Wosia huo ulisomeka hivi: “Sikusimama dhidi ya Yazid ili kusababisha uharibifu au kutolewana, wala kwa kujinyanya mimi mwenyewe mbele za watu, wala kuonea. Mimi nimesimama tu ili kurekebisha mambo ya Ummah wa babu yangu na hali ya Shi’ah wa baba yangu Ali ibn Abi Talib. Napenda kuamrisha mema na kukataza maovu. Yeyote anayekubali nafasi yangu mimi atakuwa upande wa Mwenyezi Mungu na upande wa haki. Yeyote anayenikataa mimi, Mwenyezi Mungu awe hakimu wa mwisho kati yao na mimi. Yeye Ndiye hakimu bora. Ewe ndugu yangu! Kwa kweli mafanikio yanatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye ndio nimetegemea na Kwake Yeye ninarejea.” Imam aliikunja barua hiyo na akaifunga kwa muhuri wa pete yake. Kisha akaikabidhi kwa ndugu yake Muhammad ibn al-Hanafiyyah. (*Nahj al-Shahadah*).

HOTUBA YA IMAM HUSEIN WAKATI WA KUONDOKA KWAKE MAKKA

Kabla ya kuondoka kwake, Imam alitoa hotuba nzuri sana, vyote katika fasaha na yale yaliyomo. Hotuba hii inajulikana kama mstari wa kifo (*khatwi al-mawt*). Kutoka kwenye hotuba hiyo, sisi tutaelezea ile kauli yake ya mwisho kwa sababu ya umuhimu wake ambao umesababisha marejeo mengi ya mara kwa mara yaliyofanywa na

kila mtu, wanahistoria, makhatibu, wanamapinduzi na wale ambao wanampenda yeye: “Yule anayependa damu yake imwagike kwa sababu yetu na ambaye ameamua kukutana na Mwenyezi Mungu aondoke pamoja nasi kesho, kwani ninanuia kuondoka kesho asubuhi kwa mapenzi ya Allah (swt).” (*Muthir al-Ahzan*).

NYOYO NA PANGA ZA WATU WA KUFAH

Imam na kundi lake taratibu na kwa umadhubuti walisonga mbele kuelekea Iraq wakipita kwenye sehemu na maeneo ambayo yanakuwa kati ya Makka na Iraq. Sehemu walizopita kutoka Makka na kuendelea zilikuwa ni Tan’im, Sifah, Dhat ‘Irq, Khazimah, Zrud, Hajiz, Dhu Husum, Tha’libiyah, Shuquq, Zubalah, Batn al-‘Aqabah, Sharaf, Bidah, Rahimah, Qadasiyah, ‘Udhayb, Qasr Banu Muqatil, vijiji vinavyoelkezea Karbala na mwishowe Karbala penyewe. Watu wengi walikutana na Imam akiwa njiani kuelekea Iraq na katika kila makutano, Imam alielezea asili ya vuguvugu lake na akawaalika watu hao kujiunga na safu zake dhidi ya utawala wa kidhalimu wa Bani Umayyah.

Kilomita chache kutoka Makka, mahali panapojulikana na Sifah Imam alikutana na Farazdaq, yule mshairi maarufu na mfuasi mtifu wa Imam. Farazdaq alikuwa ndio kwanza amewasili kutoka Kufah. Imam akamuuliza kuhusu hali ya Kufah na hisia za watu huko. Farazdaq kwa hili akajibu: “Nyoyo zao ziko pamoja na wewe lakini panga zao ziko pamoja na Bani Umayyah. Amri ya mwisho itashuka kutoka Mbinguni.” Imam akajibu: “Umesema kweli. Kila kitu kinatoka kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Yeye yuko katika hali ya utukufu wakati wote. Kama amri ya Allah imekuja kupita, sisi tunamtukuza na kumsifia Yeye. Kama sio hivyo, basi mtu ambaye nia yake ni safi na ambaye moyo wake unamcha Mungu huyo hatoshindwa.” (*Al-Kamil cha Ibn Athiir*).

Jibu kama hilo hilo lilitolewa kwa Imam (a.s.) kutoka kwa Bushayr ibn Ghalib huko Dhat al-'Irq. (*Muthir al-Ahzan*)

Wakati Imam alipokuwa karibu na Qadisiyyah, alikutana na Tirimmah ibn 'Adi na akamuulizia kuhusu watu wa Kufah. Tirimmah alijibu: "Wakuu na watu waungwana wa Kufah wamerudi upande mmoja na ibn Ziyad na wamempa udhibiti juu ya mali zao. Wamefanya maandalizi ya kupigana dhidi yako. Na kuhusu watu wengine waliobakia, nyoyo zao ziko pamoja na wewe lakini panga zao ambazo zimefutwa (zimechomolewa) zina kiu juu ya damu yako." (*Muthir al-Ahzan*).

SHAHADA YA QAIS IBN MUSHIR AL-SAYDAWI – MJUMBE WA IMAM HUSEIN

Wakati Imam (a.s.) alipokaribia mahali panapojulikana kama Hajiz, alimtuma Qays ibn Mushir al-Saydawi kama mjumbe wake pamoja na barua kwenda kwa watu wa Kufah. Barua hiyo ilisomeka kama ifuatavyo: "Barua ya Muslim ibn Aqil imenifikasi. Inaeleza kwamba ninyi mmejiandaa na mmeungana katika kunisiaidia mimi na mna maoni mazuri kuhusu kusudio letu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu kwamba kukutana kwetu kuwe kunakofurahisha na kwamba mbakie imara katika njia ya haki. Nimeanza safari yangu kuelekea kwenu mnamo ile Siku ya Tarwiyyah – 8 Dhul-Hajj. Ninamtuma mjumbe wangu kwenu kabla yangu mimi ili ninyi muweze kujiardaa. Kwa idhini yake Allah nitakuwa nanyi hivi karibuni."

Qays ibn Mushir aliondoka kuelekea Kufah kwa farasi. Hata hivyo, Husayn ibn Numayr na vikosi vyake walimkamata huko Qadisiyyah. Qays alichukuliwa chini ya ulinzi hadi kwa ibn Ziyad. Wakati alipotokeza mbele ya ibn Ziyad, aliiweka ile barua ya Imam kinywani kwake na kuitafuna. Ibn Ziyad akauliza: "Wewe ni nani?"

Qays akajibu: "Mimi ninatokana na Shi'ah wa Amirul-Mu'minin Ali Ibn Abi Talib." Ibn Ziyad akauliza kwa kudai: "Kwa nini umeitafuna barua ile?" Qays akajibu: "Ili wewe usiweze kujuu kilichoandikwa ndani yake." Halafu ibn Ziyad akamuuliza: "Ni nani aliyeiandika barua hiyo na ilikusudiwa kwenda kwa nani?" Qays akajibu: "Barua hiyo imetoka kwa Imam Husein kwa ajili ya watu wa Kufah ambao siwajui kwa majina yao."

Ibn Ziyad alighadhibika na akamuamuru Qays: "Panda juu ya jukwaa umkane na kumlaani al-Husein, mtoto anayedanganya, mtoto wa baba muongo." Qays alipanda jukwaani. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, yeye akasema: "Enyi watu! Husein ni mbora wa viumbe wa Mwenyezi Mungu. Yeye ni mtoto wa Bibi Fatimah binti ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Mimi nimekuja kama mjumbe wake kwenu. Yeye nimemuacha huko Hajiz. Enyi watu! Itikieni mwito wake wa kutaka msaada na unganeni naye." Baada ya haya, Qays akamlaani ibn Ziyad, baba yake na Bani Umayyah na akawaombea Imam Ali, Imam Hasan na Imam Husein (a.s.).

Ibn Ziyad akawa amekasirika sana kupita kiasi juu ya haya na akawaamuru wanyongaji kumchukua Qays hadi kwenye paa la kasri hilo na kumuua kwa kumtupa hadi chini ardhini. Qays aliuliwa kwa namna na njia hiyo. Kisha ule mwili wake usio na uhai ukakatwa kichwa na mmoja wa walanzi wa ibn Ziyad aliyeitwa Abd al-Malik ibn Umayr. (*Muthir al-Ahzan*).

Maelezo mengine kama hayo yametolewa kuhusu mjumbe mwingine wa Imam Husein (a.s.) kwa jina la Abdallah ibn Yuqtur. (*at-Tabarii*).

Imam Husein (a.s.) na msafara wake waliendelea kutoka Hajiz, ukakutana na kundi la watu wapanda farasi kutoka Kufah. Kundi hilo lilikuwa na Nafi' ibn Hilal na Umar ibn Khalid. Imam (a.s.) akaulizia

kuhusu mjambe wake, Qays ibn Mushir na akajulishwa kwamba ibn Ziyad amekwishamuua. Imam alilia sana kwa taarifa hizo za kuuliwa Qays na akasema: “Sote ni wa Mwenyezi Mungu, na kwa Kwake Yeye tutarejea! Hakika Mwenyezi Mungu amempatia yeye mahali huko Peponi.” Kisha Imam (a.s.) akamuomba Mwenyezi Mungu, “Ewe Allah! Wajaalie Shi’ah wetu na sisi wenyewe mahali karibu na Wewe. Hakika Wewe uko juu ya vitu vyote, Mwenye uwezo.” (*Al-Luhuf*).

Walipofika mahali pa kupumzika hapo Dhu Husum, Imam (a.s.) alitoa hotuba kuhusiana na hali ya uasi na ukosa uaminifu wa dunia hii. Kuelekea mwishoni mwa hotuba hiyo, yeye alionyesha sababu za upinzani wake na nia na dhamira yake kwa maneno haya yafuatayo:

“Hamuoni namna jinsi kweli ilivyokuja kutelekezwa na jinsi udanganyifu unavyokuwa haukemewi? Katika mazingira kama haya, muminini wa kweli hana budi kutamani kukutana na Mwenyezi Mungu, kwani mimi sikioni kifo kama kitu chochote isipokuwa kama chanzo cha furaha na maisha na watu hawa waovu, madhalimu kama si chochote bali ni huzuni na fedheha.”

(*Muthir al-Ahzan*).

MAZUNGUMZO YA ALI AL-AKBAR IBN HUSEIN NA IMAM

Wakati wa mchana Imam alipokuwa anasafiri kupita kwenye mawanda ya Tha’alabiyyah, alikuwa mara kwa mara akipitiwa na usingizi nyuma ya farasi wake bora. Alipokuwa anaamka alisoma ile aya “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.” Hii ni aya inayosomwa kwa kawaida wakati wa matatizo na maafa. Mtoto wa Imam (a.s.) Ali al-Akbar ibn al-Husein ambaye alikuwa kwenye

kipando karibu naye alimuuliza Imam kuhusu wasiwasi wake wa ghafla. Imam (a.s.) akamjibu: “Ewe mwanangu! nililala kidogo na nikasikia sauti nyuma yetu ikitangaza: “Enyi watu! Mnatembea kwa haraka na kifo kinawaongoza kwa kasi kuelekea kwenye bustani za Peponi.” Alipoyasikia haya, Ali al-Akbar akasema: “Ewe baba! sisi hatuko kwenye njia ya haki?” Imam (a.s.) akamjibu: “Ndio mwanganu! Naapa kwa Yule ambaye Kwake ndio marejeo ya viumbwe wote, sisi tuko kwenye njia ya sawa.” Hapo Ali al-Akbar akasema, “Kwa hali hiyo sisi hatuna wasiwasi iwapo kifo kinatujia au ni sisi tunakiendea.”

Imam (a.s.) akamuangalia Ali al-Akbar na kisha akasema: “Mwenyezi Mungu akujaalie malipo bora yale aliyompa mwana kwa niaba ya baba yake.” (*Luhuf*).

MAOMBI YA IMAM YA KUTAKA MSAADA

Wakati wa safari yake kuelekea Iraq, Imam (a.s.) aliwaalika watu na machifu wa makabila mbalimbali ambayo alikutana nao kuja kumsaidia yeye. Hapa itatutosha sisi kuelezea maafa ya watu watatu kama hao ambao Imam aliwaita kumsaidia.

1. Ubaidullah bin Hurr al-Ju’fi

Vile Imam (a.s.) na wafiasi wake walipofika mahali pa kupumzika pa Qasr Banu Muqatil, walikuta kwamba kuna hema lililosimamishwa hapo. Kulikuwa na farasi aliyefungwa nje ya hema hilo na upanga uliokitwa ardhini. Imam (a.s.) aliulizia kuhusu mmiliki wa hema hilo na akajulishwa kwamba lilikuwa ni mali ya Ubaydullah ibn Hurr al-Ju’fi.

Imam (a.s.) alimtuma Hajjaj ibn Masiru, ndugu wa mbali wa Ubaydullah kwenda kumkaribisha kwenye kambi ya Imam. Hajjaj

akamwambia Ubaydullah: “Kama utamlinda Imam na familia yake dhidi ya maadui zao, wewe utalipwa. Kama utauawa katika kuwatetea wao, utakuwa umeuawa Shahidi.” Kwa hili Ubaydullah akajibu: “Wallahi! Mimi nimeondoka Kufah kwa sababu watu wa Kufah wamewatelekeza Shi’ah wa al-Husein na wamefanya maandalizi ya kumuua yeye lakini mimi sina uamuzi ama nguvu ndani ya moyo wangu ya kumsaidia Husein. Sipendi kukutana na Husein, wala yeye kuniona mimi.”

Hajjaj alirudi kwa Imam (a.s.) na kumjulisha yale yaliyokuwa yamejiri. Imam pamoja na kikundi cha watu wa familia yake na marafiki wa karibu walikwenda kwa Ubaydullah. Ubaydullah alimpokea Imam na akamkalisha kwenye sehemu ya heshima mionganii mwa mkusanyiko ule ndani ya hema. Ubaydullah alimtazama Imam (a.s.) na akasema: “Mpaka kufikia sasa nilikuwa sijaona uzuri na nuru kama ninayoiona kwa Husein na moyo wangu haujawahi kuungua kwa huzuni juu ya yeote yule kama ulivyokuwa kwa Husein, ambaye ameingia kwenye safari hii pamoja na wanawake na watoto.” Kisha Ubaydullah akaziona ndevu nyeusi za Imam (a.s.) na akauliza kama alikuwa amezipaka rangi au kama zilikuwa ni nyeusi za kawaida. Imam (a.s.) akajibu kwamba umri mkubwa umemtupa mkono. Ubaydullah alielewa kwamba Imam alikuwa amezitia rangi ndevu zake.

Baada ya mkusanyiko huo kutulia, Imam alimwambia Ubaydullah: “O Ubaydullah ibn Hurr! Watu wa mji wako (Kufah) wameniandikia kunijulisha juu ya uungaji mkono wa pamoja juu yangu. Wameniomba mimi niwaongoze. Kwa kukimbia kwako wewe umetenda dhambi kubwa. Je ungependa kutubia na kujiondolea mwenyewe mzigo wa dhambi hii?” Ubaydullah akamuuliza: “Na hilo ni kwa namna gani?” Imam (a.s.) akasema: “Toba yako itapatikana kwa kumsaidia mtoto wa binti ya Mtume wako na upigane pamoja

naye dhidi ya maadui zake.” Baada ya kuyasikia haya, Ubaydullah akasema: “Wallahi, Mimi ninafahamu kwamba yule atakayekufa katika kukutetea wewe atapata Furaha kuu ya Milele huko Akhera. Pamoja na hayo, mimi sina azma kama hiyo wala ujasiri. Watu wa Kufah wamekutelekeza na wamekuwa upande mmoja na adui yako. Mimi niko tayari kukupa farasi wangu ambaye kamwe hajashindwa kumpita adui anayekimbia au katika kumtoroka adui anayefukuzia.”

Imam (a.s.) alionyesha kusikitishwa kwake na majibu ya Ubaydullah na akasema: “Kama una hofu ya kutoa muhanga uhai wako kwa ajili yangu, basi sina haja na farasi wako wala wewe mwenyewe.” Na kisha akasoma: “Sitawachukua watu ambao wanageukia mbali kuwa kama wasaidizi.” Halafu Imam (a.s.) akasema: “Napenda kukuonya kwamba ni kwa hiari yako kwamba hutaki kuzingatia ombi langu. Hata hivyo, kumbuka kwamba yule mtu anayegeukia mbali na mimi baada ya kusikia wito wangu wa kutaka msaada atakuja kutupwa kwenye mashimo ya Jahannam kichwa chini.”

Kutokana na udhaifu wa maamuzi, Ubaydullah alishindwa kujitenga mwenyewe na mapenzi ya dunia katika wakati muhimu kama huo. Aliishi maisha yake yote akijutia udhaifu wake wenye mkosi mbaya. (*Maqtal al-Husayn al-Muqarram*).

2. Zuheir ibn Qayn al-Bajali

Zuheir ibn Qayn pamoja na wafuasi wake walikuwa wakirejea kwenda Kufah wakitokea Makka baada ya kutekeleza ibada ya Hijja. Zuheir na wafuasi wake walikuwa wamefahamu juu ya lengo la Imam (a.s.) na harakati zake za kuelekea Iraq. Hata hivyo, wao hawakuwa tayari kuungana na Imam na walikuwa wakijaribu kue-puka kukutana na msafara wa Imam kwenye safari yao. Hata hivyo,

ilikuwa ni hukmu ya Mwenyezi Mungu kwamba Zuheir alipaswa kusimama mahali ambapo Imam (a.s.) tayari alikuwepo.

Wakati kundi la Zuheir lilipokuwa linapumzika na kula chakula, mtu mmoja katika msafara wa Imam al-Husein aliwaendea na kusema: “O Zuheir! Abu Abdillah al-Husein ametuma kukuita.” Zuheir na kundi lake walipigwa na butwaa baada ya kusikia jina la Husein. Zuheir alikuwa anasita lakini Dalham mke wake alisimama na akazungumza: “Utukufu ni kwa Allah! Hivi mtoto wa Mtukufu Mtume anakuita na wewe unasita kwenda? Kwa nini huendi kwake na kusikiliza hilo analotaka kusema?”

Zuheir alitingishwa sana na kauli hii na akaenda kwa Imam (a.s.). Haikuwa muda mrefu kabla Zuheir hajarudi akiwa mng’avu mwenye kuonyesha furaha. Aliamuru mahema yake yashushwe na akahamia pamoja na mizigo yake na wanyama hadi karibu na yale ya Imam (a.s.). Halafu akamgeukia mke wake na akasema: “Nimekutaliki, nenda kajjunge na familia yako kwani sitawezza kuvumilia kukufikiria wewe kama mateka baada ya kifo changu.”

Kisha akawageukia wafuasi wake na akasema: “Wale wanaotaka kufuatana na mimi nawafanye hivyo. Vinginevyo huku kutakuwa ni kukutana kwetu kwa mara ya mwisho.” Aliendelea kusema: “Sikilizeni yale nitakayoyasema! Tulikuwa tukipigana na adui pale Balanjar. Tuliwashinda na tukapata ngawira nyingi mno. Salman Farsi alikuwa pamoja nasi wakati ule. Yeye alisema: ‘Mmefurahishwa na ngawira hizi?’ Sisi tukasema: ‘Ndiyo.’ Yeye akasema: ‘Utakuja wakati ambapo mtamuona Bwana wa vijana wa Peponi. Piganeni sambamba naye na mtakuwa na mengi ya kupata kuliko ngawira hizi.’ Kwa hiyo, mimi ninakuacheni kwenye ulinzi wa Mwenyezi Mungu.” Kwa hayo yeye akaenda kuungana na Imam Husein (a.s.) (*Kitab al-Irshaad*).

3. Wahb

Wahb, mama yake Qamar na mke wake Haniyyah ambaye amemuoa hivi karibuni tu waliishi katika jangwa la Tha'labiyyah. Wahb ali-kuwa akiwachukua kondoo wake na mbuzi kwenda kwenye malisho kwenye milima na angekuwa akirejea nyumbani wakati wa usiku. Wote watatu walikuwa ni Wakristo na waliishi maisha rahisi na ya amani ingawa walikuwa ni masikini sana.

Wakati msafara wa Imam Husein (a.s.) ulipokuwa ukisonga mbele kuelekea Kufah, yeye aliona hema lililokuwa limeungua nusu yake katika jangwa hilo la Tha'alabiyyah. Imam alikwenda kwenye hema hilo na akamkuta bibi mzee aliyekuwa ameshambuliwa na umasikini. Imam akamuuliza kuhusu hali yake ndani ya jangwa. Yeye akaeleza, “Tunamudu kuishi lakini kuna upungufu mkubwa wa maji. Kama kungekuwa na maji tu hapa, maisha yetu yangetuwa ya starehe zaidi kidogo.” Imam akamchukua mwanamke huyo hadi kwenye jiwe na alipoligonga kwa mkuki wake, chemchemi ya maji baridi na matamu ikabubujika. Yule mwanamke mzee hakuweza kuzuia furaha yake na akarudiarudia kumshukuru Imam (a.s.).

Kabla hajaondoka na kumuacha pale, Imam alimueleza sababu ya safari yake na akasema kwamba ataweka kambi hapo Karbala. Alimuomba yule mwanamke mzee huyo amwambie kijana wake wakati atakaporudi ajiunge naye na kumsaidia katika njia ya haki.

Baada ya Imam (a.s.) kuondoka pale, yule mwanamke mzee alifikirishwa na ile heshima, ukarimu, upaji na huruma ya Imam (a.s.). Alitamani kumfuata Imam mara moja lakini akatambua kwamba hana budi kusubiri marejeo ya mwanawewe Wahb na Haniyyah. Mara tu baada ya kurejea kwa Wahb pamoja na mke wake aliyemuoa punde tu, Qamar aliwasimulia juu ya matukio ya siku ile na akawasilisha ujumbe wa Imam kwake. Nyoyo za watatu hao mara

moja zikatawaliwa na mapenzi ya Imam Husein (a.s.). Waliondoka mara moja kuelekea Karbala na wakajiunga na familia na wafuasi wa Imam Husein. Ilikuwa ni wakati huu ambapo wote watatu waliitikia imani na dini ya Uislam mikononi mwa Imam Husein. Mnamo siku ya Ashura, mwezi 10 Muhamarram, siku ambayo Imam Husein (a.s.) aliuliwa kikatili, Wahb na Haniyyah walikuwa wameoana kwa takriban siku kumi na saba kufikia siku hiyo.

(Ma ‘ali al-Sibtayn).

TAARIFA ZA KUUAWA SHAHIDI KWA MUSLIM BIN AQIL

Abdallah ibn Sulaym na Madhri ibn Musha’il, ambao wote wali-kuwa ni wa kabile la Asad, walikuwa wamejiunga na Imam Husein (a.s.) walipokuwa wamekamilisha ibada yao ya Hijja, wanasimulia yafuatayo:

“Wakati tulipowasili kwenye sehemu ya mapumziko ya Zurad pamoja na Imam, tuliwaona wasafiri wakija kutokea Kufah. Mara tu watu hawa walipomuona Imam wakabadili mwelekeo ili kukwepa kukutana na Imam. Tulipanda farasi wetu na kuwakimbilia watu hao na tukawauliza wao wali-kuwa ni akina nani. Wakajibu kwamba walitoka kwenye kabila la Asad. Sisi tukasema kwamba na sisi tunatoka kwenye kabila hilo pia na tukawauliza kuhusu hali mjini Kufah. Walijibu, ‘Tuliondoka Kufah tu kwa sababu tuliona miili ya Muslim ibn Aqil na Hani ibn Urwah ikiwa imefungwa na kuburuzwa na kupitishwa kwenye mitaa ya Kufah.’

“Tuliendelea na safari yetu pamoja na Imam (a.s.). Tulipowasili Tha’labiyyah, tulikwenda kwa Imam na tukasema:

‘Tunazo taarifa za Kufah. Je, tukujulishe mbele ya hawa wengine ama tukuambie kwa siri?’ Imam (a.s.) akawaangalia wafuasi wake na kisha akasema: “Mimi sifichi siri yoyote kwa watu hawa.’ Baada ya kusikia hivyo, tukamwambia Imam (a.s.) kile tulichokuwa tumekisikia kuhusu kifo cha Muslim ibn Aqil na Hani na yaliyofanywa juu ya miili yao. Imam akarudia ile aya ya, “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.’

“Tulimuomba Imam (a.s.) kusimamisha safari yake ya kwendwa Kufah na arejee kwenye sehemu yenye usalama, kwani imekuwa dhahiri na wazi kwamba hakuwa na uungwaji mkono tena huko Kufah.

“Imam (a.s.) akawaangalia watoto wa Muslim ibn Aqil na akasema: “Muslim ameuawa. Je, mna maoni gani kuhusiana na jambo hili.” Watoto hao wakajibu: “Wallahi sisi hatutarudi nyuma mpaka tuwe tumelipa kisasi cha damu yake au tunywe kutoka kwenye kikombe maalum cha Shahada kama yeye alivyokufa kishahidi.” Imam (a.s.) akasema: “Hakuna ubora katika maisha baada ya watu hawa.” Tukaelewa kutokana na kauli hii ile dhamira ya Imam (a.s.) ya kutoa uhai wake katika njia ya Mwenyezi Mungu.””

VILIO NA MACHOZI KWA TAARIFA ZA SHAHADA YA MUSLIM BIN AQIL

Taarifa za kifo cha Muslim Ibn Aqil zilipoifikia kambi ya Imam Hussein (a.s.), vilio na mayowe vya maombolezo ya sauti kubwa vilijaza anga hewa ya jangwa na mafuriko ya machozi yalibubujika kutoka kwenye macho ya familia yake na wale waliompenda yeye.

Baada ya kujua kuhusu kifo cha Muslim Ibn Aqil, na uimara wa Imam kwa ajili ya njia ya Mwenyezi Mungu, hata kama italazimu uhai wake na ule wa watu wa familia yake, idadi kubwa ya watu ambao walikuwa wamefuatana naye kutoka Makka kwa matumaini ya kupata ngawira za vita walivunjika moyo. Waliangaliana wenyewe kwa wenyewe kwa chukizo na hatimae wakatawanyika na kumtelekeza Imam (a.s.). Imam aliachwa pamoja na wana familia yake na wafuasi wake wa karibu wachache tu. (*A yan al-Shi 'ah*)

Farazdaq, yule mshairi na mpenzi mtiifu wa familia ya Mtukufu Mtume, alikuja mbele ya Imam na akasema: “Ni vipi utawaamini watu wa Kufah? Wao ndio watu wale wale ambao wamemuua binamu yako Muslim na wasaidizi wake!” Imam alitokwa na machozi aliposikia jina la Muslim ibn Aqil na akasema: “Ewe Allah! Jaalia huruma Zako juu ya Muslim. Ameondoka kwa ajili ya furaha isiyo kifani ya Peponi na amepata radhi za Allah. Kilichoamriwa kwa ajili yake hakina budi kupita. Sisi tunasubiri juu ya kile kilichoamriwa kwa ajili yetu. Maamuzi ambayo yatakuja kupita.” (*Al-Luhuf*).

Sheikh Abbas Qummui anasimulia katika *Muntaha al-Amal* kwamba Muslim Ibn Aqil alikuwa na binti aliyeitwa Hamidah, ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi na tatu. Alikuwa akisafiri pamoja na msafara wa Imam (a.s.). Wakati Imam alipojua kuhusu kifo cha Muslim ibn Aqil, alimwita Hamidah. Akamkalisha Hamidah kwenye paja lake na akampapasa kichwa chake kwa upendo mwangi mno. Hamidah hakuweza kuelewa sababu ya upole huu na akauliza kwa sauti ya kwikwi: “O ami yangu mpendwa! Ni nini kimemtokea baba yangu?” Husein (a.s.) alilia wakati alipokuwa akijibu: “Ewe mtoto! Usihuzunike kama Muslim hayupo pamoja nasi tena. Tambua kwamba mimi ni baba yako, dada yangu ndiye mama yako, mabinti zangu mimi ni dada zako wewe na wanangu wa kiume ni kaka zako.”

Hamidah alilia katika kuomboleza juu ya kuuliwa kikatili kwa baba yake. Watoto wa kiume wa Muslim Ibn Aqil walivua vilemba vyao na wakalia sana kwa sauti kwa ajili ya baba yao. Imam pamoja na watu wote waliobakia wa familia ya Bwana Mtume (s.a.w.w.) walihuzunishwa na kufadhaishwa sana kwa tukio hilo.

(Muntaha al-Amal).

KUZUIWA NJIANI IMAM NA MAJESHI YA HURR IBN YAZID RIYAH

Wakati taarifa za kusonga mbele kwa Imam (a.s.) kuelekea Kufah zilipomfikia ibn Ziyad, alijishughulisha na kuiweka hali katika mji wa Kufah chini ya udhibiti na kupanga majeshi yake ili kuzima uasi wowote utakaojitokeza dhidi yake na kumshinda Imam katika vita. Alituma kikosi cha jeshi cha askari thelathini elfu walioandalialiwa vyema kwa silaha kwenda kumzuia Imam pamoja na wafuasi wake wasiingie mjini Kufah.

Vikosi vilivyotumwa kumzuia Imam vilipangwa katika safu na chini ya uongozi wa majenerali wafuatao:

1. Hurr akiwa pamoja na jeshi la watu elfu moja
2. Mudhar ibn Rahinah na kikosi cha wapiganaji elfu tatu
3. Shimr ibn Dhi Jawshan na kikosi cha wapiganaji elfu nne
4. Yazid ibn Riqab pamoja na idadi takriban elfu kumi na mbili
5. Husayn ibn Numayr pamoja na watu elfu nne
6. Shabath ibn Rib'i na watu elfu moja
7. Ka'b ibn Talhah na watu elfu tatu
8. Hajjar ibn Abjar na askari elfu moja

9. Nasr ibn Harshah akiongoza watu elfu mbili

Mpaka kufikia mwezi 6 Muharram wapiganaji elfu ishirini walikuwa wamekwisha kukusanyika hapo Karbala. Ibn Ziyad alipeleka vikosi vya ziada ambavyo vilileta idadi ya mwisho ikizungukia kwenye elfu thelathini.

(Maqtal al-Husayn al-muqarram)

Kwa amri ya Imam ngozi za maji zote na vyombo vingine vilijazwa maji wakati walipoondoka mahali panapoitwa Sharaf katika giza la usiku. Wakati wa mchana walivyokuwa wakiendelea na safari yao, mtu mmoja katika kundi lao aliguta kwa sauti, “*Allah Akbar – Mungu ni Mkuu!*” Imam akamtazama na akasema: “Hakika Mungu ni Mkuu lakini ni ipi sababu yako ya kutamka hivyo kwa wakati huu?” Yeye akajibu: “Ninaiona miti ya mitende ya Kufah.” Watu waliofuatana na Imam katika kundi hilo, ambao walikuwa wakizitambua vema njia hizo na waliojua mahali hasa walipokuwa walisema: “Bado tuko mbali sana na mji wa Kufah. Wale ni askari waliojiandaa kikamilifu na silaha wakitujia sisi.” Imam baada ya kuangalia kwa makini na uhakika akasema: “Ni kweli ni jeshi lililogubikwa na silaha ambalo linatukaribia sisi.” Baada ya kushauriana na watu wake, Imam (a.s.) aliamua kuweka kambi karibu na kijiji jirani na hapo kiiwacho Dhu Husum.

Haikuchukua muda wakati jeshi la watu elfu moja lenye silaha kamili likafika kwenye kambi ya Imam (a.s.). Hata hivyo ilionekana kutokana na hali yao kwamba hawakudhamiria kuingia kwenye mapambano mara moja tu. Imam (a.s.) aliziona ishara za kiu na uchovu mwingi kwenye nyuso za askari hao. Aliwaagiza watu wake kuwahudumia kwa maji watu hao na wanyama wao. Maji yakatolewa kwa kila mtu na farasi hadi yule wa mwisho kabisa.

Ali bin Tan'an alisimulia: "Mimi nilikuwa mtu wa mwisho kuwasili pamoja na jeshi hilo hapo Dhu Husum. Pale Imam al-Husein alipoona jinsi mimi na farasi wangu tulivyokuwa na kiu, aliniambia nimfanye farasi wangu apige magoti nami ninywe nitoe kiu yangu na kisha nimpe farasi wangu maji. Mimi nikafanya kama alivyosema.

(Nafas al-Mahmum).

SWALA YA JAMAA

Wakati wa swala ya mchana uliwadia. Mpaka hapo hakuna mazungumzo yoyote yaliyofanyika kati ya Imam na Hurr. Baada ya Hajjaj ibn Masruuq kumaliza kuadhini kwa ajili ya swala, Imam (a.s.) aliamua kuongoza swala kwa ajili ya wafuasi wake. Alitoka mbele na akasimama katikati ya majeshi hayo mawili. Baada ya kumhimidi Mwenyezi Mungu akasema: "Enyi watu! Mimi sikuja bila ya kuitwa. Ninyi kwa kupitia barua zenu na kwa kupitia wajumbe wenu, mlinialika niye Kufah na mkasisitiza kwamba sina budi niye. Ninyi mlisema: 'Njoo haraka kwetu. Sisi hatuna kiongozi. Tunataka kufuata njia ya haki chini ya himaya na uongozi wako.' Nitabakia pamoja nanyi endapo bado mngali imara katika uamuzi wenu. Vinginevyo niruhusuni nirejee kwenye ardhi ya nyumbani kwangu." Kila mmoja alibakia kimya na wakashusha vichwa vyao chini.

Adhana ya swala ilisomwa kwa mara nyingine. Halafu Imam (a.s.) akamgeukia Hurr na akasema: "Hudhuria kwenye swala yenu na sisi tutahudhuria kwenye swala yetu." Hurr akajibu: "Sisi sote tutatekeleza swala yetu nyuma yako." Na hivyo makundi yote yakaswali swala yao nyuma ya Imam (a.s.).

(Kitab al-Irshaad).

MAZUNGUMZO YA IMAM NA HURR

Wakati swala ya mchana ilipokwisha, Imam (a.s.) aliligeukia jeshi la Hurr. Baada ya kumsifu Mwenyezi Mungu, na kumtakia rehema na amani Bwana Mtume (s.a.w.w.) na kizazi chake (a.s.) yeye akasema: “Enyi watu! Kama mnaamua kushikamana na kanuni za uchamungu na kujichunga na kuwapa wale wenye ukweli haki yao, hakika mtafunikwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu swt. Enyi watu! Sisi ni dhuria ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) nasi tunayo haki kubwa kabisa kuliko wengine kwenye uongozi na utawala wa Waislam. Barua zenu vilevile zimelithibitisha hili. Tafakarini kwa makini na kama mkitaka, sisi tutarejea majumbani kwetu.”

Hurr akamwambia Imam (a.s.): “Sisi hatuna habari na hizi barua za mwaliko!” Kwa maagizo ya Imam (a.s.) mmoja wa wafuasi wake akaleta magunia mawili yaliyojazwa barua. Hurr akaziangalia barua zile na kisha akasema: “Mimi sio mmojawapo wa wale ambao waliandika barua kwako na mimi sina lolote la kuhusika na wewe. Mimi nimeagizwa kubakia na wewe na nitakuchukua hadi Kufah na nikakukabidhi kwa ibn Ziyad.” Imam (a.s.) alichukia kwa hili na akasema: “Kifo kipo karibu sana na wewe kuliko kile mlichokipanga.” Hurr hakujibu kitu.

Imam (a.s.) aliwageukia wafuasi wake na akasema: “Simameni na mjiandae kwa ajili ya kurejea kwenu.”

Wakati msafara huo ulipokuwa karibu kuondoka, Hurr kwa ushupavu akashika hatamu za farasi wa Imam kumzuia asisonge mbele. Imam kwa hasira sana akamwambia: “Mama yako alie kwa kifo chako! Wewe una sababu gani dhidi yetu?” Hurr akiwa ameshtushwa na kuduwaalimwangalia Imam (a.s.) na akasema: “Kama mtu mwingine yejote katika Arabia angetamka jina la mama

yangu, mimi pia ningesema hayo hayo juu ya mama yake. Hata hivyo, Wallahi mimi ninaweza tu kulitaja jina la mama yako kwa heshima ya hali ya juu kabisa.”

Kisha Imam (a.s.) ndipo akamuuliza: “Ni nini unachokitaka?” Hurr akajibu: “Mimi nimeariwa nikuchukue na kukupeleka kwa ibn Ziyad huko Kufah.” Baada ya kupishana kwa maneno, Hurr akamwambia Imam (a.s.): “Sina nia ya kuingia vitani pamoja na wewe lakini nimeagizwa nisikuache. Nitamuandikia ibn Ziyad na kusubiri maelekezo zaidi. Nina matumaini kwamba hakuna machungu yatakayotokea baina yetu.” Kisha Hurr akasema kwa nia ya kumuasa Imam (a.s.): “O Husein! Nakusihii kwa jina la Allah swt. kuokoa maisha yako. Mimi sina shaka kwamba utauliwa kama utaingia vitani.” Kwa hili Imam (a.s.) akasema: “Je unatafuta kunitishia na kifo? Kama mkinua mimi, ndio kwamba mambo yatakuwa yameamuliwa?” Mwishowe Imam (a.s.) akamwambia Hurr: “Nitakupa majibu yale yale kama yaliyotolewa na mtu mmoja wa kabile la Aws ambaye alitaka kumsaidia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na akakabiliwa na ndugu zake na wakamwambia kwamba atauliwa. Katika kuwajibu alisoma beti zifuatazo:

“Nitasonga mbele, kwani kifo sio dosari juu ya kijana
anaponuia haki na akapigana kama Muislam.

“Na anapoyatoa muhanga maisha yake kwa ajili ya haki.

Kama nitaishi, nitafanya hivyo bila majuto na nikifa basi bila lawama.

“Ufidhuli huu unatosha juu yenu kwamba mnaishi.
Na bado pua yako imesuguliwa juu ya ardhi.”

Hurr alipozisikia beti hizi, na akaelewa kwamba Imam (a.s.) alikuwa tayari kufa kwa kile alichoamini na hatonyenyeyekea

kwenye udhalili kwa mtu yoyote, alikwenda kwa askari wake na akaanza kuondoka. Na Imam naye na wafuasi wake akaanza upya safari yake.

HOTUBA ILIYOTOLEWA NA IMAM HAPO BIDAH

Majeshi mawili hayo yaliendelea kusonga mbele kwenye njia zao pakiwa na umbali kidogo kati yao mpaka yalipofika kwenye ardhi ya Bidah. Ili kuzishinda hoja za wapinzani wake na kueleza sababu zake vizuri zaidi, Imam kwa mara nyingine tena alitoa hotuba. Baada ya kumsifu na kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema na amani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na familia yake (a.s.) akalihutubia jeshi hilo (pinzani): “Enyi watu! Mtume wa Mwenyezi Mungu amesema kwamba kama yejote mionganini mwenu ambaye anamuona kiongozi dhalimu akihalalisha yale aliyyaharamisha Mwenyezi Mungu, akivunja agano la Allah swt., akipinga Sunnah ya Bwana Mtume (s.a.w.w.), akiwatendea waja wa Mwenyezi Mungu kwa ukandamizaji na uonevu, na asifanye jitihada ya kurekebisha hali hiyo, basi itakuwa ni haki ya Mwenyezi Mungu kumtupa mja Wake kama huyo kwenye Moto wa Jahannam pamoja na huyo dhalimu.” Kwa njia hii Imam (a.s.) alibainisha sababu zake za kwa nini alisonga kuelekea Kufah.

Kisha majeshi yote yakaendelea na safari yao mpaka majibu ya ibn Ziyad juu ya barua iliyokuwa imetumwa na Hurr yalipowasili. Barua hiyo ilisomeka hivi: “Ukisha kuipokea barua yangu hii, muelekeze Husein na wafuasi wake hadi mahali palipokosa maji na malisho kisha uwaweke kizuizini hapo.”

(Kitab al-Irshaad)

KUWASILI KWA IMAM KARBALA

Imam alikuwa amekwishawasili kwenye bonde la Nainawa wakati barua hiyo ilipopokelewa. Imam aliyatambua yaliyokuwemo ndani ya barua hiyo. Alimwangalia Hurr kisha akasema: “Huzuni na iwe juu yako! Turuhusu tuchukue njia yetu hadi kwenye kijiji hiki au kwenye kijiji kingine cha Shafayyah.” Hurr akajibu: “Mimi sina uwezo wa kufanya hivyo. Mjumbe wa ibn Ziyad ananilinda kwa makini ili kutoa taarifa kwa ibn Ziyad ya iwapo kama ninatii maelekezo yake.”

Zuheir ibn Qayn alimsogelea Imam na akasema: “Itakuwa ni kwa upande wa upendeleo kwetu sasa kuwashughulisha watu hawa katika vita.” Imam (a.s.) akajibu: “Sipendi kuanzisha mimi mapigano.” Zuheir ndipo akashauri: “Kwa hali hiyo, kuna kijiji karibu na kingo za mto Furati ambako itakuwa inafaa kwetu sisi kuweka kambi.” Imam (a.s.) akauliza: “Kijiji hicho kinaitwaje?” Zuheir akajibu: “Kinaitwa Aqr – neno Aqr maana yake ni ‘jeraha.’ – Imam (a.s.) akasema: “Tunajikinga kwa Mwenyezi Mungu kutokana na arq (maangamizi).”

Imam (a.s.) alimgeukia Hurr na akasema: “Usituzuie sisi kwenda karibu na kingo za Furati.” Hata hivyo Hurr na jeshi lake wakajaribu kuzuia njia ya Imam (a.s.) vile makundi yote yalivyokuwa yakisonga mbele. Kipingamizi cha kupita kikazidi kuendelea mpaka yule farasi ambaye alikuwa amepandwa na Imam (a.s.) akakataa kusogea mbele. Imam alimtia chonjo farasi wake lakini hakusogea. Aliomba farasi mwingine badala yake lakini naye pia aligoma kusogea. Aliwaweka matandiko farasi kadhaa, mmoja baada ya mwingine lakini hakuna hata mmoja aliyejaribu kusogea.

Kwa kuona tabia hii ya ajabu, Imam (a.s.) aliulizia kuhusu jina la mahali hapa. Zuheir akasema: “Hapa panajulikana kama Taff.”

– Taff lina maana ya ‘ukingo wa mto.’ Imam (a.s.) akauliza, “Je pana jina jingine?” Jibu likawa: “Panaitwa *Sail al-Furat.*” – Sahil al-Furat ina maana ya ‘ukingo wa mto Furati.” Imam akauliza tena: “Je panajulikana kwa jina jingine tena?” Zuheir akajibu: “Ndio, panaitwa Karbala.”” Aliposikia jina la Karbala, Imam akashuka kwenye kipando huku akiwa anasema: “Ewe Allah! Tunajikinga Kwako kutokana na *karb* (huzuni) na *bala*’ (majonzi).”

Kisha Imam (a.s.) akakita mkuki aliokuwa ameushika mkononi mwake kwenye mchanga chini yake na akasema: “Hapa patakuwa ndio sehemu ya kupumzikia wanyama wetu. Hapa patakuwa ndio mahali yatakapokitwa mahema yetu. Hapa ndio mahali ambapo damu yetu itamwagika, ambapo wanawake wetu watakuwa mateka, mahali ambapo watoto wetu watakuwa mayatima na watatawanyishwa kwenye mawanda yote. Tutazikwa hapa na kutoka hapa tutakuja kufufuliwa mnamo Siku ya Kiyama.”

(Maqtal al-Husayn cha Khawarizmi)

Bibi Ummu Kulthum alikuja kwa kaka yake Imam Husein (a.s.) na akasema: “Ndugu yangu mpendwa! Nyika hii inaogopesha. Nahisi wasiwasi na upweke kwa hofu kubwa moyoni mwangu.” Imam (a.s.) akamtazama dada yake huyo na akasema: “Dada yangu mpendwa! Wakati tulipotoka na baba yetu kwenda kwenye viwanja vya mapambano vya Siffin tulipumzika mahali hapa hapa. Baba yetu aliweka kichwa chake kwenye paja la ndugu yangu al-Hasan (a.s.) na akapitiwa na usingizi kidogo. Mimi nilikuwepo wakati alipoamka na kuanza kulia. Al-Hasan akamuuliza, “Ewe baba! Ni kwa nini unalia?” Baba yetu akajibu: “Nimeliona jangwa hili kwenye ndoto kana kwamba limekuwa bahari ya damu na al-Husein alikuwa anazama kwenye damu hiyo huku akiomba msaada bila ya mtu yoyote kumjibu.” Kisha baba yetu alinigeukia mimi na akasema: ‘O Husein! Utakuja kufanya nini wakati utakapokabiliwa

na tukio kama hilo?" Mimi nilijibu kwamba nitakuja kuvumilia
kwa subira."'"

(*Ma'ali al-Sibtayn*)

Kuwasili kwa Imam (a.s.) hapo Karbala kulikuwa ni mnamo
mwezi 2 Muharram 61 A.H. Hapo aliweka kambi yake mpaka wakati
wa kifo chake cha Kishahidi.

(*Maqta al-Husayn cha Khawarizmi*)

MLANGO WA NNE

MATUKIO YA KARBALA KABLA YA SIKU YA ASHURA

KUWASILI KWA HABIB IBN MUDHAHIR HAPO KARBALA

Habib Ibn Mudhahir, Shi'ah mwenye ndeupe na maarufu wa Kufah alikuwa mionganini mwa watu wa Kufah waliokuwa wamemuandikia Imam kumualika kuja Kufah kuwaongoza watu dhidi ya Yazid. Alibakia mfuasi mwaminifu wa Imam (a.s.) hadi kifo chake.

Wakati Imam (a.s.) alipokuwa yuko njiani kuelekea Iraq, na aliposikia habari za kifo cha kishahidi cha Muslim ibn Aqil na ule usaliti wa watu wa Kufah, aliagiza kikundi cha wafuasi wake kubeba bendera zao. Bendera moja ilibakia. Alipoulizwa na sahaba mmojawapo kuhusu ni nani aliyekuwa mbebaji wa bendera ile iliyobakia, Imam alijibu kwamba mbebaji wa bendera hiyo hatimaye angewasili hivi punde tu.

Imam ndipo akamwandikia Habib. Barua hiyo ilisomeka hivi: "Kutoka kwa Husein mwana wa Ali kwenda kwa Habib ibn Mudhahir, mwanachuoni na faqih. Oh, Habib! Wewe unatambua uhusiano wangu na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu na unanijua mimi vizuri sana kuliko wengine. Wewe ni mtu wa msimamo na mtu huru. Usijibakishe nyuma katika kuja kunisaidia mimi. Mtume wa Mwenyezi Mungu awe mwenye kukulipa mnamo Siku ya Kiyama."

Barua hiyo iliibiwa kisirisiri kuingizwa Kufah na kufikishwa kwa Habib. Yeye alikuwa akifkiria namna ya kukwepa vituo vya ukaguzi vilivyowekwa na kuzunguka mji wa Kufah ili mwenyewe aweze kufika Karbala. Alikwenda kwa Muslim ibn Awsajah. Muslim, kama ilivyokwisha kuelezwu kabla, alikuwa ni wa kabila moja na Habib na wa umri mmoja naye, alikuwa amenunua henna ya kupaka kwenye ndeu zake. Habib akamwambia, “Wewe huna habari kwamba bwana wetu al-Husein amewasili Karbala na kwamba amezingirwa na maadui? Fanya haraka ili tumuwahi kabla hatujachelewa bado.” Muslim akaitupilia mbali ile henna na akasema kwamba atazipaka ndeu zake kwa damu yake mwenyewe katika kumnusuru Imam Husein. Usiku ule, watu wawili hawa wote walitoroka kwa siri kutoka Kufah na wakaenda kwa Imam (a.s.).

(Fursan al-Hayjan)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Imam aliweka pembeni bendera moja. Alipoulizwa kuhusu ni nani atakayekuja kubeba bendera hiyo, yeye Imam alijibu: “Yule atakayeibebe bendera hii yuko njiani anakuja.” Kwa wakati huo, wingu la vumbi lilionekana kwa mbali kidogo likiibuka kutoka ardhini kutokana na kwato za farasi anayekwenda shoti. Alipoliona hili, Imam alitabasamu akiwa bado ameishikilia bendera hiyo mkononi mwake. Yeye akasema: “Mbebaji wa bendera hii ni yule mtu anakuja kuelekea kwetu.” Na mwenye kipando huyo akakaribia, wakaona kwamba alikuwa ni Habib ibn Mudhahir. Habib akashuka kwenye kipando na akatoa salamu zake. Kisha akiwa anamwangalia Imam huku amejawa na machozi, akasema:

“Ingawaje nimekuwa mzee na nisije na uwezo tena, lakini kila ninapokuangalia wewe, basi ujana unaanza kumiminika kwenye mishipa yangu kwa mara nyingine tena.”

Aliposikia sauti za furaha zikitoka kwa wafuasi wa Imam, bibi Zainab aliuliza, “Huyo ni nani?” Akajibiwa akaambiwa, “Huyo ni Habib ibn Mudhahir.” Yeye akasema: “Nitoleeni salamu zangu kwake.” Salamu zake zilipofikishwa kwa Habib, alitingishwa na huzuni na simanzi kwa hasara ya kuondokewa inayomsubiri bibi huyo. Habib alilia na kujipiga usoni mwake kwa mikono yake alipokuwa akilalamika kwa huzuni: “Ah! simanzi ya hasara ya kuondokewa! Habib ni nani kwa bibi Zainabu kutolea salamu zake kwake yeye?” Inasemekana kwamba tukio hili lilitukia kabla ya Imam kuwasili Karbala.

(Ma’ali al-Sibtayn).

Wajibu mkubwa unaojitokeza ambao ulifanywa na Habib huyu katika jumla yote ya tukio la mageuzi ya Imam ulikuwa ni kwamba alijitahidi bila kuchoka katika kuwahamasisha watu kumuunga mkono Imam Husein (a.s.). Yeye alikuwa ndiye mfuasi mashuhuli sana wa Imam mjini al-Kufa katika kuwasihii watu kutoa kiapo cha utii kwa Muslim ibn Aqil (a.s.). Habib pia aliwatoa baadhi ya watu wa famillia yake na wengine kutoka kwenye kabilia lake kwenda kumsaidia Imam. Hawa wote waliuliwa katika siku ya Ashura. Baadhi ya watu ambao Habib ibn Mudhahir alikuwa amewapeleka ni:

1. Ndugu yake, Ali ibn Mudhahir
2. Binamu yake, Rabi’ah ibn Khawt
3. Suleiman ibn Rabi’ah Asadi
4. Anas ibn Harith

5. Muslim ibn Awsajah
6. Umar ibn Khalid Asadi
7. Sa'd, mtumwa alieachwa huru na Umar ibn Khalid
8. Mawqa' ibn Thumamah
9. Anas ibn Kahil Asadi
10. Mtumishi wake Habib Mudhahir

KUWASILI KWA UMAR BIN SA'D HAPO KARBALA

Wakati ibn Ziyad alipoarifiwa kuhusu hali ya Imam hapo Karbala, alimuandikia Imam barua kumtaka atoe kiapo cha utii kwa Yazid na kumtishia kwa kifo kama atakataa kutoa kiapo. Imam aliisoma barua hiyo na akaitupilia mbali. Alimwambia mjumbe wa Ibn Ziyad kwamba kwa madai kama hayo kulikuwa hakuna majibu.

Wakati majibu haya yalipowasilishwa kwa ibn Ziyad na mjumbe wake, yeye alighadhibishwa sana nayo. Alimwita Umar ibn Sa'd, ambaye kwa uchu sana alikuwa na kiu sana kwa ajili ya nafasi ya gavana wa ardhi ya Rayy. Alimuagiza: “Nenda kakomeshe jitihada za al-Husein na ndipo utaweza kudai ugavana wa Rayy kwa muda wa miaka kumi ijayo.” Umar aliomba usogezaji mbele wa siku moja ili kufikiria juu ya pendekezo hilo na akapewa ruhusa hiyo.

Umar alitafuta ushauri kutoka kwenye familia yake kuhusu suala hilo na wote walimpinga na kumkatisha tamaa. Hamzah ibn Mughirah mpwa wake Umar kutoka upande wa dada yake alimwambia: “Ewe ami yangu! Mimi nakusihi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu usitoke na kusonga mbele dhidi ya al-Husein (a.s.). Kumbuka kwamba una mafungamano ya kifamilia pamoja naye. Wallahi! hata kama utajiri wa ulimwengu mzima ungekuwa utolewe kupewa wewe, hautakuwa na thamani ya wewe kuwa na mchango katika mauaji ya al-Husein. Umar alikubali akisema: “Hayo unayosema ni kweli. Mimi sitafanya jambo kama hilo.”

Wakati wa usiku Umar alikuwa ameshughulishwa sana kama alivyokuwa akiwaza: “Hivi nisitoke kweli dhidi ya al-Husein na niachilie ugavana wa Rayy au niwe mmojawapo kwenye mauaji ya al-Husein na kuitwaa Rayy.” Usiku ule Umar alisikika akisoma shairi lifuatalo:

“Wallahi mimi sijui. Nimesimama katika mkanganyiko.
“Nimesimama kwenye njia mbili zenyehatari,
nikikabiliwa na kuchagua mojawapo.
“Niachane na Rayy wakati Rayy ndio tulizo la moyo wangu?
Au nimuue al-Husein na nirejee na mizigo ya dhambi?
“al-Husein ni mtoto wa ammi yangu na misiba ni mingi sana.
Naapa kwa Mola wangu! Rayy ni tunda (tufaha) la jicho langu.”

Uchu wa madaraka ya dunia yalikuwa tele kichwani mwake. Baada ya kudhamiria kutia doa mkono wake kwa damu ya Imam al-Husein (a.s.), alimalizia shairi lake kwa beti zifuatazo:

“Wanasema kwamba Allah ndiye Muumba wa Pepo na Moto,

Ile adhabu na mikono na ufungwaji nira za mikono

“Kama wako sahihi katika wanayoyasema, basi nitatubia kwa dhambi zangu

Kwa Mola Mwenye huruma, kwa miaka miwili baada ya kumuua Husein

“Na kama ni waongo katika wanayosema, basi mimi nitafuzu

Pamoja na milki kubwa na ufalme mkubwa uliopambwa kama maharusi.”

Asubuhi yake, Umar alikwenda kwa Ibn Ziyad na kumfahamisha juu ya kukubali kwake pendekezo la kupigana dhidi ya Imam Husein (a.s.). Umar bin Sa'd akiwa na jeshi la askari alfu nne hadi sita aliwasili Karbala mnamo mwezi 3 Muharram.

(*Maqta al-Husein cha Abu Mikhnaf*)

MAZUNGUMZO YA MJUMBE WA IMAM NA UMAR BIN SA'D

Umar aliwasili Karbala pamoja na jeshi lake. Mara tu akaweka aina zote za vikwazo juu ya kambi ya Imam Husein (a.s.), hata kuwazuia kuyafikia maji ya mto Furati.

Burayr ibn Hudayr, mfuasi wa Imam aliomba ruhusa ya kwenda kuongea na Umar kuhusiana na kule kuzuiliwa kwa maji. Alivyopewa ruhusa, Burayr alikwenda moja kwa moja kwenye hema la Umar na akaketi mbele yake bila ya kumtolea salamu. Umar alikasirishwa na ushupavu huu na akasema: “Je mimi sio Mwislam, na bado hukunisalimia? Burayr akajibu akasema: “Kama ungekuwa

Mwislam usingenyanya upanga wako dhidi ya familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kudhamiria kumuua al-Husein (a.s.) na kuifanya familia yake kuwa mateka. Hata nguruwe na mbwa wa mwituni wanakunywa maji ya mto Furati. Bado wewe unawazuia mwana wa Fatimah na familia yake wasipate njia ya kuyafikia maji hayo na kuwaangalia wakifa kwa kiu. Una haki gani baada ya haya yote ya wewe kujichukulia kwamba ni Mwislam? Umar aliinamisha kichwa chake na akasita akifikiri. Kisha akiinua kichwa chake akasema: “Ewe Burayr! nina uhakika kwamba yejote anayepigana dhidi ya al-Husein na familia yake, na akahuksika na vifo vyao atatupwa kwenye mashimo ya Jahannam. Lakini ni vipi nitatelekeza na kuuacha ugavana wa Rayy? Hivi mimi niiache Rayy ichukuliwe na watu wengine? Wallahi! moyo wangu hautalikubali hilo.”

Burayr alirudi kwa Imam na kumfahamisha yale yaliyojiri baina yake na Umar. Katika kuyasikia hayo, Imam akasema: “Yeye hataipata ardhi ya Rayy. Kwa hakika kabisa yeye atauliwa katika kitanda chake mwenyewe.”

MAZUNGUMZO YA IMAM NA UMAR BIN SA'D

Ili kuvishinda visingizio vya Umar ibn Sa'd kwa hoja za Mwenyezi Mungu, Imam alituma ujumbe kumualika aje wazungumzie juu ya hali hiyo. Umar aliukubali mwaliko huo na mkutano ukafanyika kati ya pande mbili hizo. Katika mazungumzo hayo, wote, Imam na Umar walihudhuria, kila mmoja akiandamana na watu ishirini. Kabla mazungumzo hayajaanza Imam aliwaomba sahaba zake wote, isipokuwa ndugu yake Abbas ibn Ali na mwanawewe Ali Akbar waondoke. Umar naye pia aliwaamuru watu wake waondoke isipokuwa mwana wa Hafs na mtumishi wake.

Imam (a.s.) akamwambia Umar: "Huzuni iwe ndio fungu lako! Ewe mwana wa Sa'd! Humuogopi Mwenyezi Mungu, ambaye Kwake utarejea? Je, utakwenda vitani dhidi yetu sisi? Wewe unanijua mimi vizuri. Mimi ni mwana wa Mtume, wa Fatimah na Ali. Oh, mwana wa Sa'd! Ondoka kwenye kambi ya Yazid na ujiunge nasi." Umar akajibu: "Ninahofia kwamba wataketeteza nyumba yangu." al-Husein (a.s.) akamjibu: "Kama wataketeteza nyumba yako mimi nitaijenga upya." Umar akasihi: "Watalitaifisha shamba langu." Kwa hili al-Husein (a.s.) alisema: "Hapo mimi nitakupa mto huko Baghibagha ambao Muawiyah alijaribu kuununua kwa dirham alfu moja." Ndipo Umar akatoa kisingizio: "Mimi nina familia na ninahofia juu ya usalama wao." Kwa hili Imam alinyamaza kimya na hakumjibu. Lakini wakati alipokuwa akiondoka kwenye mkusanyiko huo, ye ye alisema: "Mwenyezi Mungu akufanye wewe uuliwe kitandani mwako! Yeye asikusamehe wewe katika Siku ya Kiyama! Jaaliwa usifaidi hata ukufi wa kiganja kimoja cha ngano ya Rayy!" Umar akajibu kwa kejeli akisema: "Nitajitosheleza mwenyewe kwa shayiri."

Huu ndio ulikuwa mtazamo wa Umar kwamba ingawa alihofia juu ya usalama wa familia yake, alikuwa hana habari na familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Bibi Fatimah (a.s.). Humayd ibn Muslim amesimulia: "Mimi nilikuwa rafiki wa Umar bin Sa'd. Baada ya matukio ya Karbala, nilikwenda kwa Umar na kumjulia kama alikuwa na hali gani. Yeye alisema: "Hakuna mtu fidhuli zaidi kuliko mimi ambaye anarudi nyumbani akiwa amebeba mzigo wa dhambi kubwa, nikiwa nimevunja mahusiano yangu ya kifamilia na kumuua mwana wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)." Umar alikuwa na undugu na Imam kupitia baba yake Sa'd, ambaye alikuwa anatokana na kizazi cha Abd al-Manaf.

(Ma'ali al-Sibtayn)

BARUA DANGANYIFU YA UMAR BIN SA'D KWA IBN ZIYAD NA MAJIBU YAKE

Mnamo mwezi 7 Muharram, Amr ibn Hajjaj akiwa na kikosi cha askari wapanda farasi mia tano alikuwa akilinda kingo za Mto Furati kumzuia Imam na wafuasi wake wasiweze kupata maji.

Wakati huo huo Umar ibn Sa'd alikuwa na matumaini ya kuiamua hali hiyo kwa amani kabisa. Aliandika barua ya udanganyifu kwa Ibn Ziyad ambayo ilieleza kwamba: "Al-Husein yupo tayari kufuata moja ya njia tatu: kurejea Madina au kwenda kwenye moja ya vituo vya mpakani mwa himaya ya Kiislam, au kukutana na Yazid na kufikia namna fulani ya mapatano naye. Kwa vile suala lenyewe ni hilo, tatizo limetatuliwa na pia itakuwa kwa faida ya Ummah."

Hili lilikuwa ni jambo lililohusishwa na Imam kwa uongo kabisa na Umar bin Sa'd. Hii ni dhahiri kutokana na maneno ambayo Imam alikuwa akiyasema mara kwa mara: "Mwana wa haramu wa baba wa haramu ameniacha na machaguo mawili: kifo au fedheha. Hiyo fedheha na iwe ni jambo mbali sana nasi! Mwenyezi Mungu haturuhusu sisi kwa hili, wala Mtukufu Mtume wala waumini."

Wakati barua ya Umar ibn Sa'd ilipomfikia Ibn Ziyad, yeye alimsifu Umar akisema: "Hii ni barua ya mtu ambaye ameweka mbele maslahi ya watu moyoni mwake." Ibn Ziyad alikuwa akikusudia kujibu barua hiyo kwa kuikubalia. Hata hivyo Shimr ibn Dhi Jawshan alimvunja moyo. Yeye alisema: "Je utayakubali haya kutoka kwa Umar Ibn Sa'd baada ya al-Husein kuwa amevamia ardhi yako na akakataa kutoa kiapo cha utii kwako? Kama matokeo ya maelezo ya Shimr, ibn Ziyad alibadili mawazo yake na akaandika barua ifuatayo kumjibu Umar: "Sikukutuma Karbala kwenda kujadili mkataba au makubaliano na kuchelewesha mambo bila ya

sababu ya maana. Kama Husein akikubali masharti yangu ya kutoa kiapo cha utii kwangu, mlete kwangu kama mateka. Vinginevyo mbughudhi na uingie vitani naye. Baada ya kuuliwa kwake fanya mwili wake ukanyagwe kanyagwe chini ya kwato za farasi. Endapo utatii maelekezo yangu, basi utakuwa na stahiki ya kuwa gavana. Vinginevyo kabidhi hatamu za uongozi kwa Shimr.” Barua hii alipewa Shimr na alitolewa pamoja na jeshi la wapiganaji alfu nne kwenda Karbala.

Katika kuwasili kwake Karbala, Shimr aliikabidhi barua hiyo kwa Umar ibn Sa’d. Baada ya kuisoma, Shimr alimwambia: “Umeamua nini? Je, utatekeleza amri za gavana au nichukue uongozi wa jeshi ili nitekeleze amri zake?” Umar ibn Sa’d akajibu: “Sitakabidhi kamwe ukamanda wa jeshi kwako wewe. Heshima kama hiyo imehifadhiwa kwa ajili yangu mimi. Wewe utakuwa mkuu wa askari wa miguu.

(at-Taarikh Tabari)

HABIB IBN MUDHAHIR ANAJARIBU KUPATA KUUNGWA MKONO NA BANI ASAD

Kitendo kingine cha uaminifu cha Habib ibn Mudhahir kwa niaba ya Imam kilikuwa kile cha mwezi 7 au 8 Muharram wakati walipokuwa Karbala. Aliomba ruhusa kutoka kwa Imam (a.s.) ya kwenda kijiji cha jirani na kuwaalika watu wa kabilia lake, Banu Asad kuja kumsaidia Imam (a.s.). Baada ya kuruhusiwa, Habib aliwaendea Banu Asad na kuelezea hali halisi ilivyokuwa. Yeye alisema: “Kama mnapenda furaha ya dunia hii na ile ya Akhera, basi njoo ni kumsaidia Husein. Wallahi, yule ambaye anauliwa akimtetea Husein atawekwa katika safu za juu kabisa za Pepo na atapata nafasi karibu na Mtukufu Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Abdallah ibn Bashshar amesimulia: “Mimi nilikuwa wa kwanza kujitolea kutoka Bani Asad. Nilisoma mashairi ya kusifia kumsaidia Imam Husein (a.s.). Kwa matokeo ya hilo, watu tisini wengine walismama na kutangaza kuwa tayari kwao kwenda kumsaidia Imam Husein (a.s.).”

Taarifa ya tukio hili kwa namna fulani ilifikishwa kwa Umar ibn Sa’d na mmoja wa wapepelezi wake. Ibn Sa’d ndipo akatumia watu mia nne chini ya ukamanda wa Azraq kwenda kuwakomesha na kuwazuia wasifike kwa Imam. Azraq aliwazuia njiani Bani Asad kwenye kingo za mto Furati na vita ikazuka baina yao.

Habib alimwita Azraq, “Ewe Azraq! Sio sahihi kwetu sisi kupigana wenyewe kwa wenyewe. Achia mtu mwingine achukue mamlaka ya jeshi lako na apate laana ya Mwenyezi Mungu.” Azraq hakujali ushauri wa Habib na mapigano yakaendelea. Bani Asad hawakuweza kutoa upinzani mkubwa kutokana na udogo wa idadi yao. Matokeo yake baadhi yao waliuliwa wakati wengine waliokoa maisha yao kwa kukimbilia kwenye sehemu za usalama. Habib ibn Mudhahir alimudu kurejea kwa Imam na kumjulisha juu ya yale yaliyojiri. Imam (a.s.) akasema: “Hakuna nguvu wala uwezo ila kupitia kwa Mwenyezi Mungu, aliye Mkuu, Mwenye nguvu.”

MATUKIO YA MWEZI 9 MUHARRAM

Jioni ya mwezi 9 Muharram Umar ibn Sa’d alitoa maelekezo yafuatayo kwa jeshi lake: “Enyi wapiganaji wa Mungu, pandeni kwenye vipando vyenu na mpokee habari njema za Peponi. Yazungukeni mahema ya al-Husein na muwazingire na kuwashambulia.”

Wakati huo huo Imam (a.s.) alikuwa ameegemea kwenye mkuki wake nje ya hema lake wakati akipitiwa na usingizi wa mara kwa mara. Imam alimuona Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) akimwambia: “Oh

Husein! Adui amefika karibu nasi!” Imam mara moja akaamka na akamwita ndugu yake Abbas Ibn Ali. Akamwagiza atoke nje kwenda kwa maadui hao na kuwauliza ni kwa nini wamesonga mbele kuwajia wao.

Abbas ibn Ali pamoja na Zuheir ibn Qayn, Habib ibn Mudhahir na wafuasi wengine kumi na nane walipanda vipando na kuwaendea maadui na kuwauliza sababu ya wao kuwajia kwenye mahema ya Imam (a.s.). Walijibu kwamba wao wameamrishwa kumtaka Husein akubaliane na madai ya ibn Ziyad au waingie kwenye mapambano. Abbas ibn Ali alirudi kwa Imam na kumjulisha juu ya majibu hayo, wakati Habib na Zuheir wakisimama na jeshi hilo wakiwaonya askari wake.

Katika mazungumzo hayo, Habib ibn Mudhahir alitambua ni kiasi gani tabia zao zilivyokuwa za kifidhuli na akasema: “Wallahi ninyi ni watu waovu. Ni watu ambao mnamo Siku ya Kiyama mtafuliwa kama wauaji wa Nyumba ya Mtukufu Mtume. Mtajulikana kama wauaji wa hawa waja waadilifu wa Mwenyezi Mungu.” Mtu mmoja aliyeitwa Azrah alimjibu kwa kusema: “Ewe Habib! Je, umejisafisha na dosari na kujifunza mwenyewe maadili mema ya hali ya juu?” Kwa hili Zuheir alijibu na kusema: “Mwenyezi Mungu amemtakasa na kumuongoza Habib, bwana wewe! Ogopa ghadhabu za Mwenyezi Mungu na twaa uchamungu. Nakuonya usiwe upande wa batili dhidi ya haki na ukweli.”

Wakati huo kwenye kambi ya Imam (a.s.), Imam alimwangalia Abbas na akasema: “Nafsi yangu itolewe muhanga kwa ajili yako! Ewe Abbas! Hebu waendee na uwaombe siku moja ya nafasi kwa ajili ya sisi kufanya ibada za Mwenyezi Mungu na kufanya maombi na du'a Kwake, kwani Yeye anajua jinsi Husein anavyotamani kumuabudu Yeye, kusoma Kitabu Chake na kujishughulisha katika mazungumzo ya siri pamoja Naye.”

Abbas ibn Ali alirejea kwa adui na akafikisha maombi ya Imam (a.s.) kwao. Ujumbe huo ulipelekwa kwa ibn Sa'd ambaye alitafuta maoni ya maafisa wake. Baadhi yao walikuwa na maoni kwamba vita vianzishwe bila kuchelewa wakati wengine kama Amr ibn Hajjaj walisisitiza kwamba nafasi itolewe wakisema: “Mwenyezi Mungu atukuzwe! Kama madai ya namna hii yangetolewa na makafiri wa Daylam mngeweza kuwakubalia hao.” Hatimae iliamuliwa kumpa Imam (a.s.) haki ya fursa hiyo na ujumbe ukatumwa kwake kwamba ama awe amesalimu amri asubuhi yake au ajiandae kwa mapambano.

KUKATALIWA KWA HATI YA USALAMA

Katika siku hiyo hiyo ya mwenzi 9 Muhamarram, Shimr alikuja karibu na kambi ya Imam (a.s.) na akaita kwa sauti, “Wako wapi wana wa dada yangu?” Abbas, Ja’far, Uthman na Abdullah watoto wa Imam Ali (a.s.) na Ummu al-Banin walijitokeza mbele na kumuuliza Shimr kwamba alikuwa anataka nini. Yeye akaguta kwa sauti, “Enyi wana wa dada yangu! Mimi nawatunuku hati ya usalama.” Ndugu hao wa Imam (a.s.) walimjibu kwa sauti kubwa: Mwenyezi Mungu akulaani wewe na hati yako ya usalama! Unatupa sisi hati ya usalama wakati ambapo mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hana hifadhi wala pa kukimbilia?”

(*Kitab al-Irshaad*)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, wakati pendekezo la hati ya usalama lilivyotolewa kwa Abbas ibn Ali, yeye alijibu: “Mikono yako nainyaukilie mbali! Ewe adui wa Mwenyezi Mungu! Hivi unatutaka sisi tumtelekeze Maula wetu al-Husein, mwana wa Fatimah na tuijunge na watoto waliolaaniwa na wa yule aliylaaniwa?”

(*Nafs al-Mahmuum*)

Bado kuna riwaya nyingine inayoleza kwamba wakati mnamo mwezi 10 Muharram (ile siku ya Ashura), Imam alikuwa amepanda juu ya farasi wake na alikuwa akikaribia kuingia vitani, Shimr aliita: “Enyi wana wa dada yangu! Msikubali ninyi wenyewe kuuliwa pamoja na al-Husein. Tokeni na njooni mjiunge na sisi chini ya bendera ya Amir wa waumini, Yazid!” Abbas ibn Ali akajibu: “Na uangamie wewe! Hivi sisi tumtelekeze bwana na ndugu yetu na kutoa kiapo cha utii kwa waliolaaniwa pamoja wa watoto wao?”

(Muthir al-Ahzan)

Kutokana na hili itaonekana dhahiri kwamba Shimr alitoa pendekazo la hati ya usalama katika siku ya mwezi 9 Muharram na mwezi 10 Muharram pia, lakini lilikataliwa katika matukio yote na Abbas ibn Ali na ndugu zake (a.s.).

MATUKIO YA MKESHA WA ASHURA

Imam Ali ibn al-Husein Zayn al-Abidiin (a.s.) alisimulia: “Vile usiku wa Ashura ulipotandaza joho lake kwenye upeo wa macho, Imam al-Husein (a.s.) aliwakusanya wafuasi wake. Wakati wanaume wa kam-bi hiyo walipokusanyika karibu yake, ye ye alimtukuza Mwenyezi Mungu na kumuombea rehema na amani Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na kizazi chake (a.s.). Kisha aliwahutubia akisema: “Kwa hakika si-jawajua wafuasi wa mtu yoyote yule walio bora na waaminifu kuliko wangu mimi na wala sijajua familia yenye thamani na ya wacha-mungu kuliko yangu. Namuomba Mwenyezi Mungu awajaalie ninyi wote malipo makubwa kwa niaba yangu! Enyi watu! Jueni kwamba mimi nimepoteza matumaini kwa watu hawa (wa Kufa). Wao wana kiu na damu yangu. Iwapo mtaishi au kufa mimi sitaachwa. Enyi watu! Kwa hiyo jueni kwamba nimewaondolea ule wajibu wa kiapo

cha utii ambacho mmenipatia mimi. Tumieni giza la usiku huu kama kinga na mjiokoe nafsi zenu wenyewe.”

Kufikia hapo, Abbas ibn Ali pamoja na ndugu wengine wa Imam (a.s.), watoto na wapwa zake walijkusanya karibu naye. Walisema kwamba maisha ambamo hakuwemo Husein hayakuwa na thamani ya kuishi. Wakati Imam alipoyaona majibu haya kutoka kwa watu wa karibu sana wa ukoo wake, Banu Hashim, aliwageukia watoto wa yule aliyeuliwa kikatili kabisa, Muslim ibn Aqil na akasema: “Enyi watoto wa Aqil! Kifo cha Muslim ni hasara ya kuondokea kubwa kabisa ya kutosha kwenu ninyi. Ninawapa ruhusa ya kuokoa na kubakisha maisha yenu!” Wao walijibu: “Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu! Je, sisi tumtelekeze mkuu wetu, maula wetu na ami yetu, ambaye mfano wake dunia haijawahi kushuhudia kuona? Hivi tusipigane kwa panga, mikuki, mishale katika kukulinda wewe kutokana na watu hawa mafidhuli? Hasha! Sisi tutayatoa maisha yetu, watoto wetu, wanawake zetu, utajiri na mali zetu kwa ajili yako. Tutapigana bega kwa bega na wewe na kwenda popote utakapokwenda wewe. Mwenyezi Mungu asiyafanye maisha kuwa na thamani kuyaishi bila ya wewe.”

Kutoka mionganini mwa wale wasiokuwa Bani Hashim, Muslim ibn Awsajah alisimama na kusema: “Hivi sisi tukuache peke yako mikononi mwa wale maadui wa Mwenyezi Mungu? Ni kisingizio gani tutakachompa Mwenyezi Mungu kwa kutokukulinda wewe? Tutakulinda hadi mwisho kiasi kwamba itakuja kuwa dhahiri kwamba tulitetea hadhi ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuititia kwako. Oh, Husein! Elewa kwamba kesho nitapambana na maadui zako kwa mkuki wangu. Utakapovunjika nitapambana kwa upanga wangu madhali utakuwa umebakia mikononi mwangu. Wakati upanga wangu utakapovunjika nitawarushia mawe. Oh Husein! Wallahi kama wakikata mikono yangu na kuniua mimi na kunichoma na

kisha kunihuisha mara sabini, sitaacha kukutetea wewe. Oh Husein! Bali kuna kifo kimoja tu na kukionja kwa ajili yako ni heshima kubwa sana.”

Baada ya Muslim ibn Awsajah, ndipo Zuheir akasimama na kusema: “Naapa Wallahi, ewe Husein kwamba sitaki chochote zaidi ya kuuliwa mara alfu moja ili kukuokoa wewe pamoja na familia yako kutoka kwenye mikono ya wale watu wasio na mungu.”

Wengine pia walismama kwa zamu na kuongea maneno yenye athari moja kama hiyo. Imam (a.s.) aliwashukuru mmoja baada ya mwingine na kuwaombea.

(Kitab al-Irshaad)

“Ni ubora uliokuwaje wa ujana wa watu ambao walivumilia katika subira,

mfano wake ambao sijawahi kuuona kamwe mionganii mwa watu.

“Wale walikuwa watu wachamungu waungwana kama maziwasi safi

kinyume na maji machafu yakigeuka kuwa mkojo baada ya kunywewa.”

(Nafas al-Muhmuum)

TANGAZO LA IMAM JUU YA KUDHIHIRI KWA IMAM MAHDI (A.T.F.S.)

Kuna riwaya kutoka kwa Imam Muhammad ibn Ali al-Baqir kwamba baada ya wafuasi wa Imam al-Husein kuonyesha uaminifu wao kwake, yeche aliisema: “Wallahi! pokeeni habari njema za Peponi.

Wallahi! baada ya kuwa tumekwisha kuuliwa, muda fulani utapita ambao baada yake tutahuishwa kwa mara nyingine tena. Huo utakuwa ni wakati wa kudhihiri kwa al-Qa'im kutoka mionganini mwetu. Yeye atachukua kisasi kwa maadui zetu na sisi tutashuhudia adhabu hiyo ikitolewa kwao.”

Mtu mmoja akauliza, “Ni nani huyo al-Qa'im kutoka mionganini mwenu?” Imam akajibu, “Yeye atakuwa ni kizazi cha saba kutoka kwenye nasaba ya Muhammad al-Baqir na atakuwa ni al-Hujjah ibn al-Hasan. Baada ya kutokuwepo kwa kipindi kirefu, yeye atarejea na atasababisha amani na uadilifu kuenea katika kila sehemu ya dunia kama vile tu itakavyokuwa imejawa na dhulma na ukandamizaji kabla yake yeye.”

(Maqtal al-Husein al-Muqarram)

Imesimuliwa pia kwamba Imam aliomba du'a kwa ajili ya wafuasi wake kwenye usiku wa ule na akawaonyesha nafasi zao za juu kabisa ndani ya maeneo ya peponi. Udhamini na kuridhika kwao kuliongezwa kwa kile walichoonyeshwa. Hivyo ile hofu ya kifo iliondolewa kutoka kwenye nyoyo zao kwa kiasi kwamba walishindana wao kwa wao katika kusonga mbele kwenye medani ya vita ili kupata shahada.

MACHUNGU MAKALI YA BIBI ZAINAB KATIKA USIKU WA ASHURA

Imam Ali ibn Husein Zayn al-Abidiin (a.s.) alisimulia kwamba: “Nilikuwa nimepumzika katika ule mkesha wa Ashura wakati shangazi yangu Zainabu akiniganga. Tulimsikia baba yangu, al-Husein (a.s.) akiingia kwenye hema lake ambamo Jawayr, mtumishi wa siku ny- ingi wa Abu Dharr alikuwa anatayarisha upanga wake na kuufanyia

marekebisho. Kwa wakati ule baba yangu alisoma beti zifuatazo kuhusu hali ya kukosekana uaminifu katika dunia hii:

“Ewe wakati! Aibu iwe juu yako kama rafiki!

Katika machweo ya siku na kuzama kwa jua.

“Ni masahaba wangapi au wakutafutao wewe watakuwa mizoga!

Wakati hautaridhishwa kwa mbadala wowote.

“Hakika jambo lenyewe litakuwa kwa Yule Mwenye nguvu,

Na kila kiumbe hai kitatembea katika njia yangu”

(Ubeti huu wa mwisho umesimuliwa pia kwa namna ifuatayo:

“Hakika ile ahadi ya kuondoka imewadia,

Na jambo lenyewe linabakia na Yule Mwenye nguvu Mmo-ja).

Imam (a.s.) alizirudia kuzisoma beti hizi mara mbili au tatu. Nilizisikia beti hizi na nikatambua alimaanisha nini. Machozi yalinitiririka na nikayarudisha nyuma. Nilinyamaza kimya na nikajua kwamba majonzi yametufika. Kuhusu shangazi yangu, yeye alisikia kile nilichosikia mimi. Hakuweza kujizuia. Yeye aliruka huku akichana nguo zake na kushusha pumzi kwa wingi alipokuwa akikimbilia kwa Imam huku akiguta kwa sauti kubwa: “Hivyo nitapoteza na kumkosa kaka yangu! Kama tu kifo kitaninyang’anya uhai wangu siku ya leo. Mimi ninaye wewe tu, kwani mama yangu, baba yangu na kaka yangu wote wamekwisha kufariki.”

Imam akamwambia huku akimuangalia na machozi yakijaza macho yake: “Ewe dada yangu! Usimfanye shetani akupore uvumilivu wako. Kama kwale wa michangani wakiachwa wenyewe usiku basi watalala.” (yaani wacha maumbile yachukue mkondo

wake). Zainab alilalamika alipokuwa akijipiga usoni na begani ili kuchana nguo zake. “Oh huzuni yangu! Uhai wako utavutwa vibaya sana kutoka mwilini mwako na hilo linajeruhi sana moyoni mwangu na ni kali sana kwa nafsi yangu.”

Shinikizo la kimhemko la tukio hili lilimzidi sana na akazimia. Imam (a.s.) alimnyunyizia maji usoni na akamliwaza huku akisema: “Oh dada yangu! Muogope Mungu na pata faraja katika uliwazaji wa Mwenyezi Mungu. Fahamu kwamba watu wa dunia watakuwa na wakazi wa Mbinguni wataishi milele. Kila kitu kitafika mwisho isipokuwa wajihii wa Mwenyezi Mungu (swt). pekee. Babu yangu alikuwa mbora kuliko mimi; baba yangu, mama na kaka yangu wote walikuwa wabora kuliko mimi. Lakini bado Mwenyezi Mungu amewachukua wote. Kila Muislam pamoja na mimi tutafuata kigezo cha mfano wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Ewe dada yangu! Nakusihu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu usichane nguo zako kwa huzuni baada ya kifo changu na kujikwaruza usoni mwako.”

Baada ya haya, baba yangu alimleta Zainab kwenye hema langu na kisha akarejea kwa masahaba zake.

(Kitaab al-Irshaad)

KUJIZATITI KWA IMAM NA WAFUASI WAKE KATIKA USIKU WA ASHURA

Inasimuliwa kwamba Imam (a.s.) na wafuasi wake katika mkesha wa Ashura walikuwa wamezama katika swala na ibada mbalimbali. Baadhi yao walionekana wamesimama, wengine wameinama katika rukuu, wengine walikuwa wanajudia Mwenyezi Mungu na wengine walikuwa wakishughulika na kusoma Qur’ani na du’aa za siri. Mrindimo wa maombi na du’aa zao ulifanana na mvumo wa nyuki.

Ilikuwa ni sauti hizi zenyenye mguso wa moyo za ibada ambazo zilikuwa zikitoka nyoyoni mwa wapenzi waaminifu wa Mwenyezi Mungu swt. ambazo zilimudu kugeuza watu thelathini na wawili kutoka kwenye jeshi la Yazid na kuja upande wa Imam Husein (a.s.).

(Nafas al-Muhmuum)

TUKIO LA NAFI'I IBN HILAL KWENYE USIKU WA ASHURA

Baadaye kabisa katika usiku wa mkesha wa Ashura, Imam (a.s.) alitoka kwenye hema lake kwenda kukagua mawanda tupu ambamo vita vilikuwa vije kupiganwa katika siku inayofuatia. Nafi'i ibn Hilal alimuona Imam na akasimulia: ‘Kwa kuona Imam alikuwa peke yake, nilimfuata ili kumlinda endapo adui atamshambulia. Imam (a.s.) akatambua kwamba nilikuwa ninamfuatilia nyuma yake naye akanigeukia na kusema: “Wewe kwa nini umetoka nje?” Mimi nikajibu: “Nilikuwa nikihofia kwamba huenda maadui wakakushambulia kutokea upande wa nyuma.” Yeye akaniambia: “Mimi nimekuja kukagua ardhi zilizonyanyuka na mitaro katika mawanda haya ili niweze kujizoesha na sehemu ambazo maadui wanaweza wakajificha wakisubiri kutuvamia wakati vita vitakapoanza kesho.”

Kisha wakati Imam na mimi tulipokuwa tukirejea, alinishika mkono wangu na akasema: “Lililoamuliwa litakuja kupita. Ahadi ya Mwenyezi Mungu haiwezi kuvunjwa.” Akaendelea zaidi, “Wewe hupendi kutoroka kwa kutumia giza la usiku huu na ukaokoa maisha yako?” Kwa hili nilianguka miguuni mwake na huku nikitokwa na machozi nikajibu: “Mama yangu ajaaliwe kulia kwenye kifo changu kama ningekuwa nikutelekeze wewe! Mwenyezi Mungu amenitunuku kwa kunifanya niwe pamoja nawe. Mimi sitakuacha wewe hadi nitakapokatwa vipande vipande kwa ajili yako.”

Baada ya haya Imam (a.s.) alikwenda kwenye hema la dada yake ambako Zainab alikuwa anamsubiri yeye. Nilimsikia yeye Zainab akimwambia Imam (a.s.): “Je umewajaribu wafuasi wako, kwani nahofia kwamba watakutelekeza katika saa yako ya haja? Imam (a.s.) akajibu, “Wallahi! mimi nimeujaribu uaminifu wao. Wenye wote wana shauku ya kufa kwa ajili yangu kama mtoto alivyo kwa kifua cha mama yake.”

Nilipoyasikia mazungumzo hayo na Bibi Zainab mimi nililia sana na kutokwa na machozi. Kisha nikaenda kumuelezea Habib ibn Mudhahir kuhusu hayo. Habib akasema: “Wallahi! Kama isingekuwani kuwahikabla yaamri ya Imam(a.s.), ningemshambulia adui wakati huu huu hasa.” Mimi nikasema: “Nahisi ni wanawake ndani ya mahema ambao wanamsababishia Zainab wasiwasi na mshughuliko huu. Inafaa kwamba tungewakusanya wanaume na kumliwaza kwa kuzungumzia juu ya uaminifu na utiifu wetu kwa ndugu yake.”

Habib ibn Mazahir aliwakusanya wanaume hao na kuwaelezea kuhusu hali hiyo. Wote walikuwa na shauku kuruhusu utayari wao kuingia kwenye mapambano na kuonyesha dhamira yao isiyotikisika ya kufa kwa ajili ya al-Husein (a.s.). Habib aliwaombea wote kwa Mungu.

Kisha wote tukaenda kwenye mahema ya wanawake hao na tukaita: “Enyi wanawake wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) wa Mwenyezi Mungu swt.! Hizi ni panga za watetezi na walinzi wenu ambao wameapa kutorudisha panga zao kwenye ala zao bila kumkata adui yenu! Hii ni mikuki yao ambayo wameapa kwamba haitaanguka chini bali itatumbukizwa kwenye mioyo vifuani mwa maadui.” Kwa hili, wanawake wakilia na kupiga mayowe walitoka mbio kutoka kwenye mahema yao wakisema: “Enyi wapiganaji wakweli na safi! Lindeni heshima ya mabinti

na wanawake wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.), nabii wa Mwenyezi Mungu swt. na Amirul-Mu'mini (a.s.)” Wote sisi tulilia na kuwaliwaza.

(Maqta al-Husein al-Muqarram)

KULETA MAJI

Katika ule usiku wa Ashura, wakati maji katika kambi ya Imam (a.s.) yalipokuwa yamekwisha, ye ye alimuelekeza mwanawe Ali Akbar pamoja na wafuasi wake takriban thelathini na mbili kuelekea Mto Furati na kuleta maji. Walikwenda katika mazingira hatari kabisa na wakarudi na maji. Pale waliporejea, Imam aliwaambia wafuasi wake wanywe maji hayo na kuchukua udhuu. Wafue na nguo zao vilevile kwani zitakuwa ndio sanda zao.

(Nafsi al-Mahmuum)

Imesimuliwa vilevile kwamba Imam (a.s.) alimtuma ndugu yake Abbas ibn Ali pamoja na watu thelathini juu ya farasi na ishirini wa miguu kwenda kuleta maji. Waliufikia Furati kwa siri wakiwa wamebeba mifuko ya ngozi. Walipokuwa wanajaza mifuko hiyo ya maji, Amr ibn Hajjaj, ambaye alikuwa ndio kiongozi wa askari waliokuwa wanalinda mto Furati aliwaona. Akasema: “Mnawenza mkanya wa maji kwa kiasi chochote mnachotaka lakini hamruhusiwi kubeba kiasi chochote cha maji kuondoka nacho hapa.” Abbas ibn Ali na wenzie hawakutilia maanani onyo hilo na baada ya kujaza mifuko hiyo ya ngozi wakaelekeea kwenye mahema. Walivyokuwa wanaondoka kutoka kwenye mto Furati, maadui walifunga njia yao na mapambano yakazuka. Wengi wa maadui wakauliwa hapo lakini wote katika kundi la Abbas hawakupata hata mikwaruzo. Imam (a.s.), familia yake na wafuasi wake, wote walikunywa kutokana na

maji yale yaliyoletwa na Abbas. Ilikuwa ni kwa sababu hii ambapo Abbas anajulikana kwa jina la ‘*Saqqa*’ (mletaji maji).

(*Kibrit al-Ahmar*)

KUCHIMBA MTARO

Imam (a.s.) aliwaelekeza wafuasi wake kusogezza mahema yao karibu kabisa na hema lake na kuyaweka mbele ya mahema ya wanawake. Kisha akafanya uchimbwe mtaro nyuma ya mahema hayo, ambao ulijazwa kuni na matete. Halafu aliamuru kwamba hivyo vichomwe moto. Hili lilifanyika ili kuzuia mashambulizi kutokea nyuma ya mahema.

(*Kibrit al-Ahmar*)

MAJADILIANO YALIYOFANYIKA USIKU WA MANANE

Bibi Zainab alisimulia: “Ilikuwa ni usiku wa manane katika mkesha wa Ashura wakati nilipokwenda kwenye hema la kaka yangu Abbas ibn Ali. Nilisikia mvumo wa sauti ya chini wa mazungumzo ukija kutoka ndani ya hema lake hilo. Hivyo nilinyanya ile nguo kwenye ule uwazi wa kuingilia wa hema hilo na nikaangalia ndani yake. Nilimuona ndugu yangu katikati ya hema akitambaa kwa magoti yake akifutafuta upanga wake ambapo Bani Hashim wengine walikuwa katika mduara kumzunguka ye. Aliwaita wote: ‘Enyi ndugu na binamu zangu! Kesho wakati vita vitakapoanza, ninyi mtakuwa wa mwanzo kabisa katika kuyatoa maisha yenu, isije watu wakasema Bani Hashim waliyapenda maisha yao zaidi ya yale ya wafuasi wengine wa Imam al-Husein (a.s.).’” Bani Hashim hao wakamjibu, “Sisi

tutafanya kama unavyoamuru.' Nilishindwa kujizuia kwa hili na si-kuweza kuyarudisha nyuma machozi yangu.””

Baada ya haya nilirejea kwenye hema langu. Nikiwa njiani nilisikia mvumo wa sauti kama ule ukitoka kwenye hema la Habib ibn Mudhahir. Nilinyanya ile nguo kwenye mlango wa hema lile na nikachungulia ndani. Nilimuona Habib kama vile nilivyomuona ndugu yangu Abbas na wenzake, wafuasi wa Imam al-Husein (a.s.) wakiwa kwenye mduara kumzunguka yeye. Habib aliwaita wote: “Enyi wafuasi wa al-Husein! Kesho wakati vita vitakapoanza, ninyi mtakuwa wa kwanza kusonga mbele ili kuutoa uhai wenu kabla ya Bani Hashim. Wao ni viongozi wetu na mabwana zetu.” Masahaba hao wakajibu: “Tutafanya kama unavyoamuru wewe.” Nilizidiwa na mhemko na niliridhika kwamba ndugu yangu hatatelekezwa.

(Kibrit al-Ahmar)

TUKIO PAMOJA NA BARAYR IBN HUDAYR

Ikielekea mapambazuko katika mkesha wa Ashura, Imam (a.s.) ali-paka manukato kwenye mwili wake ambayo yalikuwa na harufu ya miski. Burayr ibn Hudayr na Abd al-Rahman ibn Abd Rabbih wali-kuwa wakisubiri zamu yao ya kuchukua udhuu nje ya hema. Burayr alifanya mzaha na Abd al-Rahman. Mwenzie akamwambia kwamba ule haukuwa usiku wa kwa ajili ya maskhara na mchezo. Burayr akamjibu: “Watu wangu wanatambua kabisa kwamba mimi sijawa kamwe mmoja wa wale wanaojishughulisha na vichekesho. Furaha ambayo unayoiona kwangu wakati huu ni kutokana na ufahamu kwamba hivi karibuni nitauawa kishahidi na kisha nitafungiwa ndoa na wanamwali wa mbinguni na kusherehekeea ndani ya Pepo.”

(Muthir al-Ahzan)

NDOTO ALIYOIOTA IMAM

Mapambazuko ya Ashura yalipokuwa yanakaribia, Imam (a.s.) alilala kwa muda kiasi. Kisha akaamka na kuwaambia wale waliokuwa karibu yake, “Nimeota ndoto. Kundi la mbwa wa mwitu lilikuwa likinishambulia. Miongoni mwao alikuwepo mbwa mwenye mabaka na huyo alikuwa ndio mkali zaidi katika kunishambulia mimi. Ninhofia kwamba muuaji wangu atakuwa ameugua ukoma. Halafu nili-omuona Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) pamoja na kundi la masahaba zake akiniambia: ‘Mwanangu! Wewe ni Shahidi mfiadini wa Nyumba yangu. Wakaazi wa Peponi na Mola wa walimwengu wanakusubiri kwa shauku kubwa. Ewe mwanangu! Usiku huu utavunja saumu yako pamoja nami. Usichelewe kuja kwangu! Malaika huyu ametumwa kazi ya kukusanya damu iliyomwaga kutoka kwenye mwili wako na kuiweka kwenye chupa ya kijani.’ Ndoto hii inaashiria kuondoka kwangu kwa hivi punde kuelekea kwenye Makazi ya Milele.””

(*Muthir al-Ahzan*)

MLANGO WA TANO

VIFO VYA KISHAHIDI VYA WAFUASI WA IMAM KUANZA KWA SIKU YA ASHURA

Baada ya swala ya Asubuhi katika ile Siku ya Ashura, Imam (a.s.) na watu wake waliandaa safu zao kwa ajili ya mapambano ya kivita. Kwa jumla kulikuwa na watu thelathini na wawili juu ya farasi na arobaini wanaotembea kwa miguu. Zuheir ibn Qayn alipewa ukamanda wa kuongoza vikosi vya upande wa kulia vya jeshi hilo wakati ambapo Habib ibn Mudhahir aliongoza vile vya kushoto. Bendera ilikabidhiwa kwa Abbas ibn Ali. Imam na Bani Hashim walitwaa nafasi zao katikati ya jeshi hilo.

Kuhusu upande wa maadui, Umar ibn Sa'd alikuwa amemuweka Amr ibn Hajjaj kuwa kiongozi wa vikosi vya upande wa kulia na Shimr ibn Dhi Jawshan kiongozi wa vikosi vya kushoto. Urwah ibn Qays alikuwa kamanda wa askari wa farasi ambapo Shabath ibn Rib'i aliongoza askari wa miguu. Bendera ilikabidhiwa kwa Durayd, mtumishi wa Umar ibn Sa'd.

Kikundi cha maadui waliwasogeza farasi wao karibu na kambi ya Imam (a.s.). Waliona ule mtaro nyuma ya kambi ya Imam na moto ukichoma zile kuni na mabua ya matete yaliyotupwa ndani humo. Hapo Shimr ibn Dhi Jawshan aliita kwa sauti: "Oh, Husein! unaharakisha kukimbilia kwenye moto kabla ya Siku ya Hukumu?" Imam (a.s.) alimrudishia maneno makali: "Ewe mwana wa mbarika! Wewe ndiye unayestahili haswa kuunguza katika moto wa Jahannam!"

Katika wakati huo Muslim ibn Awsajah alikuwa akimlenga mshale Shimr lakini Imam (a.s.) alimkataza kumrushia mshale huo. Muslim ibn Awsajah akaomba: “Niruhusu nimrushie na kumchoma yule. Yeye ni dhalimu mbaya na Mwenyezi Mungu ameruhusu damu yake kumwaga na sisi kuwa ni halali kwetu.” Imam akamjibu: “Nachukia kwamba sisi tuwe ndio waanzilishi wa mapambano.”

Halafu Imam (a.s.) akampanda ngamia wake na akaelekea kwenda kwa maadui na kuzungumza nao. Hii ilikuwa ni hotuba yake ya kwanza katika Siku ya Ashura. Baada ya kumsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu alijitambulisha mwenyewe: “Hamkusikia kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema kwamba al-Hasan na al-Husein ni mabwana wa vijana wa Peponi? Kama mna shaka na hilo, basi waulizeni watu mfano kama Jabir ibn Abdullah al-Ansari, Abu Sa’id al-Khudri, Sahl ibn Sa’d, Zayd ibn Arqam na Anas ibn Malik masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusu ukweli wa kauli hii. Hili halitaweza kuwazuia kumwaga damu yangu?”

Shimr aliguta kwa sauti: “Anamuabudu Mwenyezi Mungu kwenye kingo (yaani kinafiki).” Habib ibn Mudhahir akamkemea Shimr kwa sauti kali: “Bali ni wewe unayemuabudu Allah juu ya kingo sabini (yaani kwa unafiki uliokamilika dhahiri). Nashuhudia kwamba wewe huelewi neno katika yanayosemwa na kwamba moyo wako umefungiwa mbali na ukweli.”

Baada ya kitambo kifupi cha zaidi cha kurushiana maneno, maadui waliamua kuanzisha shambulizi. Wakati Hurr ibn Yazid Riyahi alipotambua kwamba vita vilikuwa karibu vianze, yeye alishitushwa sana na kile ambacho kitakuja kutokea kiasi kwamba alijitoa binafsi kutoka kwenye safu za adui na akajiunga upande wa Imam Husein (a.s.).

Umar ibn Sa'd alimwitisha Durayd kuleta mbele bendera yake. Kisha akaweka mshale kwenye upinde wake na akaurusha kuelekea kwenye safu za Imam Husein (a.s.) akisema: "Shuhudia kwamba mimi nimekuwa wa kwanza kurusha mshale kumwelekea Husein." Mmiminiko wa mishale ulifuatia na vita vikawa vimeanza rasmi. Askari kutoka pande zote waliuliwa katika mashambulizi haya ya kwanza. Katika mashambulizi yaliyofuata iliamuliwa kwamba wafuasi wa Imam (a.s.) watashambulia kwa vikundi vyatya wawili wawili, watatu na wanne hadi idadi yao itakapopungua ndipo watakapopigana mmoja mmoja.

(Kitab al-Irshaad)

IDADI YA WAFUASI WA IMAM AMBAO WALIUAWA

Inakubalika kwa jumla kwamba waliouliwa kishahidi hapo Karbala walikuwa ni sabini na mbili kwa idadi. Hata hivyo, zipo riwaya kwamba kabla ya Shahada ya Imam (a.s.), yeye aliangalia pale mahali ambapo miili ya mashahidi hao ilikuwa imekusanywa na akagundua kwamba wafuasi wake waliokuwa sio Bani Hashim walikuwa ni sabini na wawili ambapo kwa upande wa Bani Hashim walikuwa ni kumi na wanane kwa idadi yao.

(Ma'ali al-Sibtayn)

Al-Marhum Mustawfi anaandika: Baada ya kukagua maelezo ya Ashura, ninashawishika kwamba idadi ya wafuasi wa Imam (a.s.) ilikuwa ni zaidi ya sabini na wawili. Hii idadi ya sabini na mbili inaweza kuwa imepata umaarufu kutokana na watu sabini na wawili walioondoka Madina pamoja na Imam (a.s.)

(Nasikh al-Tawarikh)

Majina sabini na tisa yametajwa katika *al-Ziyarah al-Nahiyyah* iliyosimuliwa na Sayyid ibn Tawus kutoka kwa Imam wa kumi na mbili (a.s.).

Muhaddith Mahalati amehesabu mashahidi mia mbili na ishirini na mbili. Kati ya hawa, mmoja kwa jina la Sulayman ibn Abi Zarin aliuliwa mjini Basra na kumi na wawili huko al-Kufah. Wale walieuawa hapo Kufa ni:

Muslim ibn Aqil na wanawe wawili

Muhammad ibn Kathir na kijana wake

Hani ibn Urwah

Abd al-A'la ibn Yazid

Abbas ibn Ja'dah

Abdullah ibn Harith

Abdullah ibn Afif

Abdullah ibn Yaqtur

Qays ibn Mushir

Hao mia mbili na sabini waliobakia waliuawa hapo Karbala – (*Fursan al-Hayjan*).

Sayyid Muhsin Amin amehesabu mashahidi mia moja na thelathini na tisa. Hawa ni kama ifuatavyo:

Kumi kati ya watoto wa Amirul-Mu'minin (a.s.)

Wanne kati ya watoto wa al-Hasan ibn Ali (a.s.)

Watatu kati ya watoto wa al-Husein ibn Ali (a.s.)

Watatu kati ya watoto Abdullah ibn Ja'far (a.s.)

Tisa kati ya watoto wa Aqil ibn Abu Talib (a.s.)

Abdullah ibn Muhammad al-Hashimi ambaye nasaba yake na Bani Hashim haikuwekwa wazi.

Kwa mujibu ya hii Bani Hashim walikuwa thelathini kwa idadi.

Waliokuwa sio Bani Hashim ambao waliuliwa hapo Karbala ni watu mia moja na sitini ambapo watatu waliuliwa al-Kufah: Hani ibn ‘Urwah, Abdallah ibn Yaqtur na Qays ibn Mushir.

(*A’yan al-Shi’ah*)

HURR BIN YAZID RIYAHİ ANAREJEA KUTO-KA KWENYE JESHI LA UMAR BIN SA'D

Kabla ya kuanza kwa vita wakati wa mawio mnamo Siku ya Ashura, Hurr ibn Yazid alimfuata Umar ibn Sa'd na akamuuliza: “Je, umeamua kumpiga vita al-Husein (a.s.)?” Umar ibn Sa'd akajibu: “Kwa hakika itakuwa ni vita ambamo vichwa vitaruka na mikono itakatwa.” Kwa hili, Hurr alisikia ombi linalosumbua akili la Imam (a.s.) alipokuwa akiita akisema: “Hakuna mtu atakayeku kutusaidia? Hakuna mtu atakayeitetea familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?” Hurr alitetemeka kwa ukelele huo wa Imam na akajitenga na watu. Pamoja naye alikuwa ni Qurrah ibn Qays, mtu anayetoka kwenye kabila lake. Hurr alimuuliza Qurrah kama alimpaa farasi wake maji ya kunywa. Qurrah akajibu kwamba hakuwahi kumpatia maji. Hurr akashauri: “Basi ni kwa nini humpeleki kwenye maji?”

Qurrah anasimulia: “Wakati huo nilifikiria moyoni mwenyewe kwamba Hurr alikuwa anataka kukimbia vita na kwamba hakutaka mimi nilishuhudie hilo. Nilikwenda kumpaa maji farasi wangu na nikamuona Hurr taratibu akielekea kwa al-Husein (a.s.). Muhajir,

afisa mmoja wa jeshi la Umar ibn Sa'd alimpigia kelele akimwambia: “Ewe Hurr! je, unakusudia kumshambulia Husein?” Hurr hakujibu, rangi yake ilikwajuka na akaanza kutetemeka. Muhajir alisema kwa sauti kubwa: “Sijawahi kukuona ukiwa na woga kiasi hicho hapo kabla. Wallahi! kama ingekuwa naulizwa kwamba ni mpiganaji gani jasiri sana wa al-Kufah ningesema ni wewe hapo!” Hurr hapo akamjibu: “Wallahi, najikuta mwenyewe nikiwa kati ya Pepo na Jahannam, na nisingependelea chochote kuliko Pepo hata kama nitakatwa vipande vipande na kisha nikachomwa!” Kisha Hurr akampelea shoti farasi wake kuelekea kwa al-Husein (a.s.) na akajiunga na jeshi dogo la Imam (a.s.).

Wakati Hurr alipomfikia Imam, alisihi akitokwa na machozi mengi: “Uhai wangu uwe kafara kwa ajili ya uhai wako, Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)! Ni mimi niliyekuzuua kurejea kule utokako. Ni mimi niliyekuweka katika ardhi hii mbaya. Sikuweza kuamini kwamba watu hawa wasio na Mungu wangeweza kukataa kukubaliana na pendekezo lako na kwamba wangeweza kufikiria kukuuwa. Ewe Husein! Ninakuja nimeaibika, mwenye kujuta, mwenye kutubia na kuomba msamaha. Je, kuna uwezekano wa kuwepo njia ya kusamehewa kwangu?” Imam (a.s.) akajibu: “Ndio, Mwenyezi Mungu ameikubali toba yako. Ewe Hurr! Shuka kwenye farasi wako na usogee hapa kwangu.” Hurr akasema: “Ni bora nibakie juu ya kipando na nipigane na adui nikiwa juu ya mgongo wa farasi.” Kisha Hurr akaja kwenye uwanja wa mapambano na akasimama akiwaangalia maadui akiwalaumu na kusema: “Mwenyezi Mungu asizizime kiu zenu mnamo Siku ya Kiyama kwa sababu ya namna mlivyofanya kwa familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).” Maadui walirusha kiasi cha mishale kwa Hurr lakini ye ye alirejea kwa Imam (a.s.) na akasubiri maelekezo kutoka kwake.

(Kitab al-Irshaad)

Inasimuliwa kwamba baada ya Hurr kuomba msamaha kutoka kwa Imam (a.s.), aliomba ruhusa ya kwenda kwenye mahema ya wanawake ili kwenda kuomba radhi kutoka kwao. Imam (a.s.) alimpatisi ruhusa hiyo. Hivyo Hurr kwa moyo uliovunjika na macho yaliyojaa machozi alikwenda akiwa juu ya farasi wake hadi nje ya mahema ya akina mama. Aliita kwa sauti: “Amani iwe juu yenu, enyi kizazi cha Mtume! Mimi ndiye yule mtu aliyeingilia kati kwenye njia yenu. Mimi ndiye niliyewasababishia huzuni na kuwaleta ninyi kwenye hali hii mbaya. Nimekuja kama mwenye kutubia, nikitafuta kimbilio kwa al-Husein (a.s.). Nina matumaini kwamba hamtalalamika juu yangu mbele ya Bibi Fatimah (a.s.).”

Huo ndio uliokuwa uzito wa athari ya kuomba radhi kwa Hurr kwamba vilio na mayowe ya wanawake yalisikika kutoka kwenye mahema yao. Inasimuliwa kwamba Hurr aliguswa sana na hili kiasi kwamba alishuka kwenye farasi wake na akalia kwa sauti kubwa mno akijipiga usoni mwake kwa mkono wake kwa huzuni. Yeye alilalamika: “Kama ingekuwa tu mikono na miguu yangu ingepooza ili kwamba nisiweze kufanya hayo niliyofanya! Ingekuwa tu ulimi wangu ungekuwa umekatwa ili iwe nisingeweza kusema niliyoyasema! Kama nisingewazuia tu kurejea majumbani kwenu! Kufikia hapa baadhi ya wanawake walimliwaza Hurr na kumuombea. Hili lilimpa faraja kiasi fulani.

(Masa'il al-Abرار)

SHAHADA ZA NDUGU NA WATOTO WAWILI WA HURR BIN YAZID RIYAHİ

Baada ya Hurr kujiunga na Imam al-Husein (a.s.), alifuatwa na mwanawe Ali na kaka yake Mushab. Mushab alikuwa amewatelekeza maadui na kujiunga na Imam (a.s.) baada kusikia hotuba ya Hurr kwa maadui. Hurr aliwachukua wote, mwanawe na kaka yake kwenda kwa Imam (a.s.). Wote walitubia mikononi mwa Imam (a.s.) na wakaingia kwenye mapambano ya vita na wote waliuliwa humo.

(Nawasikh al-Tawarikh)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Hurr alikuwa na mtoto mwingine wa kiume aliyeitwa Bukayr. Yeye pia alimfuata Hurr na akajiunga na Imam al-Husein (a.s.). Kabla ya kuwenda kwenye uwanja wa vita, Bukayr alikwenda kwa Imam (a.s.) na akambusu mikono na miguu yake. Kisha akamuaga. Bukayr alipokaribia safu za maadui, Hurr alimwita na kumuamuru: “Ewe mwanangu! Msaidie yule ambaye ametutoa kutoka kwa madhalimu waovu (akimaanisha Husein). Bukayr alipigana na maadui kwa nguvu sana. Baada ya kuwauwa wengi wao, alirudi kwa baba yake akisema: “Ewe baba! Kuna njia yoyote ya mimi kuweza kupata kunywa maji?” Hurr akajibu: “Oh mwanangu! rejea kwenye mapambano na uvumilie kwa kitambo kidogo zaidi.” Bukayr akarejea kwenye mapambano na akauawa. Wakati Hurr alipowasili kwenye mwili uliochanwa wa mwanawe, yeye aliomba, “Sifa zote kwa Allah swt. Ambaye amekujaalia shahada juu yako mbele ya mtoto wa binti ya Mtukufu Mtume wa Allah (s.a.w.w.).”

SHAHADA YA HURR IBN YAZID RIYAHİ

Miongoni mwa mambo ambayo Hurr alimwambia Imam (a.s.) ni haya yafuatayo: “Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mimi nilikuwa mtu wa kwanza kukuilingilia kati kwenye safari yako. Sasa nataka niwe wa kwanza kwenda vitani dhidi ya adui yako ili niweze kuja kupokea uombezi wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) mnamo Siku ya Hukumu.” Imam alimruhusu Hurr kufanya hivyo. Wakati Hurr alipokuwa akielekea kwenye uwanja wa mapambano, alisoma beti zifuatazo:

“Mimi ni Hurr, ambaye nyumba yake ni kimbilio la wageni na yenye sifa ya juu ya ukarimu

“Hawa (yaani Husein na familia yake) ni wageni wapendwa kabisa wa Allah mionganoni mwa wale walioko Makka na Mina

“Sitauzuia upanga wangu kwa yoyote katika kuwatetea hawa viumbe wapendwa wa Mwenyezi Mungu.

“Mimi ndiye Hurr, ambaye nimekulia kwenye Nyumba ya uhuru (hurr) na nimerithi ujasiri na uhuru kutoka kwa wahenga wangu.”

Hurr alishambulia kwa ukali sana na akauwa maadui wengi mno hadi farasi wake akalemazwa. Alishuka na akaendelea kupigana kwa miguu. Baada ya kuua takriban maadui arobaini, ye ye alishambuliwa na idadi kubwa ya maadui. Hurr akaanguka chini. Masahaba wa Imam Husein (a.s.) walibeba mwili wa Hurr kuupeleka kwa Imam (a.s.) kukiwa kumebakia chembe kidogo ya uhai ndani yake. Imam (a.s.) aliisafisha damu kutoka kwenye uso wa Hurr na akasema:

“Wewe ni mtu huru kama mama yako alivyokuita jina hilo. Wewe ni mtu huru katika dunia hii na ile ijayo ya Akhera.”

(*Nawasikh al-Tawarikh*)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Imam (a.s.) alitamka maneno haya wakati akiwa anakimbia kwenda kwenye uwanja wa vita kwenye mwili wa Hurr pale alipoanguka chini.

(*al-Amali cha al-Sheikh Saduq*)

Imam Ali ibn al-Husein (a.s.) amesimulia kwamba sahaba mmoja wa Imam Husein (a.s.) aliomboleza kifo cha Hurr kwa kusoma beti hizi:

“Mtu huru aliye bora kabisa ni Hurr kutoka kabilia la Riyah madhubuti katikati ya mikuki inayoshambulia.

“Yeye ndiye mtu huru bora kwani aliutoa uhai wake kwa ajili ya al-Husein na aliyefanikiwa kwa muongozo na wokovu

“Yeye ndiye mbora katika watu huru katika kujibu mwito wa al-Husein, na kutoa muhanga uhai wake ndani ya medani ya mapambano.

“Ewe Mola! Mpokee katika viwanja Vyako vyta Peponi na umfungie ndoa na wanamwali warembo wa Pepo Yako.”

Imesimuliwa vilevile kwamba Imam (a.s.) alifunga hanjifu yake juu ya paji la uso la Hurr ili kuzuia uvujaji wa damu kutoka kwenye majeraha makubwa na mabaya aliyokuwa ameyapata katika mapambano hayo. Hurr alizikwa baadaye na hanjifu hiyo ikiwa imefungwa juu ya uso wake.

(*Ma’ali al-Sibtayn*)

MANENO YA IMAM ALI IBN HUSEIN JUU YA MWILI WA HURR

Mnamo mwezi 13 Muharram Imam Ali ibn al-Husein alitokeza kimuujiza kwenye uwanja wa mapambano ili kuizika miili ya wafiadini hao kwa msaada wa Bani Asad. Alichukua kikundi cha Bani Asad kwenda kwenye mwili wa Hurr. Akiuangalia mwili huo alisema: “Na kuhusu wewe, Mwenyezi Mungu ameikubali toba yako na ameiongeza furaha yako kuitia muhanga wako kwa ajili ya mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).” Kisha kwa msaada wa Bani Asad akauzika mwili wake.

(Maqtal al-Husein)

Imesimuliwa pia kwamba watu wa ukoo wake waliondoa mwili wa Hurr kutoka kwenye uwanja wa vita ili kuuzuia kutokana na kukanyagwa kanyagwa na kwato za farasi. Hurr alikuwa na mtumishi aliyeitwa Qurrah. Baada ya kuuliwa kishahidi kwa Hurr, Qurrah alikuja kwa Imam (a.s.) na akatubia. Halafu akapigana dhidi ya maadui hadi alipouliwa kishahidi.

(Nawasikh al-Tawarikh)

UINGILIAJI KATI WA MAPEMA WA ABBAS IBN ALI KATIKA MAPAMBANO

Abbas ibn Ali alikuwa auawe baadaye katika Siku ya Ashura na hili litaelezewa baadaye. Mapema siku hiyo yeye alikuwa akifanya doria kwenye mahema ili kuwazuia maadui kuwashambulia. Wakati huu Zuheir ibn Qayn alimwendea Abbas na akasema: “Nimekuja hapa wakati huu ili kukukumbusha juu ya wosia wa baba yako kwako.” Abbas ambaye alihofia hatari kutokeza punde tu hakushuka kwenye kipando chake. Yeye alisema: “Huu sio wakati wa mazungumzo.

Lakini kwa vile umetaja jina la baba yangu, mimi siwezi kukataa. Wewe zungumza na mimi nitakusikiliza nikiwa juu ya farasi wangu.” Zuheir akajibu: “Wakati baba yako aliponua kumuoa mama yako, alimwambia ndugu yake Aqil amtafutie mwanamke jasiri kutoka kwenye familia jasiri atakayemzalia mtoto shujaa ambaye atakuja kumlinda al-Husein (a.s.). Oh, Abbas! Baba yako alikutafuta wewe kwa ajili ya siku kama ya leo hii. Tafadhalii usirudi nyuma katika ulinzi wako kwa Husein (a.s.).”

Hisia ya hadhi ya Abbas ilihalifiwa kwa hili. Akasukuma kwa nguvu mguu wake kwenye vikuku vya farasi akivivunja na kujibu kwa hasira: “Oh Zuheir! Unataka kunichochea mimi kwa mazungumzo yako haya? Wallahi sitamtelekeza ndugu yangu kamwe au kuzembea katika kuilinda familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Nitakuonyesha wewe kitu ambacho hujawahi kukiona hapo kabla kamwe.”

Kisha alianzisha shambulizi dhidi ya maadui akiwauwa kwa idadi kubwa. Miongoni mwa maadui aliyepambana naye katika pambano la mmoja mmoja alikuwa ni mpiganaji hodari kwa upanga aliyeitwa Marid ibn Sudayf Taghlabi. Abbas alivuta mkuki kutoka mikononi mwa Marid. Alipokuwa anakaribia kumshambulia Marid, aliguta kwa ghafla: “Oh Marid ninajihakikishia kwamba nitakusukumia kwenye mashimo ya Jahannam kwa mkuki wako mwenyewe.”

Halafu Abbas akauchoma mkuki kwenye farasi wa Marid na kumfanya aanguke chini. Marid akaruka chini ardhini. Kwa wakati huo huo kikundi cha maadui kilikimbilia kuja kumnusuru yeye. Hata walivyokuwa wakimshambulia Abbas, yeye Abbas alifanikiwa kuutosa mkuki kwenye shingo ya Marid na kukata kichwa chake kuanzia eneo la masikioni ambapo wakati huo huo akikwepa mashambulizi ya wafuasi wa Marid.

(Kibrit al-Ahmaar)

MAELEZO JUU YA SHAHADA YA MUSLIM IBN AWSAJAH

Kabla ya kuingia kwenye mapambano, kila mmoja kati ya wafiasi wa Imam alikuwa akija kwa Imam (a.s.) kuagana naye. Kila mmoja alisema: “Amani iwe juu yako, ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).” Imam (a.s.) alikuwa akijibu: “Amani iwe juu yako nawe pia! Hakika sisi karibuni tutakufuata.” Vilevile alikuwa akisoma ayah ifuatayo: **“Miongoni mwa waumini wapo wanaume waliotimiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea; wala hawakubadilisha ahadi yao hata kidogo.”** (33:23). Imam vilevile aliwasomea aya hii kwenye miili ya wafiasi wake walipokuwa wakimwita kabla hawajaaga dunia.

Muslim ibn Awsajah alikuwa na umri sawa na ule wa Imam (a.s.) na alikuwa anatokana na kabilia la Bani Asad, kabilia lile lile la Habib ibn Mudhahir. Yeye alitoroka kwa siri kutoka al-Kufah pamoja na Habib ibn Mudhahir na akajiunga na Imam (a.s.).

Sasa Muslim ibn Awsajah alikwenda kwa Imam na akamuaga, kisha akaingia uwanjani. Baada ya pambano la kishujaa Muslim aliangushwa chini na kundi la maadui. Vile alivyokuwa akianguka chini alimwita Imam (a.s.). Imam pamoja na Habib ibn Mudhahir walimkimbilia. Wakati kukiwa kuna uhai kiasi uliokuwa umberakia kwa Muslim, Imam (a.s.) aliketi karibu yake na akasema: “Mwenyezi Mungu akurehemu, ewe Muslim!” Kisha akasoma: **“Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea; wala hawakubadilisha ahadi yao hata kidogo.”**

Habib alichuchumaa karibu na ule mwili wa Muslim uliokuwa umelowa damu na akasema: “Haistahimiliki kwangu mimi

kuuangalia mwili wako uliotapakaa damu. Pokea bishara njema ya Peponi.” Kwa sauti dhaifu Muslim akajibu: “Mwenyezi Mungu akujaalie Pepo na wewe pia.” Kwa huzuni sana Habib akamwambia Muslim: “Ningekuwa sitambui kwamba hivi karibuni nitakufuata, ningependa nisikie matakwa na wasia wako wa mwisho. Akinyooshea kidole chake kuelekea kwa Imam, Muslim alijibu: “Natoa usia wangu kwamba umlinde bwana huyu.” Habib akasema: “Naapa kwa Mola wa al-Kaaba! mimi nitafanya hivyo.” Wakati huu Muslim ibn Awsajah akavuta pumzi za mwisho na akakata roho. Alikuwa na mtumishi wa kike ambaye alimuombolezea kifo chake akiguta kwa sauti: “Oh, Muslim! Oh, Bwana mkubwa wangu! Ewe mwana wa Awsajah!”

Wafuasi wa Amr ibn Hajjaj kwa shangwe wakatangaza kwamba wamemuua Muslim Ibn Awsajah. Shabath ibn Rib'i, afisa mmoja wa jeshi la Umar ibn Sa'd akawakemea akisema: “Mnasherehekeea kumuua mtu kama huyo!” Alikuwa ni mtu mashuhuri kiasi gani! Mimi nilimuona huko Azerbaijan kabla ya kuwasili kwa majeshi ya Waislam. Aliwauwa watu sita kati ya washirikina wale!”

(At-Tariikh Tabari)

SHAHADA YA HABIB IBN MUDHAHIR

Mnamo ile Siku ya Ashura wakati vita vilipokuwa vinapiganwa vi-kali katika kile kikundi kidogo chenye kiu cha wafuasi wa Imam al-Husein (a.s.) na lile jeshi kubwa lenye maguvu la Ibn Sa'd, bwana Abu Thumamah Amr ibn Abd-Allah Saydawi, mfuasi mwaminifu wa Imam (a.s.) aliona kwamba ulikuwa ni muda wa swala ya mchana. Alikuja kwa Imam (A.s.) na akasema: “Ingawa ninajua kwamba maadui hawataturuhusu muda wa kuswali na ingawa naapia kwa jina la Allah kwamba mimi sitaacha wewe uuliwe kabla yangu mimi,

bado ninatamani kukutana na Allah nikiwa nimekwisha kuiswali swala hii pamoja na wewe.” Imam aliyebarikiwa alitazama juu angani na akasema. “Mwenyezi Mungu akufufue pamoja na wale ambao wamesimamisha swala! Na maadui watuachie sisi muda wa kuswali.”

Habib ibn Mudhahir aliwasilisha ujumbe wa Imam (a.s.) kwa maadui. Ambapo Husein ibn Numayr, mmoja wa makamanda wa jeshi la Umar ibn Sa'd aliguta: “Oh, Husein! swali swala nyingi kiasi utakavyo. Hizo hazitakubaliwa! Habib akamkemea, “Ewe kiumbe uliye fidhuli mbaya mno kuliko viumbe wote! Hivi swala zako wewe zitakubaliwa ikiwa swala za mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) hazitatakabaliwa?” Husayn ibn Numayr kwa kughadhibishwa na kauli ya Habib akaanzisha shambulizi dhidi yake akimlazimisha Habib kuingia kwenye pambano. Habib ibn Mudhahir alipigana vita vikali na hatimae akauliwa. Kwa mujibu wa hili, Habib alipata Shahad kabla ya kuswali swala ya mchana.

(*Fursan al-Hayjan*)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, kabla ya kuaga dunia kwake, Habib ibn Mudhahir alikuja kwa Imam (a.s.) na akasema: “Ewe Bwana mkubwa, naapa Wallahi kwamba napendelea kutekeleza swala yangu huko Peponi na kuwasilisha salamu zako kwa babu yako, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), kwa baba yako Ali na ndugu yako al-Hasan, amani juu yao wote.” Halafu Habib akaingia kwenye mapambano huku akiwa anasoma beti zifuatazo:

“Naapa tungekuwa sawa nanyi kwa idadi au japo nusu yenu, mngegeuzia migongo yenu kwetu katika kukimbia.

“Oh, enyi waovu wabaya kabisa kati ya viumbe kwa nasaba na matendo, mmekuwa na tabia ya kidhalimu kabisa!

Habib alipigana vita vyatia kijasiri akiwauwa takriban watu sitini

na wawili mpaka mmoja kati ya askari waliokuwa wamemzunguka akampiga Habib kichwani kwake kwa upanga wake wakati mwiningine alipokita mkuki wake kwenye kifua cha Habib. Habib ibn Mud-hahir, akiwa hawezi kubakia kwenye kipando chake alianguka chini. Alipojaribu kusimama, Husayn ibn Numayr kwa mara nyingine tena akampiga kichwani kwa upanga wake. Kwa hili, huyu mfuasi wa maisha wa Imam Husein (a.s.) aliachana naye.

Kifo cha Habib kilisababisha huzuni kubwa sana, masikitiko na dhiki kwenye uso wa Imam mpendwa kwa namna ambayo hajjawahi kuonekana kabla katika siku ile. Imam (a.s.) alikwenda kwenye mwili uliochanwa chanwa wa Habib na akakiweka kichwa cha Habib kwenye mapaja yake. Akitiririkwa na machozi mengi, ye ye akasema: “Ni jinsi gani ulivyokuwa mtu bora wewe. O Habib! Hakika wewe ulikuwa ukiweza kuisoma Qur’ani yote kwa usiku mmoja.”

(*Maqtal al-Husayn* cha Abu Mikhraf)

SWALA YA MWISHO YA IMAM (A.S.)

Kulingana na riwaya nyingine wakati wa mchana wa Siku ya Ashura, Abu Thumamah Saydawi, alipotambua kwamba jua lilikuwa limesogea hadi kupita anga ya juu yao, alikwenda kwa Imam (a.s.) na akasema: “Kabla sijautoa uhai wangu kwa ajili yako, mimi natamani kuswali swala ya mchana pamoja na wewe.”

Imam (a.s.) akanyanya kichwa chake na kutazama juu angani na akasema: “Mwenyezi Mungu akufufue pamoja na wale waliokuwa wakidumisha swala kwa kunikumbusha kwako. Nenda kule kwa maadui na uwaombe watupatie mwanya wa muda kwa ajili ya swala.”

Maadui walipoambiwa wasimamishe mapigano kwa ajili ya Imam (a.s.) kuswali swala yake ya mchana, Husayn ibn Numayr aliguta: “Swalini mara nyingi kiasi mpendavyo, swala zenu hazitatakabaliwa!”

Hapo Habib ibn Mudhahir akamkemea, “Ewe mlevi mkubwa, je zitakubaliwa swala zenu ninyi na zisitakabaliwe za mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?”

Imam (a.s.) pamoja na kikundi cha wafuasi wake waaminifu kabisa waliswali swala yao ya mchana kwa hofu (*Salat al-khauf*) ambapo Zuheir ibn Qayn na Sa’id ibn Abd-Allah wakasimama mbele ya Imam (a.s.) wakitumia vifua vyao kama ngao katika kuikinga mishale iliyokusudiwa kwa Imam (a.s.).

Idadi ya mishale ambayo ilimdunga Sa’id ilimsababishia kuanguka chini ardhini. Alimgeukia Imam na kusema: “Je nimekuwa mwaminifu kwenye dhima yangu kwako?”

Imam (a.s.) akamjibu: “Ndio, wewe utanitangulia kuingia Peponi.”

Sa’id akavuta pumzi zake za mwisho na akaondoka kwenda kwenye mabustani ya milele. Kulikuwa ni mishale kumi na tatu kwenye mwili wake.

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

SHAHADA YA ZUHEIR IBN QAYN

Kuanzia ule muda ambapo alijiunga na Imam (a.s.) uaminifu na wajibu wake kwa Imam (a.s.) umetajwa katika matukio mengi. Im-ekwisha kutajwa kwamba katika mkesha wa Ashura alipoulizwa kuhusu wajibu wake, Zuheir alijibu kwa maneno kama haya: “Ewe

bwana mkubwa! Kama ingekuwa niuawe na kuchanwa vipande
vipande mara elfu moja na kisha nikarudishiwa uhai tena, mimi nis-
ingeweza kukutelekeza wewe.”

Sasa, katika Siku ya Ashura yenye, Zuheir alikuja kwa Imam (a.s.), akaweka mkono wake kwenye bega la Imam na akaomba ruhusa ya kwenda kwenye mapambano. Baada ya Imam (a.s.) kumpa ruhusa, Zuheir aliingia kwenye uwanja wa vita kama simba aliye na hasira kali. Alijitangaza mwenyewe kwa beti zifuatazo:

“Mimi ni Zuheir nami ni mwana wa Qayn

Nitakufukuzilieni mbali kutoka kwenye familia ya al-Husein
kwa upanga wangu!

Yeye aliwa watu mia moja na ishirini kutoka kwenye kundi la maadui. Watu wawili wajeshi la adui wakati huo huo wakamshambulia kwa pamoja na wakamuwa. Wakati alipoanguka chini, Imam (a.s.) alimkimbilia. Alimuangalia na akasema: “Oh, Zuheir! Mwenyezi Mungu atenge sehemu kwa ajili yako karibu na Yeye Mwenyewe na awalaani wauaji wako.”

(*At-Tariikh ya Tabari*)

SHAHADA YA ANAS IBN HARITH KAHILI

Kama ilivyotajwa hapo kabla, mmoja wa watu kutoka kwenye kabila lake ambalo Habib ibn Mudhahir aliwasihii kujiunga na Imam Husein (a.s.) alikuwa ni Anas ibn Harith Kahili. Anas ibn Harith alikuwa ni mmoja wa masahaba wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na alishiriki katika vita vya Badr na Hunayn. Hapo Karbala yeye alikuwa ni mzee sana kiasi kwamba kope za macho yake zilikuwa nyeupe na zilikuwa zikiangukia kwenye macho yake kwa urefu.

Anas alikwenda kwa Imam (a.s.) katika Siku ya Ashura na akaomba ruhusa ya kupigana dhidi ya maadui. Kisha Anas akafunga kilemba chake kwenye kiuno chake ili kukinyoosha na akafunga leso kwenye paji la uso wake ili kunyanya zile kope zake. Vile Anas alivyokuwa akijiandaa kwa vita, alisoma beti za mapenzi na utii kwa Imam (a.s.). Imam (a.s.) alipomsikia Anas na kuiona shauku yake, yeye aliguswa sana kiasi alianza kulia. Imam (a.s.) alimuomba Mwenyezi Mungu huku machozi yakimtiririka kwenye mashavu yake akisema: “Mwenyezi Mungu azikubali jitihada zako, ewe mwenye makamu ya uzee!”

Anas alipigana kijasiri na licha ya umri wake wa uzee alimudu kuuwa watu kumi na nane mionganini mwa maadui. Mwishowe kutokana na majeraha yasiyokuwa na idadi mwili mwake, udhaifu, uzee na kiu Anas alizidiwa nguvu na maadui na akauliwa shahidi.

SHAHADA YA JUNADAH IBN HARITH ANSARI NA MWANAWE UMAR

Junadah ibn Harith Ansari alikuwa ni mkazi wa Madina. Alikuwa amefuatana na Imam (a.s.) kuanzia Hijaz. Baada ya kupata ruhusa kutoka kwa Imam, yeye aliingia kwenye mapambano huku akisoma beti hizi:

“Mimi ni Junadah na ni mwana wa Harith.

Na mimi sio mmoja wa wale wenye woga

Au wale wanaovunja viapo vyao vya utii.

Alipigana na maadui hao mpaka akauliwa. Junadah alikuwa amekuja Karbala pamoja na mwanawе Umar ambaye alikuwa na umri wa miaka ishirini na moja na mke wake, mama wa mwanawе

huyo Umar. Baada ya kuuliwa kwa Junadah mkewe akamtuma mwana wao Umar kwenye mapambano. Wakati Imam alipomuona Umar akiingia kwenye mapambano yeye alimwita arejee akihofia mama yake asije akakosa mlezi. Umar alimsihi Imam (a.s.) na akaeleza kwamba ni mama yake aliyemtuma kuingia vitani na kumwambia kwamba aihami nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Halafu Umar akaingia tena kwenye uwanja wa vita akighani:

“Bwana wangu mimi ni al-Husein (a.s.) naye ndiye aliye mbora wa mabwana

Furaha ya moyo wangu, na mtoaji wa habari njema na munonyaji.

“Ali na Fatimah (a.s.) ndio wazazi wake yeye.
Je, unamjua ye yote yule ambaye ni mwenye kulingana naye?

Umar alipigana hadi akauliwa. Adui alimkata kichwa chake kutoka mwilini mwake na wakakirusha kuelekea kwenye jeshi la Imam (a.s.). Mama yake Umar alikichukua kichwa cha mwanawе na akaomboleza: “Hongera mwanangu! Ewe furaha ya moyo wangu!
Ewe tunda la jicho langu!” Kisha akakirusha kichwa cha mwanawе huyo kuelekea kwenye jeshi la maadui na halafu akijipa silaha ya nguzo ya hema alikimbia kuelekea kwa maadui huku akiguta:

“Mimi ni mwanamke niliyesogea katika umri,

dhaifu na niliyeteketea, niliyechakaa na kuvunjika moyo.

“Nitakupigeni kipigo kikubwa katika njia ya Fatimah
Mtakatifu.

Yeye aliwahi kuuwa watu wawili kabla ya Imam (a.s.) kumfanya arudi kwenye mahema.

(*Maqtal al-Husein*)

SHAHADA YA WAHB NA MKE WAKE HANIYAH ALIYEMUOA KARIBUNI

Kama ilivyotajwa hapo kabla, Wahb, mama yake Qamar na mke wake Haniyah walikuwa ni watu watatu waliokuwa wanaishi kwenye jangwa la Tha'labiyyah. Walijiunga na Imam (a.s.) hapo Karbala na wakaukubali Uislam mbele yake Imam (a.s.). Mnamo ile Siku ya Ashura, Qamar alikwenda kwa Wahb mwanae na kusema, “Ewe mwanangu! Simama na utoe uhai wako kwa ajili ya mwana wa Fatimah binti ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wewe hutapata baraka zangu wala uombezi wa Mtukufu Mtume bila ya kutoa muhanga uhai wako kwa ajili ya al-Husein (a.s.).” Wahb alijibu akasema: “Ewe mama! Hakika mimi nitafanya hivyo na wala sitamuangusha Imam (a.s.).” Kwa hilo, Qamar alitokwa na machozi ya furaha akimtia chonjo mwanae kupigana kana kwamba anamwachia ndege kutoka tunduni na kuwa huru.

Kutokana na hofu ya umasikini na pia kwa sababu ya ndoa yake ya hivi karibuni na Wahb, Haniyah hakukubaliana na uamuzi wa mumewe kuingia vitani na maadui wa Imam (a.s.). Kwa upande mwingine, Qamar alisisitiza kwamba ye ye aende kwenye medani ya vita bila kuchelewa. Mwishowe Haniyah alimuomba Wahb ampeleke kwa Imam (a.s.).

Haniyah alifikishwa mbele ya Imam (a.s.). Yeye akamwambia Imam (a.s.): “Mimi nina maombi mawili ya kukutolea wewe. Kwanza ni kwamba wakati Wahb atakapokuwa ameuliwa na mimi kuachwa bila mlezi, nakuomba uniweke pamoja na watu wa familia yako tukufu. La pili ni kwamba wakati Wahb atakapouliwa na kufufuliwa pamoja na wanamwali wa Peponi, yeye asije akanisahau na mimi.” Maneno ya Haniyah yakamgusa sana Imam (a.s.) kiasi kwamba machozi yalitiririka kutoka machoni mwake.

Alimliwaza Haniyah na akampa ahadi yake kwamba maombi yake yatakekelezwa.

Wahb kwa ushupavu na bila hofu aliingia kwenye mapambano akighani shairi la kivita. Alipigana kishujaa na baada ya kuuwa idadi kadhaa ya maadui, alirejea kwa mama yake. Alimuuliza mama yake: “Ewe mama! je, umeniridhia mwanaao mimi? Yeye akajibu: “Oh, mwanangu! mimi sintoridhika mpaka uuliwe katika njia ya Husein (a.s.).” Alirejea kwa mara nyingine tena kwenye medani ya vita na akauwa wapanda farasi kumi na tisa na askari wa miguu ishirini. Kisha Wahb akashambuliwa kutoka pande zote. Mikono yake yote ilijeruhiwa vibaya sana kiasi ilikaribia kukatika kabisa. Wakati Wahb alipodondoka kutoka kwenye kipando chake, Haniyah, akiwa na nguzo ya hema mkononi mwake alikimbilia kandoni mwa mume wake. Aliguta, “Baba na mama yangu wawe kafara kwa ajili yako wewe! Pigana na maadui!” Wahb alijaribu kukamata nguo ya mke wake Haniyah na kumrudisha kwenye mahema. Imam (a.s.) aliliona hili na akamwambia Haniyah: “Mwenyezi Mungu akutunuku wewe na malipo yaliyo bora kabisa kwa niaba yetu! Rejea kwenye mahema tafadhali.” Haniyah akarejea mahemani.

Wahb akarejea tena kwenye mapambano. Alikamatwa na maadui na akafikishwa kwa Umar ibn Sa'd. Wahb akiwa mikono yake imekatwa kutoka mwilini mwake alisimama mbele ya Umar. Yeye Umar akapongeza umadhubuti wake kwenye vita. Halafu akawaamuru askari wake wamkate kichwa chake na wakitupe kuelekea kwenye jeshi la Imam Husein (a.s.). Mama yake Wahb akakichukua kichwa chake kilichokatwa na kukiweka mapajani mwake na akasafisha damu iliyokitapakaa na akasema: “Sifa zote ni kwa Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia heshima mimi kwa kufa kwako Shahidi.” Halafu akakikamata kichwa hicho na akakirusha kuelekea kwenye jeshi la maadui kana kwamba kusema

chochote kilichotolewa katika njia ya Imam Husein hakirudiwi tena. Akachukua nguzo ya hema mkononi mwake na akashambulia jeshi la maadui na kuuwa wapiganaji wawili. Imam (a.s.) aliliona hili na akamwita kwa sauti: “Ewe mama yake Wahb! Rejea kwenye hema. Mwanao sasa yupo pamoja na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)!” Alipoyasikia hayo, Qamar akarejea kule kwenye mahema yao.

Wakati huo huo Haniyah alipouona ule mwili wa Wahb usio na kichwa uliolowana damu akaukimbilia. Akaukumbatia mikononi mwake na akasema, “Pokea habari njema za Peponi.” Wakati Haniyah alipokuwa anapiga mayowe katika kuomboleza juu ya mwili wa Wahb, Shimr Dhi Jawshan, mmoja wa makamanda wakatili wa jeshi la adui alimuamuru mtumishi wake aliyeitwa Rustam amuue Haniyah. Rustam akampiga Haniyah kichwani kwa mkuki wake na akamuuwa.

Haniyah alikuwa ndiye mwanamke wa kwanza na wa pekee kuuliwa akimtetea Imam Husein (a.s.) mnamo ile Siku ya Ashura. Wakati wa Shahada yake, Wahb alikuwa ana siku kumi tangu kusilimu na alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano tu. Majeraha sabini yaliingizwa kwenye mwili wa Wahb uliokatwakatwa kwa panga, mikuki na mishale.

(Ma’ali al-Sibtayn)

SHAHADA YA JUWAYN

Juwain alikuwa ni mtumwa wa Abu Dharr aliyeachwa huru am-baye alibakia kuwa thabiti kama alivyokuwa Abu Dharr katika ku-wahudumia watu wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Al-imhudumia Imam Ali (a.s.) kisha Imam al-Hasan (a.s.) na baadaye al-Imam al-Husein (a.s.). Juwayn alifuatana na Imam (a.s.) hadi Karbala na akabakia naye hapo.

Mnamo siku ya Ashura yeye alikuja kwa Imam (a.s.) na kuomba ruhusa ya kwenda kupigana dhidi ya maadui. Imam akamwambia: “Wewe uko huru, okoa maisha yako na kwenda kokote unakopenda.” Macho ya Juwayn yakajawa na machozi alipoanguka miguuni kwa Imam (a.s.). Akaomba na kusihii: “Bwana! Hivi mimi niwe mfuasi wako wakati wako wa utulivu kisha niye kukutelekeze wakati wa matatizo?” Na kisha akaendelea kwa kusema: “Je, ni rangi yangu au harufu yangu au ni kwamba nasaba yangu sio ya Kiarabu? Hapana, Wallahi mimi sitakuacha hadi damu yangu ije kuchanganyika na ya kwako.”

Imam al-Husein, huku akitokwa na machozi alimruhusu kwenda vitani. Alipoingia kwenye uwanja wa mapambano alivua deraya yake na kisha akachana sehemu ya juu ya nguo zake na kuwashangaza maadui. Walimpigia makelele wakisema: “Ewe mtu wewe! Umepotelewa na akili?” Yeye akajibu: “Wallahi, mahaba kwa ajili ya Husein yamenifanya nisikumbuke kitu kingine chochote kile.” Halafu akawapa changamoto ya kuja kumchukua na panga zao.

Juwayn alipigana kama mtumiaji upanga bingwa na akawauwa askari ishirini na tano wa maadui kabla ya kuuliwa kishahidi. Imam (a.s.) alikimbilia kwenye mwili uliokatwakatwa wa mfuasi wake mwaminifu na kumuombea: “Ewe Allah! Ung’arishe uso wake. Fanya harufu yake iwe ya manukato mazuri. Umfufue pamoja na viumbe wako bora na umzoeshe na kizazi cha Muhammad (s.a.w.w.).” Du’a hii ya Imam (a.s.) ilijibiwa mara moja na manukato mazuri yakaanza kunukia kutoka kwenye mwili wa Juwayn uliotapakaa damu.

(Maqtal al-Awalim)

Imam Muhammad al-Baqir (a.s.) anasimulia kutoka kwa baba yake Imam Ali ibn Husein: “Mbali na mwili wa Juwayn, miili yote ya mashahidi ilizikwa na Banu Asad. Huo uligunduliwa siku kumi

baada ya kuzikwa kwa hiyo miili mingine na ulikuwa na manukato mazuri sana yanayotoka kwenye mwili huo. Radhi za Mwenyezi Mungu na ziwe pamoja naye!”

(*Biharul-Anwar*)

SHAHADA YA HAJJAJ IBN MASRUQ

Hajjaj ibn Masruq alikuwa ndiye Muadhini wa Imam Husein (a.s.). Yeye aliingia kwenye mapambano baada ya Unays. Baada ya kupigana kwa kitambo kidogo, alirudi kwa Imam na kughani:

“Leo hii nitakutana na babu yako, Mtukufu Mtume,
halafu na baba yako yule mkarimu

“Yule tunayemtambua kama mwandamizi, mrithi wa Mtume.

Hajjaj alirejea kwenye uwanja wa mapambano na akapigana kishujaa hadi akaauawa kishahidi.

SHAHADA YA HAFHAF IBN MUHAMMAD

Hafhaf ibn Muhammad alikuwa miongoni mwa wapiganaji mashuhuri na wafuasi madhubuti wa Shi'ah wa Basrah. Alikuwa ni mfuasi mwaminifu wa Imam Ali (a.s.) na alishiriki katika vita viliyopiganwa wakati wa Imam wa kwanza. Katika vita vyta Siffin Imam (a.s.) alimfanya Hafhaf kuwa mshika bendera wa Azd, kabila ambalo liliishi Basrah. Alimtumikia Imam wa kwanza na kisha Imam Hasan (a.s.) na baada ya kuuliwa kwa Imam al-Hasan, yeye akajiunga na Imam Husein (a.s.).

Hafhaf aliishi Basrah. Aliposikia habari za kuondoka kwa Imam (a.s.) kutoka Makkah kwenda al-Kufah, yeye aliondoka kuelekea huko al-Kufah. Hata hivyo, hakuwahi kufika Karbala mpaka ile siku baada ya Ashura wakati ambapo Shahada ya Imam tayari ilikuwa imekwisha kutokea. Yeye alikwenda kwenye jeshi la Umar ibn Sa'd na akauliza: "Yuko wapi al-Husein ibn Ali?" Wao wakamuuliza: "Wewe ni nani?" Akajibu: "Mimi ni Hafhaf Basri. Nimekuja kumsaidia Imam al-Husein (a.s.). Nimesikia kwamba yeye alilazimishwa kuja Karbala peke yake na akiwa mgeni kabisa hapa." Wakamwambia: "Tumemuua Husein na wale wote aliokuwa nao. Hakuna aliyebakia kati yao isipokuwa wanawake, watoto na mtoto wa al-Husein ambaye ni mgonjwa. Hivi huyaoni mahema yake yaliyoporwa?"

Pale Hafhaf alipotambua kuhusu kuuawa kwa al-Husein (a.s.) na kuporwa kwa mahema yake, yeye alikamata upanga wake na akaanza kuwashambulia maadui. Hao maadui wakatawanyika pande zote. Kila aliyefika karibu yake ama aliuawa au kujeruhiwa. Hafhaf alipigana kama simba mkali mpaka pale ambapo, kwa amri ya Umar ibn Sa'd, akawa amezingirwa.

Imam Ali ibn al-Husein (a.s.) amesimulia hivi: "Katika siku ile, watu wa al-Kufah walikuwa hawajaona bingwa wa upanga hodari kama Hafhaf isipokuwa wale wa Nyumba ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wapiganaji maarufu kumi na tano mionganini mwa jeshi la maadui walimzingira na kumuuwaa. Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe pamoja naye!"

(*Ma'ali al-Sibtayn*)

SHAHADA YA SUWAYD IBN UMAR

Suwayd ibn Umar alikuwa ni mzee aliyepigana kwa ajili ya Imam al-Husein mnamo Siku ya Ashura. Hata hivyo, kutokana na majeraha mengi mno aliyopata kutoka kwenye panga na mikuki, yeye alianguka chini kutoka kwenye kipando chake. Alirejewa na fahamu na akatambua kwamba Imam (a.s.) alikuwa amekwisha kuuawa. Al-iwashambulia maadui kwa kisu mkononi mwake na akapigana nao mpaka alipouawa. Kwa mujibu wa taarifa hii, yeye alikuwa ndiye wa mwisho kupata Shahada hapo Karbala.

(*Maqta al-Husayn*)

Kwa haya inafika mwisho taarifa fupi juu ya maelezo ya Shahada za baadhi ya wafuasi wa Imam (a.s.) ambao sio Bani Hashim, mnamo siku ya Ashura.

MLANGO WA SITA

KUULIWA KISHAHIDI KWA FAMILIA YA IMAM HUSEIN (A.S.)

BANI HASHIM WAJIANDAA KWA MAPAMBANO

Baada ya wale wafuasi mbali na Bani Hashim kuwa wameuawa wote, sasa Bani Hashim wakajiandaa kwa kupigana na lile genge la wauaji makatili katika mtindo wa mtu mmoja mmoja. Hawa Bani Hashim walikuwa ni watoto wa Imam (a.s.), ndugu zake, wapwa zake na binamu zake. Mmoja baada ya mwingine, walimuaga Imam na kuelekea kwenye takdiri yao ya mwisho, peke yao. Walipigana mpaka pumzi zao za mwisho, wakimtetea na kumlinda bwana wao na kipenzi cha nyoyo zao, mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na bwana wa vijana na wakaazi wa Peponi.

KIZAZI CHA IMAM (A.S.)

Kwa mujibu wa Sheikh al-Mufid, Imam alikuwa na watoto sita. Nao walikuwa ni:

- i. Ali ibn al-Husein, Zayn al-Abidin, ambaye mama yake alikuwa ni Shahzanan binti wa mfalme wa Uajemi.
- ii. Ali ibn al-Husein, Ali al-Akbar, ambaye mama yake alikuwa ni Layla

- iii. Ja'far ambaye alifariki kabla ya matukio ya Karbala
- iv. Abd Allah, yule kichanga aliyeuliwa kwa mshale mikononi mwa Imam mnamo Siku ya Ashura, ambaye anajulikana pia kwa jina la Ali Asghar ambaye mama yake alikuwa ni Rabab
- v. Sakinah, ambaye mama yake alikuwa ni Rabab
- vi. Fatimah, ambaye mama yake alikuwa ni Ummu Ishaq.

(Kitab al-Irshad)

Mmoja wa mabinti hao wawili wa Imam hapo juu hujulikana pia kwa jina la Ruqayyah. Kwa mujibu wa mkusanyaji wa kitabu hiki, ni Fatimah binti al-Husein ambaye anajulikana kwa umaarufu kama Ruqayyah.

Kuna kutokukubaliana kiasi fulani mionganoni mwa wanachuoni kuhusiana na idadi ya watoto wa Imam Husein (a.s.), majina yao na ni yupi ndiye mkubwa kati ya Imam Ali Zayn al-Abidin na Ali al-Akbar. Baadhi yao wanaeleza kwamba Imam (a.s.) alikuwa na watoto wanne wa kike na kwamba mmoja wao aliiwa Zainab. Mwenyezi Mungu awashushie rehema Zake juu yao wote, vyovyote majina yao yatakavyokuwa na idadi yao pia.

WATOTO WA IMAM AL-HASAN (A.S.) WALIOPIGANA HAPO KARBALA

Inajitokeza kwenye vitabu kwamba wakati wa kifo chake cha kisha-hidi mnamo mwaka 49 A.H. Imam al-Hasan (a.s.) alikuwa na watoto wa kiume ishirini. Kati ya hawa saba walifuatana na ami yao Imam Husein (a.s.) kwenda Karbala na sita waliuawa mnamo ile Siku ya Ashura wakimlinda yeeye (a.s.). Watoto hao wa Imam Hasan (a.s.) na Imam Husein hapo Karbala walikuwa ni:

Hasan Muthanna
Ahmad ibn al-Hasan
Abu Bakr ibn al-Hasan
Qasim ibn al-Hasan
Abd Allah Akbar
Abd Allah Asghar
Bashshar ibn al-Hasan

Kati ya hawa Hasan Muthanna alichukuliwa kutoka kwenye medani ya vita akiwa amejeruhiwa na alikuwa ndiye pekee aliyepona na kuishi. Tukio hili litakuja kujadiliwa kwa kirefu katika kurasa zinazofuatia.

Kwa mujibu wa Sheikh Mufid, ni watoto watatu tu wa Imam al-Hasan ambao waliuawa hapo Karbala. Hawa walikuwa ni: Qasim, Abu Bakr na Abd Allah.

(*Kitab al-Irshad*)

Kwa mujibu wa Sheikh Qummui alikuwepo mtoto wa nne wa Imam (a.s.) aliyeitwa Ubaydullah ambaye pia aliuawa hapo Karbala.

(*Nafs al-Mahmum*)

Sayyid Muhsin Amin amewahesabu watoto wanne wa Imam al-Hasan kama wafiadini mashahidi: Qasim, Abd Allah, Abu Bakr na Bashshar ibn al-Hasan.

(*A'yan al-Shi'ah*)

Allamah Majlis anasimulia juu ya mtoto mwingine anayeitwa Yahya.

(*Bihar al-Anwar*)

Sayyid Ibn Tawus anatoa majina ya Zayd na Umar kama ni watoto wa Imam al-Hasan ambao walichukuliwa kama mateka na jeshi la al-Kufah.

(*Al-Luhuf*)

Sheikh Jalil ibn Nima Hilli pia anamtaja mtoto wa Imam (a.s.) anayeitwa Amr ibn al-Hasan ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi na mmoja, naye alichukuliwa hadi Syria kama mateka. Anatoa maelezo yafuatayo: “Wakati Imam Ali ibn Husein Zayn al-Abidin alivyoitwa na Yazid pale alipokuwa yuko Syria, Amr ibn al-Hasan alikwenda pamoja naye. Yazid alimtzazama Amr ibn al-Hasan na akauliza kama angepigana mieleka na mwanawe. Amr ibn al-Hasan akajibu kwamba angependelea wote wawili wapewe visu kisha waruhusiwe kupigana. Kwa hili Yazid alijibu: ‘Familia ya Mtume, awe mdogo ama mkubwa hatoacha kutuchukia sisi.’ Kisha akasoma ubeti ufuatao: ‘Hii ni desturi ambayo nimejifunza kutoka kwa Akhzam. Hivi nyoka anaweza kuzaa kingine badala ya nyoka?’ Katika suala hili maana yake ni kwamba Nyumba jasiri hutoa watoto jasiri vilevile.””

SHAHADA YA ALI IBN AL-HUSEIN – ALI AKBAR (A.S.)

Ali Akbar alikuwa wa kwanza kutoka miongoni mwa Bani Hashim kwenda kwenye mapambano. Hii ilikuwa ni baada ya wale waliokutana

wa sio Bani Hashim kuuawa wote na ikawa imeamuliwa kwamba Bani Hashim watapigana mmoja mmoja katika mapambano ya mtu mmoja mmoja. Ali Akbar ameelezewa kuwa na umri kati ya miaka kumi na nane na ishirini na saba wakati wa kuuawa kwake kishahidi.

Ali Akbar alikwenda kwa baba yake, Imam Husein (a.s.) kupata ruhusa ya mapambano. Imam (a.s.) huku akitokwa na machozi aliangalia juu angani na kuinyooshea vidole vyake viwili akisema: “Ewe Allah! Kuwa shahidi dhidi ya watu hawa, kwani sasa ninamtoa dhidi yao yule mwanangu ambaye anabeba kufanana kukubwa na Mtume Wako kwa sura na tabia na maongezi. Ewe Allah! Yeye huyu ndiye ambaye huwa tunamuangalia pale tunapotamani kumuona Mtume Wako (s.a.w.w.).”

Ali Akbar alisonga mbele kuelekea kwa maadui akizivunja safu zao na peke yake akapigana dhidi yao. Hata hivyo, walianza kumzingira wakivunja ile desturi ya pambano la mtu mmoja mmoja. Wakati Ali Akbar alipokuwa akipambana vikali sana, alikuwa akighani:

“Mimi ni Ali mwana wa al-Husein ibn Ali, Sisi, naapa kwa Nyumba ya Allah, tuko karibu sana na Mtume.

“Wallahi, mtu aliyezaliwa kwa zinaa (ibn Ziyad) hatatawala juu yetu.

Nitakupiga na kukuangusha chini kwa upanga wangu nikim-linda baba yangu.

“Mapigo ya mtu wa Bani Hashim, wa kizazi cha Alawiyyah.”

Ali Akbar alishambulia vikali sana dhidi akiwauwa wapanda farasi mia moja na ishirini. Hata hivyo, kutokana na kiu kali, alirejea kwa Imam (a.s.) akisema: “Oh baba! Kiu inaniua mimi na uzito wa

deraya hii inanichosha.” Akiwa hana uwezo wa kumpatia majibu ya maombi yake, kwa ajili ya japo tone la maji, Imam (a.s.) alianza kulia na akasema: “Kuwa na subira, ewe pendo la moyo wangu! Karibuni Mtume atakupatia kinywaji kutoka kwenye chemchemi ya Peponi.” Halafu Imam (a.s.) akauchukua ulimi wa Ali Akbar na kuweka kinywani kwake ili kupunguza kiu yake.

Akitupa deraya yake pembeni, Ali Akbar sasa akiwa bila matumaini ya kuishi katika dunia hii na akitamani sana kukutana na Mola Wake alirejea kwenye medani ya vita. Alipokuwa akipenya kwenye safu za maadui, alikuja kuzingirwa ghafla na akashambuliwa kutoka kila upande. Katikati ya panga na mikuki yenyeye uchu iliyokuwa ikilengwa kwenye mwili huu mtukufu, mshale mmoja ulitupwa ambao ulichana koo lake, yeze akamgutia baba yake mwenye utu uzima wa umri: “Ewe baba! Zipokee salamu za mwisho kutoka kwa mwanao anayefariki. Huyu hapa ni babu yangu, Mtume wa Mwenyezi Mungu akikusalimia kwa amani na akisubiri kuwasili kwako. Yeze ameizima kiu yangu kwa kikombe chake kitukufu. Baada ya hapo mimi sitahisi kiu tena.”

(Maqta al-Husayn al-Muqarram)

Imesimuliwa pia: Wakati Ali Akbar, amani juu yake, alipokuwa akipambana na maadui wale waliokuwa wamemzingira, Murrah ibn Munqidh Abdi, mpiganaji katika jeshi la Umar ibn Sa'd aliweka nadhiri kwa rafiki yake akisema: “Nitapiga pigo kwenye kifua cha kijana huyu ambalo litasababisha moyo wa baba yake kutoa damu hata kama dhambi za waarabu wote zinaniangukia mimi.” Baada ya kuyasema hayo, Murrah akajificha nyuma ya mti. Ali Akbar aliendelea kupangua mapigo ya maadui waliokuwa wamejikusanya karibu yake. Wakati Ali Akbar alipofika karibu na mti ule akishughulika na mapigano, Murrah aliutumbukiza mkuki wake kwenye kifua chake.

Ali Akbar, akiwa hawezi kubakia juu ya farasi wake, alianguka chini ambako maadui walimzunguka walimkata vipande vipande kwa panga zao. Kuna riwaya nyingine pia inayosema kwamba Murrah alikipiga kichwa cha Ali Akbar kwa upanga wake.

Katika maelezo mengine, imesimuliwa kwamba: “Ali Akbar, akiwa hawezi kukaa vizuri katika kipando chake, aliweka kichwa chake kwenye manyoya ya shingo ya farasi yake na akafunga mikono yake kwenye shingo ya farasi huyo. Farasi huyo akiwa ameshikwa na hofu alikimbilia kwa maadui ambaao walimkata Ali Akbar vipande vipande. Ali Akbar akaanguka chini. Roho yake takatifu ilipofikia hatua ya mwisho ya kuaga dunia, yeche aliita: “Oh baba yangu! Huyu hapa babu yangu Mtume wa Mwenyezi Mungu. Amenipatia mimi kinywaji kutoka kwenye kijito cha mbinguni.”

(Kibrit al-Ahmar)

Imam (a.s.) akijitahidi kwa machungu makali alifika alipokuwa Ali Akbar amelala. Akiangalia hali ya mtoto wake ambaye alikuwa ndiye nuru ya macho yake, alisihii kwa kukata tamaa kabisa: “Mwenyezi Mungu awaangamize watu waliokuuwa wewe! Wamekuwa mafidhuli kiasi gani mbele ya amri za Mwenyezi Mungu katika kuvunja utukufu wa Mtume (s.a.w.w.)!” Machozi yalitiririka kutoka machoni mwake na kulowesha mashavu yake na ndevu tukufu alipokuwa akilia hivyo. “Oh, mwanangu! dunia imepoteza thamani yake bila wewe.”

Bibi Zainab alitoka akikimbia kutoka kwenye mahema huku akilalamika: “Ewe kaka yangu! Ewe Ali Akbar!” Alikimbilia kwenye mwili wa Ali Akbar na akajitupa juu yake. Imam akamvuta Bibi Zainab na kumuondoa kwenye ule mwili uliokuwa umetapakaa

damu ambao alikuwa ameukumbatia na akamrudisha hadi kwenye mahema.

(Kitab al-Irshaad)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Imam (a.s.) aliikinga kwenye viganja vyake ile damu iliyokuwa ikitiririka kutoka kwenye viungo vilivyokatwa katwa vya Ali Akbar na akairusha damu hiyo kuelekea angani mbinguni huku akilia machozi, akisema: “Oh mwanangu! Ni vigumu sana kwa babu yako na baba yako mzee kuubeba ukweli kwamba wewe uliwaita nao hawakuweza kukusaidia kitu.” Halafu Imam (a.s.) akaweka uso wake mkabala ni ule uso wa Ali Akbar uliokuwa umegubikwa na damu na akalia kwa sauti kubwa kilio kisichodhibitika kwa namna ambayo hajawahi kufanya hapo kabla ya siku ile.

(Nafs al-Mahmum)

Kisha Imam (a.s.) akaubeba ule mwili uliochanwa chanwa wa Ali Akbar, amani juu yake, mikononi mwake na akasema: “Ewe mtoto! umepata mapumziko kutokana na huzuni na dhiki za dunia hii na ukamuacha baba yako peke yake na bila ya kuwa na wasaidizi.”

(Maqtal al-Husayn cha Abu Makhnaf)

Na halafu akawageukia vijana wa familia yake na akasema: “Njoni muuondoshe mwili wa ndugu yenu.” Vijana hao wa Bani Hashim wakaubeba mwili wa Ali Akbar na wakauweka mbele ya mahema ambapo vita vilikuwa vinapiganwa hapo.

Humayd ibn Muslim amesimulia: Mwanamke mmoja alitoka nje ya mahema hayo akiguta: “Ole, mwanangu! Ole kwa huzuni ya kuondokewa! Ole kwa kukosa wasaidizi!” Imam alimwendea mara

moja na kumrudisha ndani ya hema. Mimi nikauliza: “Mwanamke huyu alikuwa ni nani?” Nikaambiwa kwamba, “alikuwa ni Zainab binti ya Ali ibn Abi Talib.” Bibi huyo alilia kwa sauti kubwa na Imam (a.s.) akalia pamoja naye huku akisoma: “Kwa hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tutarejea.”

(at-Taarikh at-Tabari)

Wengine wamesimulia kwamba Bibi Layla, mama yake Ali Akbar alikuja kwa Imam (a.s.) na akasema: “Ewe Bwana! namtaka mwanangu. Ni nini kilichomtokea mwanangu?” Imam akamchukua na kumrudisha ndani ya mahema na kumtaka aswali na kuomba.

(Ma’ali al-Sibtayn)

Kuna wengine vilevile ambao wamesimulia kwamba baada ya kupatikana Shahada ya Ali Akbar, dada yake, Bibi Sakinah alitoka akikimbilia kwa baba yake na kuuliza: “Ewe baba! kwa nini umehuzunika hivyo? Ni nini kimemfika kaka yangu?” Yeye Imam (a.s.) alimjibu: “Maadui wamemuua.” Sakinah akaguta: “Oh, kaka yangu! Ewe pendo la moyo wangu!” Imam akamwambia huku machozi yakimtoka: “Oh, Sakinah! Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, libebe hili kwa subira na ustahimilivu.” Yeye akasema: “Ewe baba yangu! Ni vipi atawenza, mtu ambaye ndugu yake ameuliwa, na ambaye baba yake ameondokewa naye alihimili hilo kwa subira na uvumilivu?” Imam (a.s.) akasoma: “Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tunarejea.”

(al-Waqai ’i wa-al-Hawadith)

Kulingana na riwaya nyingineyo, wanawake walikwenda kwenye ule mwili uliolowana damu wa Ali Akbar, wakiongozwa

na Bibi Zainab. Aliuangukia mwili huo na akauchukua mikononi mwake. Kwa mhemko mkali na huzuni, ye ye alilia kwa sauti kubwa tu: “Mwanangu! Ali wangu!”

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

Abu al-Hasan alighani beti zifuatazao zikiashiria huzuni ya Imam (a.s.) kwa kifo cha Ali Akbar, amani juu yake:

“Ewe nyota! ni mfupi kiasi gani muda wa uhai wako,
Hiyo ndio namna ya maisha ya nyota zichomozazo alfajiri!
“Kupatwa kwake kulimharakia kabla ya muda wake,
Hivyo kukamfunika kabla haujawa mwezi kamili.
“Wakati nikizungumza, basi wewe ni wa mwanzo wa maneno yangu,
Na ninyamazapo kimya, basi daima umo mawazoni mwangu.”

SHAHADA YA ABDALLAH IBN MUSLIM IBN AQIL (A.S.)

Yule mtoto wa Muslim ibn Aqil anayeitwa Abdallah alikuwa mmoja wa wafuasi wa Imam (a.s.) katika ile Siku ya Ashura. Alikwenda kwa Imam (a.s.) kuomba ruhusa ya kuingia kwenye mapambano. Imam akamwangalia Abdallah na akasema: “Oh, mwanangu! huzuni ya kifo cha Muslim inatosha juu ya familia yako.” Abdallah akajibu: “Ewe ami yangu! mimi nitajiwasilishaje mbele ya babu yako, Mtume wa Allah mnamo Siku ya Hukumu kama nitajiruhusu mwe-nyewe kuishi wakati wewe unauawa? Mimi sitalikubali hili kamwe.

Nitapigana na maadui zako hadi nitakapokutana na Mola wangu.” Abdallah alikwenda kwenye uwanja wa mapambano huku akisoma beti zifuatazo:

“Sisi ni watoto wa Hashim;
Kamwe sisi hatutamtelekeza mtoto wa binti ya Mtume,
Simba kutoka kwenye damu ya Ali.
Nitawaangamiza kwa silaha zangu
Kwani mnamo Siku ya Hesabu
Ninatamani kuokolewa na Mola wangu.

Abdallah alipigana kishujaa na akawaua wengi wa maadui mpaka hatimae mshale ukapenya kwenye shingo yake. Wakati alipokuwa akianguka chini maneno yake ya mwisho yalikuwa: “Ewe baba! mgongo wangu umevunjika.” Imam upesi sana alifika kwenye mwili huo uliochanwa na kuloana damu wa Abdallah. Akasoma, “Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tutarejea.” Halafu yeeye akaomba: “Oh, Allah! wauwe wale watu waliokiuwa kizazi cha Aqil.”

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

Imesimuliwa pia kwamba: Abdallah alikuwa ni mtu baada ya Shahada ya Ali Akbar ibn al-Husein (a.s.) kuingia kwenye medani ya vita. Alikwenda huku akisoma beti zifuatazo:

“Leo nitakutana na Muslim baba yangu
Na wale watu ambaao wametoa uhai wao
Kwa ajili ya dini ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

Abdallah alifanya mashambulizi matatu dhidi ya maadui akiuwa idadi kubwa kati yao mpaka Zayd ibn Ruqad alipomrushia mshale. Abdallah alinyanya mkono wake hadi usoni mwake ili kuukinga mshale huo. Mshale huo ulichana kwenye mkono wake na kupenya kwenye paji la uso wake ukiushona mkono na uso wake. Abdallah alishindwa kutenganisha mkono wake kutoka kwenye paji la uso wake. Kwa uchungu sana aliguta kwa sauti: “Ewe Mungu! wafanyie maadui zetu kama vile wanavyotufanya sisi.” Mwingine kati ya maadui alikuja mbele yake na akachoma mkuki wake kwenye kifua chake. Kwa namna hii ndivyo Abdallah alivyokutana na Mola Wake..

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

SHAHADA ZA AWN NA MUHAMMAD, WATOTO WA BIBI ZAINAB (A.S.)

Bibi Zainab alikuwa ni dada mkubwa wa Imam Husein (a.s.). Ali-zaliwa mjini Madina mnamo mwezi 5 Jamad al-Ula ima mwaka wa 5, wa 6 au wa 7 Hijiria. Alifariki akiwa na umri wa miaka kati ya sitini na mbili na sitini na nne ama huko Misri, Syria au Madina. Ali-olewa na Abdullah ibn Ja’far, binamu yake, kwa kuelewana kwamba wakati wowote kaka yake Imam Husein (a.s.) atakapotaka kusafiri na yeche angependa asafiri pamoja naye, yeche Abdullah asingemzuia.

Imesimuliwa kwamba Bibi Zainab alikuwa na watoto watano, wa kiume wanne ambao ni Ali, Awn Akbar, Muhammad na Abbas na binti aliyeitwa Ummu Kulthum.

(Riyahin al-Shari’ah)

Katika wakati ambapo Imam (a.s.) aliondoka Makka pamoja na wafuasi wake wakielekea Iraq, Bibi Zainab alifuatana naye. Abdullah, kutokana na umri mkubwa na maradhi, yeye hakuweza kuandamana pamoja nao. Mahali pake alituma vijana wake wawili, Awn na Muhammad, akimuagiza Bibi Zainab kuwatoa kwenda kwenye mapambano endapo maadui wataanzisha vita dhidi ya Imam (a.s.). Kuna baadhi waliosimulia kwamba Abdullah aliwatoa Awn na Muhammad kwa Bibi Zainab wakati Imam alipoamua kuondoka kuelekeea Iraq.

Na kuhusu Awn, inakubaliwa na wasimulizi wengi kwamba yeye alikuwa ni mtoto wa Bibi Zainab. Hata hivyo, Tabari anadai kwamba yeye alikuwa ni mtoto wa Jumanah binti ya Musayyib. Kwa mujibu wa baadhi ya vyanzo, Khawsa binti ya Khasafah ndiye alikuwa mama yake Muhammad. Hata hivyo, kitabu cha Kamil al-Baha'i kinashikilia kwamba wote hao walikuwa ni watoto wa Bibi Zainab. Waliuliwa hapo Karbala siku ya Ashura wakimtetea ami yao, Imam (a.s.).

(Muntakhab al-Tawarikh)

Mnamo ile Siku ya Ashura, Bibi Zainab aliwasafisha Awn na Muhammad, akawapaka wanja machoni mwao na akawavisha nguo mpya. Kisha akawakabidhi panga na akawapeleka kwa kaka yake, Imam Husein (a.s.) kwa ajili ya ruhusa ya kwenda kwenye medani ya vita. Imam alimkatalia akisema: “Abdullah mume wako anaweza asikubaliane na hili.” Zainab akamjibu: “Lakini mbona ni yeye aliyenagiza mimi kwamba itakapokuwa ni vita basi niwalete wanawe mbele kabla ya wanao wewe!” Bibi Zainab alisisitiza hivyo mpaka Imam (a.s.) kwa kusitasita akawapa ruhusa.

Wakati Umar ibn Sa'd watoto hao wawili wakiingia kwenye mapambano juu ya vipando vyao, aliguta kwa mshangao: “Ni mapenzi

kiasi gani ambayo Zainab lazima awe nayo kwa kaka yake kuweza kuwa amezituma zile nuru za macho yake kwenye medani ya vita!” Watoto hao wawili walipambana hadi pale Muhammad alipoangushwa chini. Awn alikwenda kwa ndugu yake aliyekuwa anafariki. Akimuweka kwenye mapaja yake alisema: “Ewe kaka yangu! Usihuzunike. Mimi pia nitafuata hivi punde tu.” Awn aliendelea kupambana hadi pale naye alipoangushwa chini na kuaga dunia kwenda kwenye Makazi ya Kudumu. Akilia huku amezidiwa na majonzi, Imam (a.s.) alikwenda kwa watoto hao wawili. Aliwabeba miili yao kwa mikono yake, huku miguu yao ikiburuzika chini ardhini.

Miili ya Wafiadini ilipokuwa ikifkishwa kwenye mahema, wanawake wakitanguliwa na Bibi Zainab wangetoka nje ya mahema na kuomboleza vifo vyao. Hata hivyo, wakati miili ya watoto wake wawili ilipokuwa inaletwa, yeye Zainab (a.s.) hakuweza kuonekana. Sababu ya hili inaweza kuwa kwamba yeye hakutaka kulia kwa ajili ya wanawe hao asije kudhoofisha dhamira ya kaka yake, Imam (a.s.) ya kupigana na maadui hao. Badala yake anaweza kuwa amefikiri kuwa kulia kwake kwa ajili ya wanawe kungeweza kusababisha Imam (a.s.) kufadhaika kwa kufikiri kwamba yeye ndiye amekuwa sababu ya vifo vyao. Hiyo ndiyo ilikuwa tabia tukufu ya hali ya juu ya binti huyu wa Bibi Fatimah (a.s.).

(Tadhkirat al-Shuhadaa)

TAARIFA ZA SHAHADA ZA AWN NA MUHAMMAD ZAMFIKIA ABDALLAH IBN JA'FAR (A.S.)

Wakati habari za kuuawa kishahidi kwa Awn na Muhammad zilipofika Madina, Abu Salasil, huria wa Abdallah alichana shati lake kwa

uchungu wakati wa taarifa ya vifo vyao. Kwa huzuni kubwa, yeye alimjulisha Abdallah juu ya vifo vyao na akalalamika: “Oh, Awn! Oh, Muhammad! Enyi matunda mawili ya macho yangu! Utulivu wa moyo wangu! Ni nani alikuwa bora kuliko ninyi? Masaibu haya yametufika sisi kwa sababu ya al-Husein. Kama msingeandamana naye haya yasingetokea.”

Katika kuzipokea taarifa za Shahada zao kwa mtindo huu, Abdallah alisoma ile aya ya; “Hakika sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake Yeye tunarejea.” Halafu akamkaripia Abu Salasil kwa hasira na ukali akisema: “Unathubutuje kutamka maneno kama hayo yasiyo ya heshima juu ya Imam Husein (a.s.)! Sifa zote ni juu ya Mwenyezi Mungu ambaye alikubali na kuwaruhusu wanangu kupata vyeo vya Ufiadini – Shahada sambamba na al-Husein! Endapo tu ningekuwa pamoja nao na kuuliwa kabla yao! Wallahi! mimi niliwaambia wao wafe kwa ajili ya Husein (a.s.). Sasa nimeachwa nikiwaomboleza wao pamoja na bwana wetu, Imam al-Husein.”

(Rayyhan al-Shari'ah)

SHAHADA YA QASIM IBN AL-HASAN (A.S.)

Qasim ibn al-Hasan (a.s.) alikuwa hajafikia umri wa balehe wakati wa kifo chake cha kishahidi hapo Karbala. Kwenye mkesha wa Ashura, wakati Imam (a.s.) alipowafahamisha wafuasi wake waaminifu juu ya vifo vyao vitakavyotokea karibuni, Qasim ibn al-Hasan ambaye naye alikuwemo kwenye mkusanyiko huo pia, alikwenda kwa Imam (a.s.) na kumuomba: “Ewe ami yangu! na mimi pia nitauliwa?” Imam (a.s.) akamkumbatia na kusema: “Ewe mtoto! je, unakionaje kifo?” Yeye akajibu: “Kitamu mno kuliko asali!” Imam akamwambia: “Wewe utauawa baada ya balaa kubwa mno na vivyo hivyo kwa Abdallah, kile kichanga (Ali Asghar).”

(Al-Waqa'i wa al-Hawadith)

Qasim ibn al-Hasan alijiweka tayari kwa vita katika siku ya Ashura. Halafu akaenda kwa Imam (a.s.) kwa kuagana naye kwa mara ya mwisho. Imam akamkumbatia Qasim kifuani mwake na wote wakalia kwa muda kiasi. Qasim aliomba ruhusa kwa Imam ya kuingia kwenye mapambano. Hata hivyo, Imam (a.s.) alisitasita. Qasim alimuomba kwa kurudiarudia mpaka Imam kwa shingo upande akamruhusu. Qasim akiwa amehuzunika pamoja na machozi yakimdondoka kwenye mashavu yake, alisonga mbele kwenye mapambano huku akighani:

“Mimi ni mtoto wa al-Hasan kama ninyi hamtambui”

Mjukuu wa Mtume, mteuliwa, aliyeaminika.

“Huyu ni Husein kama mateka aliyeshikiliwa kwa ajili ya fidia,

kwa ajili ya watu ambao kiu yao haiwezi kuzimwa na mvua inyeshayo.”

Qasim alianzisha mapambano dhidi ya maadui na akawauwa watatu kati yao.

Humayd ibn Muslim amelisimulia tukio hili kwa namna ifuatayo: Kijana mbichi alitoka nje ya mahema ya Imam al-Husein (a.s.) na akasogelea kwenye medani ya vita. Uso wake ulikuwa kama kijincha cha mwezi mpya. Alikuwa na upanga mkononi mwake na alikuwa amevaa shati refu. Alipokuwa akiingia ndani ya uwanja wa vita na akashughulika na kupigana, Amr ibn Sa'd aliyekuwa amesimama karibu na mimi akasema: “Wallahi, niache nimshambulie huyu mtoto!” Mimi nikamuuliza; ‘kwani wewe una sababu gani naye mtoto huyu? Yeye ni mtoto bado. Waache wale waliomzunguka wammalize. Wallahi, mimi nisingenyanua japo kidole changu dhidi

yake hata kama angekuwa aniangushe kwa pigo la upanga wake.” Yeye akarudia tena: “Wallahi niache nimshambulie mtoto huyu niyafanye maisha kuwa ni mateso kwake.” Wakati Qasim ibn al-Hasan alipokuwa akipigana na wale askari waliokuwa wamemzunguka, Amr alinyemelea nyuma yake na akampiga kichwani mwake kwa upanga wake. Kichwa cha Qasim kikapasuka na kufunguka wakati akianguka chini kutoka kwenye kipando chake akiangukia uso wake uliobarikiwa na akaguta akiita kwa sauti: “Ewe ammi yangu! Njoo unisaidie.”

Imam (a.s.) alikuwa amesimama akimuangalia mpwawe Qasim. Mara tu Qasim alipomuita yeye, Imam (a.s.) alishuka kama tai anavyoshukia mawindo yake, akaanzisha pambano kali akipenya kwenye safu za maadui hadi alipofika kwa Amr Azdi. Imam akampiga kwa upanga wake. Amr akanyanya mkono wake kujikinga na pigo hilo na mkono wake ukakatika kutokea kwenye kiwiko. Amr aliomba kusaidiwa kuokolewa kutokana na Imam (a.s.). Farasi wao wakapigana kumbo na Amr akaanguka chini. Farasi wale wakakanyaga juu ya mwili wake na akashetwashtewa kwa kwato zao hadi akafa. Hatimae waliweza kumbeba na kumuondoa. Pale wingu la vumbi na mchanga uliotimuliwa na wale farasi lilipotulia, Imam alionekana akiwa amesimama karibu na Qasim. Alikuwa anasugua miguu yake juu ya ardhi wakati roho yake ilipotoka kwenye mwili uliokatwakatwa. Imam (a.s.) aliweka shavu lake kwenye kile kifua cha Qasim kilichochanika akilia na kuomboleza; “Ewe mwanangu! Ni jambo lisilovumilika kwamba wewe ulimuita ami yako aliyezeeka nami sikuweza kufika kukusaidia. Na nilipofika, kufika kwangu hakukuwa na msaada wowote.”

Imam (a.s.) aliuchukua mwili wa Qasim mikononi mwake na akambeba huku nyayo za Qasim zikiwa zinaburuzika chini ardhini, mpaka kwenye miili ya wanae, kaka zake na wafuasi wake ilipokuwa

imehifadhiwa. Aliuweka mwili wa Qasim karibu na mwili wa mwanae Ali Akbar na akawaambia maiti hao: “Enyi wapwa zangu! Stahimilini. Enyi wanangu! Kuweni na subira. Wallahi! hamtakutana na huzuni yoyote baada ya siku hii ya leo.”

(A yan al-Shi'ah)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Imam (a.s.) aliuweka mwili wa Qasim karibu na ule wa Ali Akbar. Kisha akakaa katikati ya wawili hao. Alivua kilemba chake na akatapanya vumbi kwenye kichwa chake. Halafu akaweka mkono wake wa kulia kwenye kifua cha Ali Akbar na ule wa kushoto kwenye kifua cha Qasim. Macho yake yakiwa yamejawa na machozi, yeye aliangalia juu angani na akaita kwa sauti; “Ewe Mola wa walimwengu wote! Husein amenyang’anywa watoto wake.”

Katika baadhi ya riwaya, kwamba wakati Imam (a.s.) alipomtuma Qasim kwenye uwanja wa vita, alikichana kilemba cha Qasim vipande viwili. Aliweka kipande kimoja kwenye mabega na kifua chake Qasim, kama kile kipande cha juu cha sanda ambapo aliifunga ile nusu nyingine kichwani kwake na ncha moja ikiangukia kupita usoni mwake na kuishia kwenye shingo yake mgongoni kwake. Ni kwa sababu hii kwamba uso wa Qasim ulielezewa kama ncha ya kwanza ya mwezi mpya.

(Muntakhab Turayhi)

KUJERUHIWA KWA HASAN IBN MUTHANNA

Hasan Muthanna, mtoto wa Imam Hasan (a.s.) alikuwepo pamoja na ami yake Imam Husein (a.s.) hapo Karbala. Alikuwa amemuom-

ba Imam kumruhusu mkono wa mmoja kati ya binti zake, Fatimah ama Sakinah katika ndoa. Imam (a.s.) alikuwa amechagua kumuouza binti yake Fatimah kutokana na kufanana na mama yake Imam mwenyewe, Malikia wa wanawake wa Peponi, Bibi Fatimah (a.s.). Mwenyezi Mungu ashushe rehema Zake juu ya roho za Muhammad na kizazi chake kisafi kabisa! Ndoa hiyo ilipitishwa ama wakati wa kuondoka kwao kutoka Madina au wakiwa njiani kuelekea Iraqi.

(Nafs al-Mahmum)

Mnamo ile Siku ya Ashura, Hasan Muthanna aliwa askari kumi na saba wa adui kabla ya kuanguka kwa kukosa fahamu kutokana na majeraha mengi mno aliyokuwa ameyapata katika mapigano hayo. Hasan Muthanna alibakia amekosa fahamu hadi mwezi 11Muharram. Wakimdhania kuwa amefariki, maadui hawakumgusa mpaka siku iliyofuatia. Mnamo siku hiyo ya mwezi 11Muharram, siku moja baada ya Ashura, Umar ibn Sa'd aliamuru askari wake kuwakata vichwa wale wafuasi wa Imam Husein (a.s.) waliokuwa wameuliwa kishahidi, Bani Hashim na wale ambao sio Bani Hashim kadhalika. Ilikuwa ni katika muda huu ambapo kwamba askari hao waligundua kwamba Hasan Muthanna alikuwa bado anayo nuru ya uhai. Taarifa hizo zilimfikia Asma' ibn Kharjah, kamanda mmoja katika jeshi la Umar ibn Sa'd na ndugu yake Khawlah, mama yake Hasan Muthanna. Yeye alisisitiza kwamba Umar ibn Sa'd ayabakishe maisha ya Hasan Muthanna. Ombi lake lilikubaliwa.

Asma' alimchukua Hasan Muthanna ambaye alikuwa bado hana fahamu hadi mjini al-Kufah kwa ajili ya matibabu. Humo njiani Hasan Muthanna alirejewa na fahamu zake. Yeye alifadhaishwa na hali hiyo na akauliza kuhusu ammi yake al-Imam Husein (a.s.). Aliposikia masaibu yaliyompata Imam na wafuasi wake waaminifu, Hasan Muthanna alihuzunika kupita kiasi na kusikitishwa sana.

Asma' alimchukua hadi al-Kufah na akahakikisha kwamba anapata uangalizi wa kitiba.

Baada ya Hasan Muthanna kupata nguvu, Asma' alimrudisha Madina. Hasan Muthana alikaa pale Madina mpaka kufikia umri wa miaka thelathi na tano ambapo alipewa sumu hadi kufariki kwa maelekezo ya Abd al-Malik, khalifa wa tano wa Bani Umayyah. Hasan Muthanna alizikwa katika viwanja vya makaburi vya Baqi' hapo Madina. Hasan Muthanna alibeba jina la Tabataba'i, na ndiye ambaye Sadat ya kizazi cha Tabataba'i wanamoshukia.

(Minhaj al-Dumu')

SHAHADA ZA ABDALLAH, JA'FAR NA UTHMAN – NDUGU ZAKE ABBAS IBN ALI (AMANI JUU YAO)

Abbas ibn Ali ambaye kifo chake cha kishahidi kitaelezewa hivi punde, alikuwa na ndugu watatu kutoka kwa wazazi wale wale, Imam Ali (a.s.) na Ummu Banin. Ndugu hao walikuwa ni Abdallah ambaye alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano, Uthman aliyekuwa na umri wa miaka ishirini na moja na Ja'far ambaye alikuwa na miaka kumi na tisa. Yeye Abbas alikuwa na umri wa miaka thelathini na nne na alikuwa ndio mtoto mkubwa kati ya watoto wa Ummu Banin. Mnamo siku ya Ashura, katikati ya mapambano ya vita aliwageukia ndugu hawa watatu na kusema: "Enyi watoto wa mama yangu! Songeni mbele! Hebu nishuhudie uaminifu na utii wenu kwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake."

Kila mmoja kwa zamu yake alisonga mbele kuwaelekea maadui na akapigana hadi alipouliwa kishahidi.

(A yan al-Shi'ah)

SHAHADA YA ABBAS IBN ALI (A.S.) KUZALIWA NA HADHI TUKUFU YA ABBAS IBN ALI

Abbas ibn Ali, ambaye mama yake alikuwa ni Ummu Banin, alizaliwa mjini Madina mnamo mwezi 4 Shaaban, 25Hijiria. Alikuwa amefikisha umri wa miaka kumi na nne wakati wa kifo cha kishahidi cha baba yake, Ali ibn Abi Talib (a.s.). Hapo Karbala, yeye alikuwa ndio mshika bendera wa Imam al-Husein (a.s.) na mwenye nguvu zaidi mionganoni mwa jeshi zima. Wakati wa Shahad yake, Abbas ibn Ali alikuwa na umri wa miaka thelathini na nne.

Jina halisi la Ummu Banin lilikuwa ni Fatimah. Yeye alikuwa ni mke wa pili wa Imam Ali (a.s.) baada ya kifo cha Bibi Fatimah (a.s.). Imam Ali (a.s.) alimwendea ndugu yake Aqil ambaye alikuwa ni bingwa wa elimu ya nasaba. Akamwambia: “Hebu tafuta mwanamke ambaye amezaliwa na mwanamke bora na mkamilifu kabisa mionganoni mwa Waarabu ili mimi niweze kumuo naye aweze kunizalia mpiganaji mzuri wa kifahari.” Aqil akamjibu: “Mchumbie Fatimah Kalbiyyah na umuoe. Hakuna familia ya kishujaa zaidi ya ile yake yeye mionganoni mwa Waarabu.”

Wakati alipojifungua mtoto wake wa kwanza, ambaye ni Abbas, alipelekwa kwa Imam Ali (a.s.). Imam alimbeba mwanae mikononi mwake na huku akiangalia mikono ya Abbas Imam alianza kulia. Alipoulizwa sababu ya huzuni yake, yeye Imam alijibu: “Mikono hii ya Abbas itakuja kukatwa kutoka mwilini mwake mnamo siku ya Ashura katika kumtetea na kumlinda mwanangu Husein (a.s.).”

Ummu Banin, ambalo ni jina lenye maana ya “mama wa watoto wa kiume” kwa sababu alijifungua vijana wa kiume wanen na pia alijifungua mabinti wawili. Vijana wa Ummu Banin na Imam Ali

(a.s.) walikuwa ni Abbas, Abdallah, Ja'far na Uthman. Wote hawa wanne waliuliwa hapo Karbala wakimtetea Imam Husein (a.s.). Mabinti zake walikuwa ni Ummu Hani na Jumanah.

Abbas ibn Ali alimuoa Lubabah binti ya Ubaydullah ibn Abbas, binamu yake Imam Ali (a.s.). Alikuwa na vijana wawili kutokana naye walioitwa Ubayd Allah na Fadhl. Kwa mujibu wa baadhi ya riwaya, yeye alikuwa na vijana wengine wawili kwa majina ya Muhammad na Qasim, ambao waliuliwa hapo Karbala pamoja na baba yao Abbas ibn Ali.

Abbas Ibn Ali alifanana na baba yake katika tabia na ushujaa wake. Inasimuliwa kwamba uso wa muuaji wa Abbas ibn Ali, ambaye alitoka kwenye kabilia la Bani Darim uligeuka na kuwa mweusi. Alipoulizwa kuhusu sababu ya hilo yeye alijibu: “Nimemuua mtu ambaye ana alama ya sijida kwenye paji la uso wake na alijulikana kama Abbas.”

(Al-Waqa'i' wa al-Hawadith)

Inasimuliwa kwamba Abbas ibn Ali alikuwa ni kijana mrefu na mtanashati mno. Alipopanda farasi wake, miguu yake ilikuwa inaweza kugusa chini ardhini. Alipewa cheo cha *Qamar Bani Hashim* (Mwezi wa Bani Hashim) na alikuwa mshika bendera wa jeshi la Imam Husein (a.s.).

(Maqatil al-Talibiyyin)

Wanahistoria wamemuelezea kwa maneno yafuatayo: “Alikuwa ni mlima mkubwa wenye moyo unaoweza kuvunjavunja ardhi kwa sababu yeye alikuwa ni shujaa hodari wa ukoo maarufu na simba asiyehofu, mwenye kujasiri kwenye hali ya mapambano na panga za makafiri zenye kushambulia kwenye medani ya vita.”

(Kibrit al-Ahmar)

Maana ya neno ‘*abbas* ni “umadhubuti.” Linaonyesha umadhubuti wa Abbas ibn Ali na uimara mbele ya maadui. Sifa za ajabu za Abbas ibn Ali na hali yake ya kutokuwa na woga vilikuwa ni matokeo ya kile alichokirithi kutoka kwa wazazi wake.

MAJINA YA VYEO VYA ABBAS IBN ALI

Abbas ibn Ali anayo majina kadhaa. Kila moja kati ya hayo lin-aelezea kipengele kimojawapo cha maisha yake, tabia na shakshia yake. Majina hayo ni:

1. *Abul Fadhl*, yaani baba Fadhili, mwanae mkubwa, au baba wa fadhila, wema, ambayo ndio maana hasa ya neno *Fadhl*.
2. *Abu Qirbah*, kwa maana ya neno ni ‘baba wa mfuko wa ngozi ya maji’ kwa vile aliletu maji kutoka mto Furati kuzima kiu ya wale waliokuwa pamoja na Imam (a.s.).
3. Qamar Banu Hashim, ‘Mwezi wa Banu Hashim’ – jina alilope-wa na baba yake, Imam Ali (a.s.) alipoufunua uso wake Abbas kwa maadui katika vita vya Siffin.
4. *Al-Abd al-Salih*, ambalo lina maana ya “mja mwadilifu wa Allah.
5. *Al-Muwasi*, ambalo lina maana ya ‘mwenye kutoa maliwazo.’
6. *Al-Fadi*, ambalo lina maana ya ‘mwenye kujitoa muhanga.’
7. *Al-Hami*, lenye maana ya ‘mwenye kukinga.’

8. *Al-Waqi*, lenye maana ya ‘mlinzi’
9. *Al-Sa’i*, ambalo lina maana ya ‘mwenye jitihada.’
10. *Bab al-Hawa’ij*, ambalo maana yake ni ‘njia kwa ajili ya mahitaji (ya watu)’
11. Hamil al-Liwa, lenye maana ya “mshika bendera,’ kwa sababu yeye alibeba bendera ile siku ya Ashura.

Katika kipindi cha mwanzoni cha historia ya Uislam wabeba bendera walikuwa na hadhi kubwa sana, takriban yenye muhimu wa karibu kama Amiri Jeshi Mkuu. Mambo mengi yalikuwa mabegani mwa wabeba bendera kuhusiana na mbinu na mikakati, kuamsha hamasa ya jeshi na kuwaelekeza askari kwenye ushindi wakati wa hali ya dhahiri ya kuelekea kushindwa. Kwa hiyo ilikuwa ni jambo muhimu kuwa na yule mbora katika jeshi kama mbeba bendera. Abbas ibn Ali alishikilia bendera ya Imam Husein (a.s.) ikiwa imenyanyuliwa juu kabisa mpaka ile dakika ya mwisho. Abbas alimudu hata kuisalimisha bendera wakati mikono yake ikikatwa kutoka viwiko vyake. Mwishowe aliikumbatia bendera kifuani mwake wakati aliposonga mbele kwa mara nyingine tena kuwaelekeea maadui waliokuwa wamemzingira pande zote. Aling’ang’ania kuishikilia bendera ili isianguke chini. Hili liliendelea mpaka pale kichwa chake kitukufu kilipopigwa kwa kiguzo cha chuma ambacho kilipasua kichwa hicho na kumfanya aanguke chini. Hata hivyo bado aliendelea kuikumbatia bendera hiyo.

(*Ma’ali al-Sibtayn*)

KIFO CHA ABBAS IBN ALI WAKATI AKIENDA FURATI KUJARIBU KUPATA MAJI

Wakati wale wafuasi wote wa Imam (a.s.), ambao sio Banu Hashim walipokuwa wamekwisha kuuliwa, Abbas Ibn Ali alimgeukia Imam (a.s.) na kumuomba: “Ewe kaka yangu! Niruhusu niingie kwenye mapambano ya vita.” Imam (a.s.) alilizwa na maombi haya kutoka kwa Abbas. Lakini Abbas ibn Ali aliendelea kumsihi ndugu yake: “Moyo wangu umesongwa sana na nimechoka na maisha. Niruhusu nilipize kisasi cha damu ya mashahidi hawa!” Hatimae Imam (a.s.) akiwa amejawa na machozi alisema: “Nenda ukachote maji kwa ajili ya watoto hawa wenye kiu.”

Abbas aliwaelekeea maadui na akawaasa akiwaonya juu ya matokeo maovu ya vitendo vyao. Lakini waliziba masikio yao kwenye maneno yake. Abbas alirejea kwa Imam (a.s.) na akasikia vilio vya watoto wale wenyewe kiu wakiomba maji. Inasimuliwa kwamba Imam aliweka hema maalum kwa ajili ya maji ambamo ngozi zote za maji zilihifadhiwa humo. Abbas aliingia ndani ya hema hilo na akawaona wale watoto wenyewe kiu wakiziweka zile ngozi tupu kwenye matumbo yao ili kupunguza kiu zao kwa ule ubichibichi wa ngozi hizo. Abbas hakuweza kuivumilia hali hii na akasema: “Enyi nuru za macho yangu! Mimi nitakwenda kuchota maji kwa ajili yenu.” Alichukua mfuko wa ngozi ya maji kwenye mkono mmoja na mkuki wake mkono wa pili na akapanda farasi wake ili kutoka kuelekea Mto Furati.

(Unwan al-Kalam)

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, wakati Abbas alipomuaga Imam (a.s.) aliangalia juu angani na akaomba: “Ewe Allah! Natamani

kutimiza kiapo changu cha kuleta maji kwa ajili ya watoto hawa wenye kiu.” Kisha akabusu paji la uso la Imam na akaenda kuelekea mto Furati.

Walikuwepo karibu askari kumi elfu wanaolinda kingo za mto Furati. Maadui walianzisha mashambulizi sita dhidi ya Abbas ibn Ali ili kumzuia kuyafikia maji. Abbas aliwatawanya na akauwa askari themanini kati yao. Alifanikiwa kuufikia mto Furati na akamuingiza farasi wake kwenye mto huo. Abbas alishuka na akachota maji viganjani mwake na akainyanya kuelekea kinywani kwake. Alipokaribia kuyanywa, aliikumbuka kiu ya kaka yake, Imam (a.s.) na akayamwaga chini.

(Akthir al-Ibadat)

Baada ya kuyamwaga chini maji hayo, Abbas ibn Ali, roho zetu ziwe fidia kwa ajili ya roho yake yeye, alighani beti hizi:

“Ewe nafsi! una thamani ndogo baada ya al-Husein,
Haikufaidii wewe kuishi baada yake,

“Huyu ni Husein aliyezingirwa na umauti,
Wakati wewe unataka kunywa kutoka kwenye maji baridi na matamu.

“Wallahi! Hiki sio kitendo cha dini yangu!”

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, yeye alisema: “Wallahi! mimi sitayaonja maji wakati bwana mkubwa wangu al-Husein (a.s.) ana kiu.”

(Bihar al-Anwar)

Kulingana na watu wengine, wakati wa usiku wa kuuliwa Shahidi kwa Imam Ali (a.s.), mwezi 21 Ramadhan, alimuweka

Abbas kifuani mwake na akasema: “Ewe mtoto! Kupitia kwako wewe mimi nitaheshimiwa mnamo hiyo Siku ya Kiyama, siku ya kufufuliwa. Oh, mwanangu! Wakati itakapowadia hiyo Siku ya Ashura na ukafika mtoni Furati, usije ukayanywa maji wakati ndugu yako al-Husein bado ana kiu.”

(Ma’ali al-Sibtayn)

Abbas alijaza maji ngozi na akaining’iniza kwenye bega lake la kulia na akaanza kurejea kwenye mahema. Askari wa maadui wakamzingira kutokea pande zote. Akiwa peke yake, alijaribu kuwapangua huku akisonga mbele kuelekea kwenye mahema. Abbas aliendelea kupigana mpaka pale ambapo, ama ilikuwa ni Nawfal ibn Azraq au Zayd ibn Warqa aliyekuwa amejificha nyuma ya shina la mti alipompiga upanga kwenye mkono wake wa kulia na kuukata kutoka kwenye kiwiko chake. Haraka sana Abbas akahamishia ule mfuko wa ngozi wa maji kwenye bega lake la kushoto huku akighani:

“Wallahi! Hata mkiukata mkono wangu wa kulia,
mimi daima nitaihami dini yangu.

“Na yule Imam ambaye kwa hakika
anatokana na kizazi cha Mtukufu Mtume,
Kitoharifu na kiaminifu.

Aliendelea kupigana na kuwauwa wengi wa wapiganaji wa panga maarufu kati ya maadui. Wengine wametoa idadi ya askari mia nane na hamsini na tano waliouawa na Abbas katika kadhibihiyo. Abbas aliendelea kupambana kupasua njia kuelekea kwenye mahema. Wakati alipokuwa akipigana hivyo, Hakim ibn Tufayl, laana juu yake, aliyekuwa amejificha nyuma ya mti wa mtende alimpiga Abbas kwenye mkono wake wa kushoto na kuukata kuanzia kwenye kiwiko chake. Hapa, Abbas alisoma beti zifuatazo:

“Ewe nafsi yangu! Usiwaogope makafiri hawa.
Chukua bishara njema za Mwenye Enzi

“Kwa Mtukufu Mtume, Bwana Mteuliwa
kwa kupiduka mipaka kwao, wameikata mkono wangu wa
kushoto.

“Ewe Mola Wangu! wasukumizie kwenye joto la Jahannam.

Abbas alijitahidi huku akiwa ameyakamata maji kwa meno yake katika jaribio la mwisho la kuyafikisha maji kwa wale watoto wenye kiu. Katika wimbi la mishale, mikuki na mawe, mshale mmoja ulichana ule mfuko wa ngozi na kufanya upasuke. Mshale mwingine ulipiga kwenye kifua chake na kusababisha yeze aanguke chini kutoka kwenye farasi wake.

(Muntaha al-Amal)

Abu Mikhraf anaandika hivi: “Licha ya ukweli kwamba mikono ya Abbas ilikuwa imekatwa vibaya na kwamba ilikuwa inaning’inia na huku ikivuja damu, kwa mara nyingine tena alisonga mbele kwenye safu za maadui. Mwishowe alipigwa kichwani na kipande cha chuma ambacho kilipasua kichwa chake na alianguka chini. Alivyokuwa akitetemeka kwenye damu yake, aliguta kwa sauti: “Ewe ndugu yangu! Oh, Husein! Pokea salamu zangu za mwisho.”

Kwa mujibu wa riwaya zilizo maarufu na kujulikana mno, yeze aliguta: “Ewe kaka yangu! Njoo umsaidie ndugu yako!” Imam (a.s.) alikimbilia kwenye mwili wake na akamkuta Abbas amezama kwenye damu, akiwa amevunikwa na idadi kubwa ya mishale na mikono yake ikiwa imekatwa kutoka mwilini mwake, na jicho lake likiwa limetobolewa na mshale. Imam (a.s.) kwa ukiwa kabisa akasimama mbele ya mwili wake kwa kukata tamaa kabisa. Kushindwa kulionekana kwenye uso wa al-Husein (a.s.). Alilia kwa

uchungu sana alipokuwa akiita: “Ewe ndugu yangu! Oh, Abbas! Ewe roho ya moyo wangu! Oh, kwa maangamizi baada yako! Oh, Abbas! Sasa mgongo wangu umevunjika kabisa; njia ya uwezo wangu imeteketea na matumaini yangu yamekatika ghafla.”

(Fursan al-Hayjan)

MANENO YA MWISHO KATI YA ABBAS NA IMAM (A.S.)

Inasimuliwa kwamba: “Imam (a.s.) alikiweka kichwa kilichojeruhiwa cha Abbas kwenye mapaja yake na alivyokuwa anasafisha damu kutoka kwenye jicho lake, Imam aliona kwamba Abbas alikuwa analia. Imam (a.s.) akamuuliza: “Ewe ndugu yangu! Kwa nini unalia?” Abbas akamjibu: “Oh, ndugu yangu! Ewe nuru ya macho yangu! Ni vipi mimi nitaweza kutokulia, wakati ninakuona umekibeba kichwa changu mapajani mwako nami ninajua kwamba hivi punde tu hakutakuwa na mtu wa kunyanya kichwa chako kutoka ardhini, na kukiweka mapajani mwake na kusafisha vumbi kutoka usoni mwako?” Imam (a.s.) aliketi karibu na Abbas mpaka sauti tupu ya ajabu ilipotoka na kusikika kutoka kwenye koo la Abbas wakati alipovuta pumzi ya mwisho na kukabidhi roho yake kwa Muumba Mwenye Enzi.

(Ma’ali al-Sibtayn)

Fadhl Darbandi anaandika katika *Asrar al-Shahadah*: Imam (a.s.) alikuwa ameamua kuubeba na kuurudisha ule mwili wa Abbas uliokuwa umeloa kwa damu yake. Hata hivyo, kabla tu ya kufariki kwa Abbas, alifungua jicho lake na akauliza: “Ewe kaka yangu! ni nini unachokusudia kufanya?” Imam akamjibu: “Nataka

niurudishe mwili wako kwenye mahema.” Abbas akasema: “Niache papa hapa.” Imam (a.s.) akauliza, “Kwa nini?” Abbas akanong’ona: “Ninamuonea haya binti yako Sakinah. Nilimuahidi kurudi na maji nami sikujaaliwa kufanya hivyo.” Imam (a.s.) akaomba du’a: “Mwenyezi Mungu akujaalie malipo mema kwa niaba ya ndugu yako mimi, kwani umenisaidia sana wakati ukiwa hai na sasa baada ya kifo chako.” Imam (a.s.) akamuacha Abbas pale mtoni naye akarejea kwenye mahema.

(Ma ’ali al-Sibtayn)

KUREJEA KWA HUZUNI KWA IMAM (A.S.) KUTOKA MTO FURATI

Imam (a.s.) alimuacha Abbas kwenye kingo za alqamah na akaondoka kurejea kwenye mahema huku akiyafuta machozi yaliyokuwa yakitiririka mashavuni kutoka machoni mwake kwa mikono ya nguo yake. Alipokuwa anakaribia mahema, Sakinah alitoka mbio kumkimbilia na akakamata hatamu za farasi wake. Aliuliza kwa shauku kubwa: “Ewe baba! Je, una taarifa zozote kuhusu ami yangu Abbas?” Imam (a.s.) alilia sana wakati akijibu: “Ewe mwanangu! Ami yako Abbas ameuawa na ameondoka kwenda Mbinguni.” Alipoyasikia haya, Bibi Zainab aliguta, na yeze pamoja na wanawake wote waliobakia wakaanza kuomboleza. “Ewe kaka yangu! Oh, Abbas! Ni nani atakayekuja kutusaidia baada yako wewe?”

(Kibrit al-Ahmar)

VILIO NA MAOMBOLEZO YA BIBI ZAINAB KWA KIFO CHA ABBAS

Katika maelezo mengine, wakati Imam (a.s.) alipofika kwenye ma-hema, Bibi Zainab alimkimbilia baada ya kusikia habari za kifo cha Abbas. Yeye alimuuliza Imam: “Kwa nini hukumrudisha kaka yangu kwangu?” Imam (a.s.) alilia sana na akasema: “Oh, Zainab dada yangu! Viungo vya mwili wa kaka yako vimechanwa kwa kiasi am-bacho mimi sikuweza kuvisogeza.” Kwa kuyasikia haya Zainab ali-omboleza, “Ewe kaka yangu! Oh, Abbas! Ole kwa kukosa wasaidizi! Ole kwa maangamizi baada yako!” Imam (a.s.) akaguta kwa sauti, “Ah nimekosa kaka na kuvunjika kwa mgongo wangu!” Halafu aka-soma beti zifuatazo za maombolezo:

“Kaka yangu! Nuru ya jicho langu! Kaka yangu kutokana na wazazi wangu!

Wewe ulikuwa kwangu ni nguzo ya usalama.

“Ewe mwezi ung’arao! Wewe ulikuwa ni msaada kwangu Katika kila balaa, katika mazingira yaliyonyooka.

“Maisha kwetu sisi hayana maana baada yako tutakutana na kukusanya kesho mbele ya Allah

“Kwa hakika malalamiko yangu ni kwa ajili ya Allah na pia ustahimilivu katika kiu yangu na misiba.

(Ma’ali al-Sibtayn)

MAELEZO MENGINE JUU YA KIFO CHA KISHAHIDI CHA ABBAS

Ufuatao ni mukhtasari wa maelezo ya Mulla Habibullah Kashani juu ya Shahada ya Abbas ibn Ali (a.s.). Imam al-Husein (a.s.) ali-posikia sauti ya huzuni ya Abbas, yeye alipanda farasi wake aitwaye Dhu Janah na akakimbilia kule mtoni. Alipambana na maadui njiani mwake humo. Aliwashambulia vikali na huku wakikimbia yeye aliiita kwa sauti: “Mnakimbilia wapi? Mmemuua ndugu yangu na kuu-vunja mgongo wangu.” Imam (a.s.) aliwauwa maadui mia nane, lakin i wakati wote alikuwa akimwita Abbas; “Oh, Abbas! uko wapi?”

Ghafla Dhu Janah akasimama na akakataa kusonga mbele. Imam (a.s.) akatupa jicho aridhini na akaona ile mikono ya Abbas iliyokatwa. Alishuka chini, akaichukua ile mikono ya Abbas huku akitokwa na machozi akaifuta kwenye uso wake huku akisema: “Ole kwa huzuni ya kifo cha ndugu yangu!” Alimpanda Dhu Janah na tena farasi huyo akasita kuondoka. Safari hii Imam (a.s.) alipoangalia chini ardhini aliona ule mfuko wa ngozi uliochanika. Imam (a.s.) alilia kwa sauti na akaendelea kuelekea kule mtoni. Huko aliuona ule mwili wa ndugu yake uliokatwakatwa. Bila kukusudia alijikuta akitoa kilio cha huzuni ambacho kilitikisa Mbingu na ardhi alipokuwa akisema: “Sasa mgongo wangu umevunjika; njia na uwezo wangu vimeteketea.”

Imam (a.s.) alikitwaa kichwa cha Abbas na akakileta kwenye kifua chake na akalia kwa sauti kilio kisichodhibitika. Huzuni yake ilikuwa kubwa kiasi kwamba wale maadui walioshuhudia wenyewe walianza kulia katika kadhia hiyo. Imam (a.s.) alimwambia Abbas: “Ewe ndugu yangu! Mwenyezi Munguakujaalie malipo bora ya thawabu! Kwa hakika umejitatidi kimadhubuti kabisa katika njia ya Mwenyezi Mungu.”

(Tadhkirat al-Shuhadaa)

BAADHI YA MAELEZO YA BAADAYE YA HUZUNI NA UVUTIWAJI JUU YA ABBAS IBN ALI (A.S.)

Ummuu Banin, mama yake, katika kusikia taarifa za Shahada ya Abbas, alizungumza naye kwa beti hizi zifuatazo:

“Upanga wako ungekuwa mikononi mwako
Hakuna yejote ambaye angethubutu kusogea karibu yako.”

(Fursan al-Hayyan)

Kuna riwaya kwamba wakati ngawira za kivita ambazo zilichukuliwa kutoka kwenye familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) zilipowasilishwa kwa Yazid huko Syria, mionganini mwa hiso ilikuwepo bendera kubwa. Yazid pamoja na wale waliokuwa wamemzunguka yeye ndani ya baraza hilo waliona kwamba kila inchi ya bendera hiyo imekatwa matobo isipokuwa pale tu kwenye kishikio. Yazid aliulizia kuhusu mbebaji wa bendera hiyo na akaambiwa kwamba ilikuwa kwenye umiliki wa Abbas ibn Ali. Yazid kwa mshangao wenye hofu ndani yake juu ya muonekano wa bendera hiyo, alisimama na kukaa na kurudia kufanya hivyo. Halafu akasema: “Hebu angalia bendera hii. Hakuna sehemu hata moja iliyoachwa kutokana na mikato ya mikuni na panga isipokuwa pale mahali ilipokuwa imeshikiliwa.” Kisha akaendelea, “Oh, Abbas! Ewe bezo unayetukuzwa. Hivi ndivyo uaminifu na utii wa kaka mmoja kwa kaka yake unavyoonyeshwa.”

(Din wa Tammudun)

Wakati Imam wa Nne Ali ibn al-Husein (a.s.) alipomuona Ubaydullah mtoto wa Abbas ibn Ali (a.s.) hapo Madina, yeye alimkumbuka baba yake na akalia sana asiweze kujizua. Alisema: “Hakuna msiba uliomfika Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) ambao ni mkubwa kuliko kifo cha Hamzah, yule simba wa Mwenyezi Mungu katika vita vya Uhud mpaka pale balaa kubwa lilipomshukia kwa kifo cha Ja’far al-Tayyar katika vita vya Mu’tah. Lakini msiba ulikuwa mkubwa kabisa kupita yote ni ile siku ya kuuawa kishahidi kwa Imam Husein (a.s.). Alikuwa amezungukwa na watu thelathini waliokuwa wakidhania wamo mionganoni mwa Ummah wa Kiislam.” Kisha akaendelea kusema: “Kwa hakika Abbas anayo hadhi ya juu kabisa mbele ya Allah, hadhi ambayo mashahidi wote watatamani kuipata hiyo Siku ya Kiyama.” Halafu akaongeza kusema: “Mwenyezi Mungu amjaze rehema ami yangu Abbas ambaye aliyatoa muhanga maisha yake kwa ajili ya al-Husein (a.s.) kwa namna ambayo maadui waliikata mikono yake yote. Mwenyezi Mungu amerudishia mahali pa mikono yake mbawa mbili kama alivyofanya kwa Ja’far ibn Abi Talib (rehema na amani ziwe juu yao wote). Inakupasa utambue kwamba Abbas anapita kwenye masafa ya Peponi pamoja na Malaika.”

(Muntakhab al-Tawarikh)

MAAMKIZI (SALAMU) YA IMAM WA KUMI NA MBILI KWA ABBAS IBN ALI (A.S.)

“Amani iwe juu ya Abu Fadhl’Abbas, mwana wa Amirul-Mu’mimin!

Amani iwe kwake yule ambaye alitoa uhai wake kwa ajili ya kaka yake!

Amani iwe juu yake yule ambaye aliifanya dunia kama njia ya Akhera!

Yule ambaye alijitoa muhanga kwa ajili ya kaka yake!

Yule ambaye alimlinda na kujitahidi kupata maji kwa ajili ya nduguye!

Mwenyezi Mungu awalaani waliomuua Abbas, Yaziid ibn Ruqad na Hakiim ibn Tufayl.”

(Biharul-Anwar)

SABABU ZAIDI NA MAELEZO JUU YA HUZUNI KUBWA JUU YA ABBAS IBN ALI (A.S.)

Ili kuendelea kufahamu zaidi upeo kamili wa huzuni juu ya kifo cha Abbas ibn Ali (amani iwe juu yake) tunaelezea haya yafuatayo:

1. Wakati Luqman mwenye hekima alipokuwa akirejea kutoka kwenye safari moja ndefu, alikutana na mtumishi wake na aka-muuliza: “ Yuko wapi baba yangu?” Yule mtumishi akamjibu: “Baba yako amefariki.” Luqman akasema. “Sasa nitakuwa msimamizi wa mambo yangu. Nini kimetokea kwa mke wangu?” Mtumishi yule akajibu: “Amefariki.” Luqman akasema: “Nitaoa tena. Nini kimemtokea dada yangu?” Mtumishi akamjibu: “Naye amefariki.” Luqman akasema: “Hadhi yangu imepata ulinzi. Nini kimetokea kwa kaka yangu?” Mtumishi akamjibu: “Yeye amefariki pia.” Luqman akatamka kusema: “Sasa mgongo wangu umevunjika.”

Hii inaonyesha kwamba maangamizi yaliyompata Imam Husein (a.s.) kwa kifo cha Abbas yaliikuwa ni kama vile alisema, “Sasa mgongo wangu umevunjika.”

2. Katika zama za Allamah Bahr al-‘Ulum, sehemu ya kaburi la Abbas ilikuwa imeharibika. Bahr al-‘Ulum alikuwa atembelee kaburi hilo pamoja na mjenzi na kuhakikisha urekebishaji wa kaburi hilo. Waliingia ndani ya Sardab na yule mjenzi akaangalia ule ukubwa wa kaburi hilo. Alipoona lilikuwa ni dogo ku-liko vile alivyokuwa ametarajia, ye ye aksauliza: “Nimesikia kwamba Abbas alikuwa mrefu kiasi kwamba miguu yake ili-kuwa inagusa chini akiwa amekaa juu ya farasi wake. Kwa mu-jibu wa hilo, kaburi lake linapaswa kuwa kubwa zaidi kuliko hivi liliyvo hapa. Je, tulikuwa tukisikia maelezo ya uongo juu ya kimo chake ama kuna sababu nyingine juu ya kaburi hili dogo?” Badala ya kumjibu, Allamah aliegemeza kichwa chake ukutani na akaanza kulia kwa sauti kubwa. Alilia sana kiasi kwamba yule mjenzi alipatwa na wasiwasi, aliguswa sana na aksauliza: “Kwa nini ulie kiasi kama hiki? Je, nimesema jam-bo baya?” Allamah akamjibu: “Ulichokisikia ni kweli. Abbas alikuwa mrefu sana, lakini swali lako limenikumbusha msiba wake wa kuvunja moyo. Alikatwa mara nyingi sana kwa panga na kuchomwa mikuki na mishale kiasi kwamba mwili wake uli-chanwa na kuwa vipande vipande.”
3. Kila askari anayechomwa na mshale huuondoa au anaweza ku-uondoa kutoka mwilini mwake kwa mikono yake. Abbas alika-biliwa na warusha mishale elfu nne na wote wakamfanya ye ye peke yake ndio shabaha ya mishale yao wakati mikono yake ikiwa imelala hapo chini baada ya kukatwa.
4. Kila mpanda kipando, katika kushuka kutoka kwenye farasi wake huweka mkono mmoja kwenye tandiko lake na mwingine

hatamu. Vipi mtu asiyekuwa na mkono hata mmoja atashuka kutoka kwenye farasi wake?

5. Kila mpiganaji anayeanguka kutoka kwenye farasi wake hunyoosha mikono yake kuelekea ardhini kuzuia kichwa na mwili wake kujibwaga ardhini. Ni kwa maumivu kiasi gani ambavyo Abbas lazima awe ameshuka nayo kutoka kwenye farasi wake?
6. Abbas alikuwa amegubikwa na mishale wakati alipokuwa anaanguka kutoka kwenye farasi wake. Katika muanguko wake mishale hiyo ilizidi kujipenyeza kwenye mwili wake uliotukuka.

(Ma'ali al-Sibtayn)

7. Sayyid Abd al-Razzaq, mwandishi wa 'Maqtal al-Husayn al-Muqarram' anaandika hivi: "Yule mwanachuoni mkubwa Sheikh Kadhim Sibti ameniambia, 'Mmoja wa wanachuoni wetu wa kuaminika alinijia na akasema: Nimetumwa kwako na Abbas. Nilimuona katika ndoto na aliniuliza ni kwa nini Sheikh Kadhiim Sibti huwa hasimulii habari za msiba wangu? Mimi nikamjibu kwamba yeye wakati wote anasimulia msiba wako. Yeye akasema, mwambie Sheikh Kadhim asimulie hivi: 'Kila anayeanguka chini ardhini hutumia mikono yake katika kumsaidia. Vipi mtu aliyekuwa hana mikono na ambaye alikuwa amegubikwa na mishale mwili mzima angeweza kutua ardhini alipokuwa anaanguka kutoka kwenye farasi wake.'"

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

8. Fadhl Darbandi anaandika katika kitabu 'Asrar al-Shahadah' hivi: "Kundi la watu wa kuaminika wamenisimulia kwamba muumini aliweza kufanya ziara za kila siku kwenye kaburi la

Imam al-Husein (a.s.) lakini akalitembelea kaburi la Abbas ibn Ali mara moja tu kwa wiki. Alimuona Bibi mwenye nuru, Bibi Fatimah (s.a.) kwenye ndoto zake, akamwamkia kwa salamu njema lakini Bibi Fatimah akageuzia uso wake upande wa pili mbali na yeze. Kwa hofu na masikitiko, yeze aliuliza: “Oh, Bibi! Baba na mama yangu wawe fidia kwa ajili yako! Kwa nini unanigeuzia mbali uso wako? Nimefanya kosa gani?” Bi. Fatimah (s.a.) akamjibu: “Kwa sababu umegeuzia mbali uso wako kwenye kumzuru mwanangu!” Yule muumini akasihi: “Lakini mimi siku zote ninalitembelea kaburi la al-Husein mwanaao (a.s.).” Kwa hili Bibi Fatimah (s.a.) akasema: “Wewe unatembelea kaburi la mwanangu Husein, ni sawa, lakini unamtembelea mwanangu Abbas mara chache sana!”

(Ma’ali al-Sibtayn)

VIFO VYA HUZUNI VYA ABDALLAH IBN HUSEIN NA ALI ASGHAR IBN HUSEIN – WATOTO WAWILI WACHANGA WA IMAM HUSEIN (A.S.)

Kwa mujibu wa mwandishi, Muhammad Ishtihadi, watoto wawili wanaonyonya wa Imam Husein (a.s.) waliuliwa mnamo Siku ya Ashura. Mmoja wao alikuwa ni Abdullah kichanga ambacho ndio kwanza kuzaliwa na mwingine ni Ali Asghar.

KUUWAWA KWA ABDALLAH IBN HUSEIN (A.S.)

Na kuhusu kifo cha Abdallah, mwandishi ananukuu al-Ziyarah al-Nihiyah ya Imam wa Kumi na Mbili:

“Amani juu yako Abdallah ibn al-Husein!

Mtoto anayenyonya, aliyechomwa na kuuliwa kwa mshale,
akafunikwa na damu.

Ambaye damu yake ilipaa na kwenda Mbinguni.

Ambaye alichinjwa akiwa mapajani mwa baba yake.

Laana ya Allah imshukie muuaji wake Hurmulah ibn Kahil
Asadi!”

(Bihar al-Anwar)

Wakati wengi wa wafuasi na wanafamilia wa Imam walipokuwa wamekwisha yatoa maisha yao, Imam aliita kwa sauti: “Yupo msaidizi atakayeihami familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)? Je, yupo yeoyote, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, atakayekuja kutunusuru?” Imam aliomba msaada wakati sauti za vilio na maomboleza za wanawake zikisikika kutoka kwenye mahema yao!

Imam (a.s.) alikwenda kwa Bibi Zainab na akaomba apewe mwanawe ili aagane naye. Imam alimbeba mtoto huyo na alipokuwa anamsogezea kwenye midomo yake ili apate kumbusu, Harmalah akachoma mshale kwenye shingo ya mtoto huyo na kumchinja kabla baba yake hajaweza kumfikisha kwenye midomo yake. Imam (a.s.) alimkabidhi mtoto kwa Bibi Zainab. Alipokuwa akiondoa mkono wake kutoka chini ya shingo ya mtoto huyo, ulikuwa tayari umejaa damu tukufu ya mtoto huyo. Imam akairusha damu hiyo kuelekea mbinguni huku akisema: “Msiba huu unastahimilika tu kwa sababu Mwenyezi Mungu anaushuhudia.” Imesimuliwa katika al-Ihtijaj kwamba Imam alikwenda kando ya mahema hayo ambako alichimba kaburi kwa kutumia ala ya upanga wake na akamzika hapo mwanawe.

(Nafas al-Mahmum)

MSIBA MKUBWA WA KIFO CHA ALI ASGHAR IBN HUSEIN (A.S.)

Inasimuliwa kwa mapana sana kwamba Ali Asghar alikuwa na umri wa miezi sita wakati alipouliwa kishahidi. Mama yake alikuwa ni Rabab binti Imru' al-Qays. Yeye huyu alikuwa pia ndiye mama yake Sakinah binti yake Imam Husein (a.s.)

Kabla ya pambano lake la mwisho na maadui, Imam Huseini (a.s.) alikwenda kwa dada yake Ummu Kulthum na akasema: "Ewe dada yangu! Chukua malezi ya uangalifu wa hali ya juu kabisa kwa mwanangu anayenyonya, Ali Asghar. Ana umri wa miezi sita tu." Kwa hili Ummuu Kulthum alijibu: "Ewe kaka yangu! mwanaao hajaonja maji kwa siku tatu mfululizo sasa. Hebu nenda kwa watu hao ukaombe maji kidogo kwa ajili yake."

Imam Husein (a.s.) alimbeba kifuani mwake mwanawewe Ali Asghar na akaelekea naye kwa maadui. Alisimama mbele ya maadui na huku akimuonyesha kwao dhahiri Ali Asghar na akasema: "Enyi watu! Mtoto huyu amefanya makosa gani kwenu? Kama mna uadui wowote ule, basi huo ni kwa ajili yangu mimi. Mmewauwa wanangu, ndugu zangu na wafuasi wangu. Mtoto huyu hawezi kupigana nanyi. Hebu mzimieni kiu yake. Hamuoni anavyoungua na kiu na anakaribia kutoa uhai wake kwayo?" Imam (a.s.) wala hakumalizia kauli yake hiyo wakati, kwa amri ya Umar ibn Sa'd, maalun Harmula alilifanya lile koo lenye kiu la Ali Asghar ndio shabaha ya mshale wake wenye ncha tatu. Hivyo shingo ya mtoto huyo ilichanwa kuanzia sikio moja hadi lingine.

(Ma 'ali al-Sibtayn)

HUZUNI YA IMAM KWA KIFO CHA ALI AS-GHAR (A.S.)

Huzuni iliyompata Imam (a.s.) kwa kifo cha Ali Asghar ilikuwa ni kubwa kiasi kwamba alilia kwa uchungu juu ya mtoto huyo ali-yekuwa kwenye mikono yake inayotetemeka. Alisema katika du'a: "Ewe Allah! kuwa hakimu kati ya watu hawa na mimi. Wao wali-tuita kwa kutukaribisha na kuahidi kutusaidia sisi. Sasa wanatuua." Alivyokuwa akilia sana Imam (a.s.) kwa ajili ya kichanga chake hi-cho, alisikia sauti kutoka mbinguni: "Ewe Husein! Muachie huyo. Yeye anaye mama anayemsubiri ndani ya hema." Sauti hii ilimli-waza Imam (a.s.) na kumuwezesha kustahimili machungu ya kifo cha Ali Asghar.

(Ma'ali al-Sibtayn)

SAKINA AKABILIANA GHAFLA NA MWILI ULIOLOANA DAMU WA ALI ASGHAR

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, wakati Ali Asghar alipokuwa aki-tapata-pata kutoka kwenye uhai kwenda kwenye kifo, akiwa amebebwa katika mikono ya Imam (a.s.), Husein ibn Tamim (laana juu yake) alimrushia Imam mshale ambao uliichana midomo yake mitakatifu na chemchem ya damu ikatofoka ikidondokea kwenye mwili wa Ali Asghar. Imam (a.s.) akitokwa na machozi alimlalamikia Mwenye-zini Mungu akisema: "Ewe Allah! Nakulalamikia kwa kile ambacho watu hawa wamenifanyia mimi, ndugu zangu, wanangu na familia yangu."

Kwa mujibu wa Abu Mikhraf, Imam (a.s.) alimbeba Ali Asghar kurudi naye kwenye mahema huku damu ikuchuruzika kutoka kwenye

shingo ya Ali Asghar juu ya kifua chake. Sakinah alimkimbia ili kumpokea kaka yake. Akauliza: “Ewe baba! Umemnywesha maji ndugu yangu?” Imam (a.s.) alilia sana akisema: “Ewe mwanangu! Mchukue ndugu yako ambaye amechinjwa kwa mshale wa adui.”

(Ma’ali al-Sibtayn)

Baada ya Shahada ya Imam (a.s.), Sakinah alitoka akikimbia kwa mfadhaiko kutoka kwenye mahema yaliyoporwa na kuchomwa moto hadi kwenye mwili wake Imam uliokuwa umekatwa kichwa. Alilia na kuanguka akiwa amezimia kifuani mwa baba yake. Imam (a.s.) alimtokea kwenye ndoto zake na akamsomea beti fulani kwa ajili ya yeye kuzifikisha kwa wale waliompenda Imam (a.s.) ambazo zilionyesha ukali wa maafa yaliyokuwa yamemkuta yeye. Zifuatazo ni beti mbili zinazoelezea mauaji ya kikatili ya Ali Asghar:

“Endapo tu katika ile siku ya Ashura wote mngeliona vile jinsi nilivyoomba maji kwa ajili ya mwanangu, lakini walikataa kuonyesha huruma juu yangu.

Badala yake walizima kiu yake kwa mshale usiotegemewa mahali pa maji

Ole kwa kuondokewa kukubwa na pia maafa hayo wameivunja misingi ya milima ya Makka.”

(Ma’ali al-Sibtayn)

KIFO KINACHOPENYA MOYONI CHA MTOTO KANDO YA MAHEMA

Imesimuliwa kwamba: Wakati Imam alipokuwa amesonga mbele dhidi ya maadui, na akawa ameanza kupigana, mtoto mmoja wa kiume, mwana wa ndugu yake Muslim ibn Aqil alitoka akikimbia kutoka kwenye mahema pamoja na wanawake wakimkimbilia nyuma yake. Kijana huyo alikuwa amevaa herein kwenye sikio lake moja iliyokuwa ikienda kutoka upande mmoja hadi mwингine na akikigeuza kichwa chake huku na huko kama anayemtafuta mtu. Katikati ya tukio hili, mmoja wa maadui aliyeitwa Hani ibn Thabit Hadhrami alimwendea mtoto huyo na akampiga kwa upanga wake. Mtoto huyo alikuwa papohapo. Tukio hilo lilikuwa moja ya majanga makubwa wakati wanawake walipokusanyika kuuzunguka mwili wa mtoto huyo, ambao kwa wakati huo ulikuwa umeloa damu. Mama yake, Shar Banuwayah, kwa matokeo ya mshtuko na huzuni ya kumshuhudia mwanae, alianguka chini na kupeteza fahamu pembedi ya mwili huo wa mwanae.

Hani ibn Thabit (laana juu yake) pia alikuwa miongoni mwa wale watu kumi ambao waliishetasheta maiti ya Imam (a.s.) uliokuwa umekatwa kichwa baada ya kupata Shahada (kuuliwa kishahidi) yake.

MSIBA WA ABDALLAH ASGHAR IBN AL-HASAN (A.S.)

Abdallah Asghar mtoto wa Imam Hasan (a.s.) alikuwa na umri wa miaka kumi na moja pale wakati alipokuwa Karbala pamoja na ami yake Imam Husein (a.s.). Imam alikuwa ametoa maagizo kwa wanawake kumlinda Abdallah dhidi ya maadui. Ule wakati ambapo

Imam (a.s.) alipokuwa amesonga mbele kwa ajili ya pambano lake la mwisho na maadui, akiwa amebakia peke yake bila wasaidizi, Abdallah pamoja na kutokuwa na uwezo kwake alitoka mbio nje ya hema na kuelekea kwa Imam (a.s.). Bibi Zainab (s.a.) alimkimbilia ili amzuie asiende kwenye uwanja wa vita. Imam naye alimuona Abdallah akimkimbilia yeye na akaita kwa sauti: “Oh, Zainab! Mkamate huyo!” Abdallah alimng’ang’ania Imam (a.s.) na akamsihi: “Kwa jina la Mola Wangu! Wallahi sitamuacha ami yangu. Mimi sirudi kwenye mahema.” Abdallah alikuwa bado yuko kwenye mikono ya ami yake akimuomba kubakia naye wakati askari mmoja wa farasi aliwaelekea akiwa amenyanyua upanga wake kwa nia ya kumpiga nao Imam (a.s.). Abdallah (Mwenyezi Mungu amrehemu kabisa) alichomoa mkono wake kukizuia kile chuma kinachokata! Ule mkono wake uliokatwa ulining’inia kwa kijipande tu cha ngozi wakati yeye akiguta: “Oh, ami yangu! Oh, baba yangu! Wameukata mkono wangu.” Imam Husein (a.s.) alimkumbatia mtoto huyo na kusema: “Ewe mtoto! Stahimili! Hivi punde utakutana na babu yako, baba yako na ami yako” Imam alikuwa hajamaliza kumliwaza kijana wakati maalun Harmalah alipopiga mshale kwenye shingo changa ya Abdallah. Mtoto huyo aligwaya. Kisha akitetemeka mikononi mwa ami yake mtu mzima aliiaga dunia.

Wakati Bibi Zainab alipoliona hili, alilia bila kuweza kujizua na kwa kikwifukwifu aliomboleza: “Ewe mtoto wa ndugu yangu! Ewe nuru ya jicho langu! Angalau basi kifo kingenichukua mimi!”

Kwa mujibu wa riwanya nyingine, wakati mkono wa Abdallah ulipokatwa, yeye alimwita mama yake, “Ewe mama! Wameukata mkono wangu!” Mama yake alikuja akikimbia na kupiga yowe, “Ewe mwanangu! Ewe tunda la jicho langu.”

(Ma’ali al-Sibtayn)

UJASIRI WA MASAHLABA WA IMAM (A.S.) KAMA UNAVYOELEZWA NA MAADUI

Askari mmoja kutoka katika jeshi la Umar bin Sa'd na ambaye alishiriki katika kuwauwa masahaba wa Imam (a.s.) mnamo siku ya Ashura alishutumiwa na watu. Akalaaniwa: "Huzuni naiwe ndio fungu lako! Wewe uliridhikaje kuwa katika kundi la wauaji wa watoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?" Kwa hili yeye alijibu: "Nyamazeni kimya! Sisi tulikabiliana na watu ambaao walikuwa kama ngamia wasiodhibitiwa. Walikuwa wakitushambulia na kutukata mapande kutokea kila upande. Kwa mikono mitupu tu wao wali-songa kukielekea kifo. Ima walikuwa wamekunywa kutoka kwenye kikombe cha mauti au walikuwa tayari kukichana kifo chenyewe vipande vipande. Kule kuwauwa kulikuwa ndio njia pekee ya kujiooa sisi wenyewe. Kama mmoja wenu yoyote angekuwepo pale, pia angefanya vivyo hivyo."

(*Sharh Nahjul-Balaghah* ya Ibn Abi al-Hadiid)

MLANGO WA SABA

MSIBA MKUBWA WA BWANA WA MASHAHIDI IMAM HUSEIN IBN ALI (A.S.)

**(NAFSI ZA WALIMWENGU ZIWE KAFARA CHINI YA
MIGUU YAKE)**

Idadi ya simulizi za msiba wa Imam, kuanzia kuaga kwake hadi kifo chake cha Shahada, kwa kweli haihesabiki. Katika vifungu vifuatavyo tatarudia kuvisimulia baadhi tu kwa njia ya kufipisha.

KUAGANA KWA MWANZO

Baada ya kifo cha Abbas ibn Ali Imam (a.s.) aliachwa peke yake bila ya wasaidizi wowote. Wanawake waliomboleza na kulia kwa upweke ule wa Imam (a.s.) vile alivyokuwa akiita:

“Kuna yeьте atakayewalinda watu wa familia ya Mtukufu Mtume? Kuna yeьте atakayekuja kutunusuru kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?”

Kisha akaanza kuwaaga wanawake na watoto na akawaomba wavumilie kwa subira ule msiba wa kifo chake ambao ulikuwa unakaribia kuwakuta. Baada ya kwisha kuagana nao, alimgeukia dada yake, Bibi Zainab (s.a.) na akasema:

“Ewe dada yangu! Niletii nguo kuu kuu, iliyochakaa ambayo hakuna mtu atakayeitamani, ambayo niweze kuvalaa chini ya nguo zangu, ili nisije nikavuliwa nguo zote nitakazokuwa nimevaa baada ya kifo changu.”

Suruali moja ndogo ililetwa kwa ajili yake ambayo aliikataa akisema kwamba nguo kama hiyo haifai kwa mtu mwenye heshima kama yeche. Ndipo akapewa shati moja refu lililochakaa. Alilichukua shati hilo na akalichana sehemu kadhaa na akalivaa chini ya nguo zake. Aliomba nguo nyinyine, ambayo pia aliichanachana na kuivalaa kama nguo ya nje. Alifanya hivi kwa kuchelea kuvuliwa nguo zote baada ya kifo chake cha Kishahidi.

(Luhuf)

KUAGANA KWA MARA YA MWISHO KWA IMAM (A.S.)

NA IMAM ALI IBN HUSEIN ZAINUL-ABIDIIN (A.S.)

Wakati Imam (a.s.) alipokuwa anaondoka alirudia rudia kutoa wito wake: “Kuna mtu yoyote atakayekuja kunisaidia na kulinusuru? Kuna yoyote atakayeitetea familia ya Mtukufu Mtume?” Wanawake walilia kwa sauti kubwa kwa upweke wake huo. Kuomboleza huko kwa wanawake kulimuamsha Imam Sajjad, Ali ibn al-Husein (a.s.) ambaye kwa sababu ya ugonjwa na homa kali alikuwa ameanguka na kuzimia. Imam Sajjad alitembea kuelekea mlangoni mwa hema kwa matatizo sana lakini akiwa amebeba upanga wake. Ummuu Kulthum

alipoona kwamba alikuwa hawezi hata kusimama sawasawa, alim-kamata na kumsihi arejee ndani ya hema. Imam Sajjad (a.s.) alijitahidi kujiweka sawa mwenyewe huku akisema: “Oh, shangazi! Hebu niachie. Ngoja nimhami baba yangu.”

Imam Husein (a.s.) akitambua nia ya Imam as-Sajjad (a.s.) alimwita Ummu Kulthum: “Ewe Ummu Kulthum, usimuachie huyo isijekuwa ardhi ikakosa kuwa na kubakia kwa kizazi cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.).”

Fadhl Darbandi anaandika ndani ya *Asrar al-Shahadah* kwamba Imam Husein alikimbilia kwa Imam as-Sajjad (amani juu yao) na akamchukua na kumrudisha ndani ya hema na huku akisema: “Ewe mwanangu, ni nini makusudio yako?”

“Ewe baba yangu! Wito wako kwa ajili ya kutaka msaada umenichana mishipa kuanzia moyoni mwangu na umenipoka amani na utulivu wa akili yangu. Ninahitaji kutoka. Napenda kutoa uhai wangu kwa ajili yako!”

“Ewe mwanangu! Wewe hauna afya njema! Jihad sio wajibu kwako na wala hairuhusiwi kwako wewe kushiriki. Wewe ndiye Hujjah, ndiye Imam kiongozi wa Shi’ah (wafuasi) wangu. Wewe ndiye baba wa Maimam wanaokuja baadaye. Ndio mlezi wa mayatima na wajane. Utapaswa kuwarudisha kwenda Madina. Ardhi (dunia) haitaweza kuwa tupu bila ya Imam, aliye Hujjah kutokana na kizazi changu.” Imam Husein alimliwaza Imam as-Sajjad (amani juu yao wote).

“Ewe baba yangu, hivi mimi niwe ninaangalia tu wakati wewe unauliwa? Natamani kama tu ningefariki kabla ya hili!” Alilalamika Imam Sajjad.

Imam (a.s.) alimkumbatia Imam as-Sajjad (a.s.) na akalia. Halafu akaagana naye kwa mara ya mwisho.

(*Ma'ali al-Sibtayn*)

Maelezo mengine juu ya kuagana kwa mara ya mwisho kwa Imam (a.s.) na Imam Sajjad yanatolewa katika *al-Dam'at al-Sakibah* kama ifuatavyo:

Imam (a.s.) alivyokuwa akiondoka akiwa peke yake, alikwenda kwenye mahema ya ndugu zake. Alichungulia ndani ya mahema hayo na akayakuta yako matupu, hayana mtu. Akaenda kwenye mahema ya watoto wa Aqil. Alivyoyakuta matupu aliendelea na akaenda kwenye mahema ya wafuasi wake waliokuwa sio Bani Hashim na akayaona nayo pia kwamba yalikuwa tupu. Alikariri mara nyngi ile du'a: "Hakuna nguvu wala uwezo ila kwa Mwenyezi Mungu, Mkuu, Mwenye nguvu."

Halafu Imam (a.s.) akaenda kwenye mahema ya wanawake na baada ya hapo alikwenda kwenye hema la Imam as-Sajjad (a.s.). Alikuta kwamba Imam Sajjad alikuwa ameanguka na kupoteza fahamu, amezimia kutokana na ukali wa ugonjwa wake na kwamba Bibi Zainab (s.a.) alikuwa anamhudumia.

Imam Sajjad (a.s.) alinyanya macho na akataka kusimama kwa heshima ya baba yake, Imam Husein (a.s.) lakini hakuweza kufanya hivyo. Imam Sajjad alimgeukia Bibi Zainab na akasema: "Naomba unisaidie ili niweze kukaa."

Bibi Zainab akakaa kwenye kitanda wakati Imam (a.s.) akiwa amemuegemea na akakaa akimwelekea Imam Husein (a.s.). Imam akamuuliza Imam as-Sajjad kuhusu hali yake ambapo ye ye alijibu: "Sifa na Utukufu uwe kwa Mwenyezi Mungu." Kisha aauliza: "Kuna habari gani kuhusu mambo yako na watu hawa?"

“Shetani ameshinda pamoja na watu hawa na wametoweshelea mbali utajo wa Mwenyezi Mungu toka nyoyoni mwao. Vita vikubwa vimetokea kati yetu na wao na mawanda ya Karbala yametapakaa damu yetu.” Alijibu Imam Husein (a.s.).

“Ni kipi kimemkuta ami yangu Abbas, ewe baba yangu?” Aliuliza Imam as-Sajjad kwa machungu makali.

Bibi Zainab aliguswa. Alimwangalia kaka yake kwa macho yaliyojawa machozi kuona kwamba atajibu vipi. Imam (a.s.) hakumpa as-Sajja taarifa za kifo cha Abbas akihofia mshtuko usije ukaidhoofisha zaidi hali yake ya maradhi.

“Oh, mwanangu! wameikata mikono ya ami yako Abbas na kisha wakamuua kwenye kingo za mto Furati.” Alisema Imam (a.s.).

Imam as-Sajjad (a.s.) baada ya kujua kuhusu kifo cha Abbas (a.s.) hakuweza kujizua kulia sana hadi akazimia. Alipokuja kupata fahamu, alianza kuulizia habari za kila sahaba wa Imam (a.s.) naye Imam akaendelea kumjibu kwamba wao wamekwisha kutoa uhai wao kwa ajili yake, mpaka Imam as-Sajjad akauliza: “Yuko wapi ndugu yangu Ali? Yuko wapi Habib Mudhahir? Wako wapi Muslim ibn Awsajah na Zuhair ibn Qayn?”

“Ewe mwanangu! tambua kwamba hakuna mwanaume aliyebakia kwetu ukiacha mimi na wewe.” Alisema Imam Husein (a.s.). Imam as-Sajjad (a.s.) alilia sana kisha akamwambia shangazi yake Bibi Zainab: “Nipatie upanga wangu na mkongojo wangu.”

“Kwa nini unaomba upanga na mkongojo wako?” Aliuliza Imam Husein (a.s.).

“Huo mkongojo kwa ajili ya kunisaidia (kusimama imara) wakati nikimtetea mtoto wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa upanga wangu, kwani maisha hayana faida baada yako wewe.” Akajibu Imam Sajjad (a.s.).

Imam Husein alimkumbatia na kumliwaza huku akisema: “Ewe mwanangu, wewe ndiye safi kabisa na mtukufu bora katika kizazi changu, wewe ndiye mlezi mahali pangu wa hawa mayatima na wajane wapweke na waliokandamizwa. Hawana mwingine zaidi yako wewe wa kuwaokoa na maadui zao. Kuwa mpole kwao na chanzo cha maliwazo kwa ajili yao.” Halafu akaita; “Oh Zainab! Oh Kulthum! Oh Sakinah! Oh Ruqayyah! Oh Fatimah! Sikieni maneno yangu na eleweni kwamba huyu mwanangu (akionyesha kidole chake kwa Imam Sajjad) atachukua nafasi yangu. Yeye ndiye Imam baada yangu ambaye utii kwake ni wajibu.”

Maneno yake ya mwisho kwa Imam as-Sajjad yalikuwa haya:

“Ewe mwanangu! fikisha salamu zangu kwa Shi’ah wangu na waambie kwamba baba yako alikufa akiwa peke yake katika nchi ya ugenini, hivyo muombolezeeni kwani aliiaga dunia hii akiwa Shahidi Mfiadini. Kwa hiyo mlilieni.”

(*Ma’ali al-Sibtayn*)

MAJONZI YA KUAGA KWA MARA YA MWISHO KWA IMAM (A.S.)

Inaweza kuelezwa kwamba kule kuaga kwa mara ya mwisho kwa Imam (a.s.) kulikuwa ndio msiba mkubwa kabisa uliowaangukia familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika ile siku ya Ashura kwa sababu balaa hilo lilichana nyoyo zao na kuwaacha bila matumaini.

Imeelezwa kwamba mwanachuoni mmoja kwa jina la Mirza Yahya Abhari amesimulia kwamba:

“Nilikwenda kufanya ziyarah ya Imam Husein (a.s.) mnamo masiku ya Arafah. Kwenye ule usiku wa Idd al-Udh’ha nilikwenda kwenye nyumba yangu huko Karbala na nikalala humo. Katika ndoto nilimuona mtu ambaye aliniambia kwamba Allamah Majlisi (Muhammad Baqir al-Majlisi) alikuwa anatoa hotuba kwenye uwanja wa lile kaburi tukufu. Nikamuuliza ni wapi katika uwanja huo? Naye akanionyesha. Nilikwenda mahali hapo na nikakuta msikiti mkubwa ambamo ndani yake mlikuwa na mkusanyiko wa takriban wanachuoni mia tano. Nikamuona al-Baqir Majlisi amekaa juu ya mimbari akiwahutubia wanachuoni hao. Alipomaliza kutoa hotuba yake aliwaasa, kisha alipokuwa karibu na kusimulia msiba wa Karbala mtu mmoja alitokeza kutoka kwenye moja ya vyumba ndani ya uwanja huo na akaingia msikitini humo. Alimtazama Allamah Majlisi na akasema: “Zahra (s.a.) anakuomba usimulie ule msiba wa kuaga kwa mara ya mwisho kwa Imam Husein (a.s.).” Allamah aliusimulia msiba huo huku mkusanyiko ule wa wanachuoni ukiangua vilio vya machozi. Mpaka leo hii sijawahi kusikia msiba kama ule wala kushuhudia huzuni kama ile.

(Tadhkirat al-Shahada)

Imam Husein (a.s.) akatazama pale mahali alipokuwa ameikusanya miili ya wafuasi wake na akaona watu ishirini na mbili kutoka miiongoni mwa wale masahaba waliokuwa sio Bani Hashim, na watu kumi na nane wa familia yake mwenyewe. Alipokuwa ameama kuingia katika pambano lake la mwisho na maadui, Imam (a.s.) aliita:

“Ewe Sakinah! Ewe Fatimah! Ewe Zainab! Ewe Ummu Kulthum amani iwe juu yenu kutoka kwangu. Huu ni mkusanyiko wa mwisho. Wakati wenu wa majonzi makubwa na huzuni umewadiah sasa.” – Imam (a.s.) alilia sana wakati alipowatachia amani.

“Mwenyezi Mungu Mwenye huruma asikufanye ulie! Kwa nini unatokwa na machozi, Ewe kaka yangu? Aliuliza Bibi Zainab (s.a.).

“Kwa nini mimi nisilie wakati ambapo baada ya muda mfupi tu mtasukumizwa mionganoni mwa maadui? Alijibu Imam aliyejawa na machozi.

Maombolezo na vilio viliibuka kutoka kwa wanawake hao wakati walipomsikia Imam (a.s.) akiwaaga: “Kwaherini! Kwaherini! Tunatengana! Ni kutengana!”

KUAGANA KUNAKOVUNJA MOYO KWA IMAM NA BINTIYE KIPENZI SAKINAH (AM- ANI IWE JUU YAO)

Wakati alipokuwa anataka kuondoka, Sakinah alisimama kwenye njia yake na akasema: “Ewe baba yangu! Umejitolea kwenye mauti? Ni nani nitakayemtegemea mimi?”

“Ewe Sakinah! Vipi mtu asiye na msaidizi asijitolee kufa? Lakini tambua, ewe Sakinah kwamba huruma na msaada wa Mwenyezi Mungu utakuwa pamoja nawe katika ulimwengu huu na ule ujao wa Akhera. Stahimili kwa subira na usilalamikie amri ya Mwenyezi Mungu. Duniani humu ni safarini tu na Akhera ndio makazi ya kudumu.” Imam (a.s.) alimwambia Sakinah.

“Ewe baba yangu! Kwa hali hiyo basi nirudishe Madina.” Sakinah aliomba na kusihi.

“Kama kichuguu cha mchanga kitaachwa basi kitabakia mahali pake (ikimaanisha kwamba maadui hawatamuacha huru) ndio majibu aliyotoa Imam (a.s.). Sakinah alilia sana kwa kuyasikia haya. Imam (a.s.) alimvuta na kumkumbatia kwenye kufua chake na kumfuta machozi huku akisoma beti:

“Oh Sakinah, ndefu itakuwa huzuni yako juu yangu baada ya kifo changu

Usiuchome moyo wangu kwa machozi yako katika kusikitika madhali bado kuna uhai katika mwili wangu.

“Baada ya kuuawa kwangu, wewe ndie unayestahiki zaidi kuja kwenye mwili wangu na kulia, ewe mbora wa wanawake.”

(Nafas al-Mahmum)

MTOTO MWENYE KIU ANAMKIMBILIA IMAM (AMANI IWE JUU YAO)

Hilal ibn Nafii' anasimulia:

“Nilikuwa nimesimama katikati ya safu za maadui wakati Imam alipojitokeza kwenye safari yake ya mwisho kwenye medani ya vita. Niliona msichana mdogo wa umri wa miaka mitatu ama minne, miguu yake ikitetemeka, akikimbia polepole nyuma ya Imam. Alikamata kwenye mwishio wa joho lake na akalivuta. Imam alipogeuka kuangalia nyuma akaongea kwa sauti laini: “Oh, baba yangu, hebu niangalie, mimi nina kiu.”

“Maombi ya msichana huyo yalikuwa kama chumvi inayotiwa kwenye majeraha ya Imam. Machozi yalitiririka kutoka kwenye macho ya Imam alipokuwa akisema: “Oh, mwanangu, Mwenyezi Mungu aitulize kiu yako kwani Yeye ndiye mlezi.”

“Niliuliza mtoto huyu ni nani na ana uhusiano gani na Imam. Nilifahamishwa kwamba yeye alikuwa ni Ruqayyah, binti wa miaka mitatu wa Imam.”

(*Anwar al-Shahadah*)

KUAGANA NA BIBI ZAINAB (A.S.)

Imam (a.s.) aliwaliwaza wanawake na akawaasa kustahimili kwa subira majonzi watakayokuwa wakabilane nayo kutoka kwa maadui zao. Alimuomba Mwenyezi Mungu swt. awaokoe kutoka kwenye mikono ya maadui na awaadhibu maadui zao kwa namna nyingi za adhabu. Alimuomba Mwenyezi Mungu awajaalie na malipo yasiyo na hesabu kwa mitihani na majanga ambayo yalikuwa yawaangukie. Zainab (s.a.) wakati wa maombi haya aliangua machozi. Imam (a.s.) alimkuliza akisema: “Kuwa na subira, ewe binti ya Murtadha, kwani muda wa kulia utakuwa mrefu sana.”

Imam (a.s.) alipokuwa anatoka nje ya hema kuelekea kwenye uwanja wa vita, Bibi Zainab alimuangukia miguuni kwake akisema: “Taratibu ewe kaka yangu. Subiri kidogo nipate kukuangalia tena na kukuaga, kuagana na yule ambaye sitamuona tena kamwe.”

Bibi Zainab (s.a.) alikuwa hambanduki Imam (a.s.). Alianza kumbusu mikono na miguu yake. Wanawake waliobakia walitoka nje ya hema na kumzunguka Imam (a.s.) na kuanza kubusu mikono na miguu yake. Imam aliwaliwaza na kuwaomba warejee kwenye

mahema. Kisha akamuomba Bibi Zainab kubakia pamoja naye. Aliweka mkono wake mtukufu kwenye kifua chake na kumliwaza juu ya wasiwasi alipokuwa akisema:

“Wale wanaokuwa na subira hupata malipo makubwa kutoka kwa Mola Wao. Ewe dada yangu! Yastahimilie haya kwa subira na uvumilivu.” Kwa maneno haya Bibi Zainab (s.a.) alihisi ahuweni kidogo aliposema:

“Ewe mwana wa mama yangu! Kuwa na uhakika kwamba utanikuta mimi kama unavyopenda.” (yaani kuwa mwenye subira).

KUKUMBUKA WOSIA WA MWISHO WA BIBI FATIMAH (A.S.)

Kwa mujibu wa baadhi ya riwaya, wakati Imam (a.s.) alipotembea hatua chache kuelekea kwenye farasi wake, Bibi Zainab (s.a.) alitoka nje ya hema na kuita:

“Ewe kaka yangu! Hebu subiri kidogo ili niweze kutimiza maombi ya mwisho ya mama yetu.”

“Ni maombi gani hayo? Akauliza Imam (a.s.) huku akitulia kidogo.

“Mama alitoa wasia wake kwangu na akasema, wakati utakapokuwa unamtoa yule nuru ya macho yangu kwa ajili ya pambano lake la mwisho, basi umbusu kwenye shingo yake kwa niaba yangu.” Alisema Bibi Zainab (s.a.). Kisha akambusu shingo yake halafu akarejea kwenye mahema.

(Tadhkirat al-Shahada)

Imam (a.s.) alipanda kwenye farasi wake, na alipokuwa anamzia chonjo ili aondoke, sauti laini iliita kutoka nyuma yake: “Ewe baba!

Hebu tulia kidogo na mimi nina ombi langu la mwisho.” Imam alivutwa ugwe wa hatamu za farasi alipokuwa akitazama nyuma ya bega lake na akamuona Sakinah akimkimbilia. Alikwenda mpaka pale alipokuwa na akashika hatamu za farasi yule na akasema:

“Ewe baba! Shuka kwenye farasi wako na unibebe kwenye mapaja yako mara moja ya mwisho na unipapase kichwani mwangu kama ambavyo ungefanya kwa yatima.” Imam (a.s.) alishuka, akaketi karibu na Sakinah na akampapasa kwa huruma sana na kumfuta machozi yaliyotoka kwenye macho yake. Kisha akamliwaza na akamwambia arejee kwenye mahema.

(*Tadhkirat al-Shahada*)

TUKIO LA KUTISHA WAKATI WA KUAGANA KWA MARA YA MWISHO

Imam (a.s.) alipokuwa anaagana na kuwaliwaza wanawake, Umar ibn Sa'd aliwaelekeza askari wake kumshambulia Imam akisema: “Mshambulieni wakati akiwa ameshughulishwa na kuagana na familia yake, kwani Wallahi, kama ataachiwa amalize atapasua kati-kati ya safu zenu.”

Wakati huu Imam (a.s.) alikuwa yuko nje ya mahema na wanawake walikuwa wamemzunguka. Askari hao walimfanya Imam (a.s.) kuwa ndio shabaha ya mishale yao kutoka kila upande. Mishale hiyo ilirushwa kumlenga Imam (a.s.) ambapo mingi iliwichoma wanawake hao na kwenye mahema. Wanawake hao wakiwa wametishika kwa hofu walirejea kwenye mahema na wakawa wanamuangalia Imam kuona ni nini atakachofanya. Imam (a.s.) kama simba aliyejeruhiwa aliingia kwenye safu za maadui na akawaangusha chini ardhini kila yule aliyeingia kwenye anga

zake. Kifua na shingo ya Imam (a.s.) ilikuwa imechomwa na idadi isiyofahamika ya mishale iliyorushwa kwake katika shambulio hilo. Imam (a.s.) aliing'oa mishale hiyo pale aliporejea kwenye mahema na akakariri kusoma:

“Hakuna nguvu wala uwezo ila kwa Mwenyezi Mungu.”

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

Vilevile Imam (a.s.) wakati alipokuwa anapanda kwenye farasi wake kwa mara ya mwisho, wanawake na watoto walikuwa wanaomboleza kwa sauti na kuanguka miguuni kwake wakiwa hawana uwezo wa kuhimili kujitenga kwake na wao. Imam (a.s.) alimgeukia dada yake Zainab na akasema: “Ewe Zainab, hebu watulize hawa.”

(Muthir al-Ahzan)

UCHANGAMFU MKUBWA NA HAMASA YA IMAM (A.S.)

Hata kama nyakati zingine kutokana na matatizo aliyoyapata Imam (a.s.) alitokwa na machozi na nyakati nyingine alilia kwa sauti, machozi na huzuni yake vilikuwa ni kwa ajili ya mapenzi na huruma kwa wafuasi wake na sio kupitia kutoridhika na amri ya Mwenyezi Mungu aliye Mkuu, wala udhaifu wala uchovu. Dhamiri, nguvu na uamuzi wa Imam (a.s.) wa kupigana na maadui na kupambana na uongo mpaka alipotoa pumzi zake za mwisho. Mpaka tone lake la damu tukufu linatumika, ni dhahiri kwamba kutokana na namna ambavyo amepigana dhidi yao, bila kuogopeshwa ama na idadi yao kubwa wala na shauku yao ya kuwateka wanawake wa kambi yake

ambako kungetokea baada ya kufa Shahidi kwake. Inaweza tena kuonekana wazi kabisa ile dhamira kubwa kabisa ya Imam (a.s.) kutoka kwenye hotuba zake na kauli kwa maadui katika matukio yote machungu ya kifo chake cha Kishahidi.

Katika maelezo yafuatayo, mifano michache itatajwa kuonyesha ule morali mkubwa aliokuwa nao Imam mtukufu (a.s.): Baada ya swala ya alfajiri katika ile siku ya Ashura, Imam (a.s.) aliwageukia wafuasi wake na baada ya kumtukuza na kumshukuru Mwenyezi Mungu alisema: “Hakika Mwenyezi Mungu ameruhusu vifo vyenu na changu katika siku hii. Himilini kwa subira na ustahimilivu vita hivi.”

(Ithbat al-Wasiyyah)

Mnamo ile siku ya Ashura, wakati Imam (a.s.) na wafuasi wake waaminifu walipokuwa wamezingirwa, na kifo kilielekea kuwa karibu mno, ye ye (amani iwe juu yake) pamoja na baadhi ya watifi wake wa karibu kabisa walipatwa na hali ya bidii mpya na nguvu na walionekana kuridhika zaidi. Nyuso zao ziling’ara. Wafuasi wake wengine, ambao kutokana na hofu ya kifo walifadhaika kwa kile walichokishuhudia, waliona utulivu kwenye uso wa Imam (a.s.) na wakasemezana wenyewe: “Hebu muangalieni Imam, uso wake hauonyeshi dalili yoyote ya hofu ya kifo.” Aliposikia haya, Imam (a.s.) alisema: “Stahimilini, enyi watoto wa watu watukufu, kwani kifo ni kitu gani mbali na kuwa daraja ya kukuvusheni kutoka kwenye majanga na unyonge kwenda kwenye mabustani makubwa na neema za milele. Ni nani kati yenu ambaye asingependa kutoka gerezani na kuhamia kwenye kasri, wakati maadui zenu wanatoka kwenye gereza kwenda kwenye adhabu kubwa? Kwa hakika baba yangu amesimulia kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba dunia ni gereza kwa muumini na ni Pepo kwa makafiri na kifo ndio daraja

kwa ajili yao kwenda kwenye mabustani na kwa makafiri kwenda Jahannam. Mimi sijawahi kudanganya na wala sijadanganywa.”

(*Ithbat al-Wasiyyah*)

Humayd ibn Muslim anasimulia kwamba alimuona Imam (a.s.) akiwa peke yake huku amezingirwa na maadui huku akiyakwepa mashambulizi yao. “Wallahi sijawahi kuona mtu ambaye anavamiwa mara kwa mara na maadui zake, ambaye wanawe na wafuasi wake wameuawa na ambaye anashambuliwa kutoka kila upande na akawa anapigana kwa nguvu kama hizo. Nilimuona akiwa anashambuliwa na wale walioko juu ya farasi na wanaotembea kwa miguu na bado bila ya woga aliweza kusonga mbele dhidi yao kwa namna ambayo iliwafanya maadui hao kukimbia kama kundi la mbwa mwitu lingekimbia na kutawanyika kutoka kwa simba mwenye hasira kali.

(*Kitab al-Irshad*)

Hilal ibn Nafii’, kamanda mmoja kutoka kwenye jeshi la maadui anasimulia kwamba wakati Imam alipoanguka chini huku amegubikwa na mishale na muda mfupi kabla ya kifo chake: “Wallahi sijaona mtu aliyeuawa ambaye ndevu zake zimefunikwa na damu yake kwa kupendeza mno kama yeye, wala uso unaong’ara kama wake. Uzuri wa kupendeza wa hali ya muonekano wake na wangavu wa uso wake ulinitoa kwenye wazo la kumuua yeye.”

(*A’yan al-Shi’ah*)

Imam (a.s.) anazungumzishwa kama ifuatavyo katika *Ziyarat Qa’imiyah*: “Na walivyokukuta huna woga, madhubuti katika nia yako ya kupambana, waliamua kukuwa kwa udanganyifu.”

(*Tadhkirat al-Shahada*)

Maelezo ya mapambano ya Imam (a.s.) na maadui ni: “Alishambulia jeshi la askari thelathini alfu akiwa peke yake, na walimkimbia na kutawanyika katika mawanda ya Karbala kama wanavyotawanyika nondo. Imam (a.s.) amekuwa akirejea kwenye sehemu yake kwenye mahema baada ya maadui kukimbia mashambulizi yake na akisoma:

“Hakuna nguvu wala uwezo ila kwa Mwenyezi Mungu, Mkuu, Mwenye nguvu.”

(*A'yan al-Shi'ah*)

IMAM ANAJITAMBULISHA NA KUTOA HOJA YA KUVUNJA NGUVU KWA ADUI

Imam (a.s.) wakati fulani, wakati wa matukio ya siku ile ya Ashura alikuja na akasimama mbele ya maadui na akiwa ameegemea kwenye upanga wake akasema:

“Ninawasihi sana kwa jina la Allah, ninyi mnajua mimi ni nani?”

Askari mmoja akamjibu: “Wewe ni mtoto wa Mtukufu Mtume wa Allah!”

Imam: “Wallahi, je mnajua kwamba Ali ibn Abi Talib ndiye baba yangu?”

Adui: “Ndio, sisi tunalijua hilo.”

Imam: “Wallahi, je mnatambua kwamba Khadija bint al-Khuwaylid, mwanamke wa kwanza kuingia katika Uislam ndiye bibi yangu mzaa mama?”

Adui: “Ndio, tunatambua.”

Imam: “Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, je mnatambua kwamba Ja’far, yule ambaye anaruka pamoja na Malaika wa Peponi ni ami yangu?”

Adui: “Ndio tunatambua!”

Imam: “Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, je mnatambua kwamba upanga huu uliofungwa kiunoni mwangu ni upanga wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?”

Adui: “Ndio tunatambua!”

Imam: “Kwa jina la Allah, je mnatambua kwamba kilemba nilichovaa kichwani mwangu ni kilemba cha Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?”

Adui: “Ndio tunatambua!”

Imam: “Ninakuulizeni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kama mnatambua kwamba Ali ibn Abi Talib, baba yangu mimi, alikuwa ndiye Muislam wa kwanza. Mwenye elimu zaidi ya masahaba wote wa Mtukufu Mtume na mvumilivu wao zaidi katika mitihani na taabu na kwamba alikuwa ni bwana wa wanaume wote na wanawake wote?”

Adui: “Ndio tunalitambua hilo!”

Imam: “Basi ni vipi mnahalalisha kuniwa mimi wakati mnajua kwamba baba yangu anashikilia haudhi ya Kawthar? Yeye atampa au kumkatalia kinywaji yejote yule amtakaye. Bendera siku hiyo itakuwa mikononi mwake.”

Adui: “Sisi tunatambua yote hayo na bado hatutaacha kukuwa wewe bila ya kupata hata tone la maji.” Hilo ndio jibu la kikaidi kabisa lililotoka kwa maadui hao.

(*Nasikh al-Tawarikh*)

Imesimuliwa pia kwamba yeye, amani iwe juu yake, aliwageukia maadui na kuwahutubia kama ifuatavyo:

“Tambueni, enyi watu, kwamba dunia hii ni ya mpito na watu wataondolewa kwenye dunia hii na kupelekwa kwenye makazi mengine. Mnazitambua sheria za Kiislam na mmeisoma vizuri Qur’ani Tukufu. Mnatambua kwamba Muhammad, Mtume wa Mwenyezi Mungu atakuja kuwafikisheni kwenye kuhesabiwa kuhusu matendo yenu na bado kidhalimu kabisa mnatafuta kumuua mwanawе! Enyi watu! Utazameni Mto Furati unavyomeremeta. Jinsi mawimbi yake yanayofoka yanavyoonekana kuwa matumbo ya samaki. Wayahudi, Wakristo, majibwa na maguruwe yanakunywa kutoka mto huo wakati ambapo familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) inakufa kwa kiu!”

KUVITAZAMA VITA VYA MWISHO VYA IMAM (A.S.)

Imam (a.s.) alilingia na farasi wake kwenye uwanja wa mapambano na kutaka kupambana na wanaolingana naye. Mmoja baada ya mwingine maadui walitoka kupambana naye, lakini haikumchukua muda Imam (a.s.) kuwauwa na kuwapeleka kwenye mashimo ya Jahannam. Imam (a.s.) aliwauwa maadui wengi na kisha akaanzi-sha mapambano katika safu za upande wa kulia wa maadui huku akighani:

“Kifo kina thamani sana kwangu kuliko fedheha na fedheha ya dunia hii ni ya thamani zaidi kuliko kuingia Jahannam “Na katika hali yoyote ile Mwenyezi Mungu ndio kimbilio langu Mimi ni Husein ibn Ali.

“Nimeapa kutogeuzia mgongo kwa maadui,

Nitailinda familia ya baba yangu.

“Nitaendelea na dini ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)

(*A'yan al-Shi'ah*)

Licha ya kiu yake, joto kali la jangwani linalounguza, hasara ya kuondokewa na wafuasi wake, matazamio ya kutekwa kwa wanawake wa kambi yake na ile idadi kubwa mno ya maadui, bado Imam (a.s.) alionyesha uhodari na ushujaa mkubwa kiasi kwamba wale wapiganaji maarufu wa dunia wanasimama huku wameinamisha vichwa vyao kwa heshima juu yake.

IMAM KWENYE KINGO ZA MTO FURATI

Imam (a.s.) katika mapambano yake marefu, alizidiwa na kiu nzi-to. Alimpanda farasi wake na akaelekea kwenye mto Furati. Imam alishambulia lile jeshi la watu elfu nne chini ya ukamanda wa Umar ibn Hajjaj na akawafukuza kutoka hapo kingoni. Aliingia mtoni humo pamoja na farasi wake kisha akamgeukia farasi wake wakati alipokuwa akishuka na akasema: “Wewe unashambuliwa na kiu na mimi nina kiu. Mimi sitakunywa maji mpaka wewe uwe umekunywa.”

Farasi huyo akionyesha ishara ya kumuelewa Imam (a.s.) alinyanya kichwa chake na akakataa kunywa maji. Imam (a.s.) alinyoosha mkono wake na akachota kiasi cha maji na alipokuwa akiyanyanya kuelekea kinywani kwake, askari mmoja alipiga ukelele akisema: “Ewe Aba Abdillah! utakunywa maji wakati mahema yako yanaporwa huko?”

Imam (a.s.) aliyamwaga maji hayo na akarejea haraka sana kwenye mahema na akayakuta kwamba hayakushambuliwa hata kidogo. Alitambua kwamba zilikuwa ni njama za maadui za kumzuia yeye kunywa maji.

(Nafas al-Mahmum)

MAPIGANO YA MTU MMOJA MMOJA

Kwa mujibu wa baadhi ya riwaya, Imam (a.s.) alimkabili Umar ibn Sa'd na akaomba moja kati ya mambo haya kutoka kwake:

1. Kumruhusu yeye (a.s.) na watu wa familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kurejea Madina.
2. Kumruhusu kunywa maji kwani ini lake lilikuwa limechanwa na kiu.
3. Kama hataruhusiwa hayo mawili hapo juu, basi amuache apigane na maadui zake mmoja mmoja. Kwa haya Umar ibn Sa'd akajibu:

“Kuhusu maombi mawili ya kwanza, hayo hayawezi kukubaliwa. Ama kuhusu hilo la tatu, hilo ni jambo ambalo ninaweza kuruhusu.”

Imam (a.s.) alipigana na maadui mmoja baada ya mwingine na akauwa idadi yao kubwa mpaka Umar ibn Sa'd akatambua kwamba Imam hawezি kuzidiwa nguvu na hivyo akivunja ahadi na maagano yake akatoa maagizo kwa askari wake kumshambulia Imam (a.s.) kutoka pande zote.

(Muntakhab Turayyhi)

Askari hao wakamshambulia Imam (a.s.) naye akiwa peke yake alipambana nao akiwaua au kumjeruhi kila aliyejukia karibu naye.

Mas'ud katika *Ithbat al-Wasiyyah* anaandika kwamba Imam (a.s.) peke yake aliuwa askari elfu moja na mia nane wa adui. Kwa mujibu wa riwaya nyingine aliuwa adui elfu moja na mia tisa na hamsini na kuwajeruhi wengi wao.

Umar ibn Sa'd kuona hivyo, aliwakemea askari wake: "Huzuni iwashukieni! Huyo ni mtoto wa Ali ibn Abi Talib, mshika upanga maarufu kabisa mionganoni mwa Waarabu. Mshambulieni kutokea kila upande."

Hapo walenga mishale elfu nne waligeuzia pinde zao kumuelekea Imam (a.s.) na kumfanya ndio shabaha ya mishale yao.

(Nafas al-Mahmum)

Mwili wake mtukufu uliozingirwa na mishale mingi kupita kiasi ulielezewa kama uliofanana na mnyama nungunungu. – (Imam Muhammad ibn Ali al-Baqir (a.s.) anasimulia kwamba Imam (a.s.) alikuwa na majeraha zaidi ya mia tatu na ishirini katika upande wa mbele wa mwili wake. Hii ni kwa sababu yeye hakuwahi kugeuka na kumpa mgongo adui. – *Amali al-Saduq*).

Shimr ibn Dhi Jawshan alikuja na kundi la watu wakisonga kuelekea kwenye mahema ya Imam (a.s.).

Imam (a.s.) alipowaona hivyo aliwakemea: "Enye wafuasi wa kizazi cha Abu Sufyan, kama hamna dini au kuhofia Siku ya Kiyama, basi angalau kuweni watu huru katika mambo yenu ya kidunia!"

"Unasema nini, Ewe mtoto wa Fatimah?" Shimr alirudisha maneno.

“Mimi ndiye ninayepambana na ninyi, hawa wanawake na watoto wamefanya kosa gani? Waambie watu wako waondoke kwenye mahema haya na wasiyakaribie wakati nikiwa bado niko hai.” Alijibu Imam (a.s.).

“Sisi hatutayasogelea mahema yako wakati bado ukiwa hai.” Alijibu Shimr, kisha akiwageukia askari wake: “Oh, enyi watu, ondokeni kwenye mahema haya na muendeeni Husein na mummalize kabisa!”

Walimshambulia Imam (a.s.) naye aliyakinga mapigo yao mpaka Salih ibn Wahab alipota pigo kwenye paja la Imam (a.s.), pigo ambalo lilimsababishia yeye kuanguka kutoka kwenye farasi wake. Imam aliangukia upande wake wa kulia wakati alipotua ardhini lakini hata hivyo aliweza kusimama na kuendelea kupambana.

DU’A YA MNONG’ONO YA IMAM (A.S.)

Imam (a.s.) alipokuwa akianguka kutoka kwenye mgongo wa farasi wake kwa mara ya mwisho na kutua kwenye changa unaounguza, akiwa ametapakaa damu yake mwenyewe na akilala kwenye mishale ilioenea mwilini mwake kama kitanda, Imam (a.s.) alimnong’oneza Mwenyezi Mungu:

“Subira kwenye amri Yako Ewe Mola, hakuna mungu ila
Wewe. Oh,
Ewe Msaidizi wa kila anayetafuta msaada. Sina Mola
mwingine badala Yako,
na hakuna mwenye kustahiki kuabudiwa isipokuwa Wewe.
Ustahimilivu juu ya hukumu Yako.
Oh, Ewe Msaidizi wa yule ambaye hana msaidizi.

“Oh, Ewe wa Milele ambaye huna mwisho. Ewe Mfufuaji wa wafu.

Ewe Ambaye unahifadhi kila nafsi pamoja ni kile ilichokichuma

Hukumu kati yangu na wao, Ewe Mbora wa Mahakimu.”

(Maqtal al-Husayn al-Muqarram)

Imam (a.s.) vilevile alighani kwa shauku ya kukutana na Mwenyezi Mungu kabla ya kifo chake:

“Nimeitelekeza dunia kwa mapenzi Yako
nimewafanya wanangu kuwa mayatima ili niweze kuonana
na Wewe.

“Kama panga zingekuwa zinikate vipande vipande katika
Mapenzi Yako
Hata hivyo pia, moyo wangu usingemtamani mwingine
kuliko Wewe.”

BIBI ZAINAB KATIKA KUKATWA KICHWA KIKATILI KWA IMAM (AMANI IWE JUU YAO WOTE)

Katika nyakati za mwisho za uhai wa Imam (a.s.) Bibi Zainab alikimbia kutoka kwenye mahema huku akigutia: “Ewe Muhammad, Oh baba, Ewe Ali, Ewe Ja’far!” Halafu akaendelea kusema: “Natamani kama Mbingu zingeangukia ardhini, kama tu milima ingefikichika.”

Kisha akasimama juu ya kilima kidogo na akamuona Umar ibn Sa’d akiwa na kikundi cha watu wakienda kumuelekea Imam (a.s.) aliyekuwa amelala kwenye mchanga unaochoma akimuomba

Mwenyezi Mungu kwa pumzi zake za mwisho mwisho. Yeye alipiga ukelele kuita: “Ewe Umar, hivi utaangalia tu huku Abu Abdillah akiwa anauliwa?”

Kusihi huku kwa Bibi Zainab kulikuwa kunavunja moyo sana kiasi kwamba Umar ibn Sa'd alilia sana mpaka ndevu zake zikaloweshwa na machozi yake. Halafu akageuzia mbali uso wake kutoka kwa Bibi Zainab na hakumjibu.

Pale Bibi Zainab alipoona kwamba wao hawatamuacha ndugu yake, alipiga ukelele katika kukata tamaa: “Hivi hakuna Muislam mionganoni mwenu ninyi?”

Vilio vyake vilijaza angahewa, na Imam (a.s.) huku akishindwa kuhimili kutokuwa na msaada kwa dada yake, aliamka tena na akawashambulia maadui huku akisema: “Wallahi kamwe hamtakuja kupigana na mtu ye yote kama mimi. Mmejiingiza kwenye ghadhabu ya Mwenyezi Mungu ninyi wenyewe. Baada ya kuniwa mimi, mtakuja kuuwana wenyewe kwa wenyewe kwa laana ya Mwenyezi Mungu.” Aliendelea kupigana nao mpaka mapigo mengine sabini na mbili zaidi yakauchana mwili wake uliobarikiwa.

IMAM (A.S.) KURUSHIWA JIWE NA MKUKI WENYE NCHA TATU

Imam (a.s.) alirudi nyuma na akavuta pumzi kwa muda kidogo. Alikuwa amesimama wima wakati alipotupiwa jiwe. Hilo jiwe lili-piga kwenye paji la uso wake na likasababisha kutoka damu kwa wingi. Wakati Imam (a.s.) alipokuwa ananyanya pindo la joho lake ili kusafisha paji lake la uso, mshale wenye ncha tatu uliokuwa umechovyywa kwenye sumu ulirushwa kumuelekea yeye ambao ul-

imchoma (nafsi zetu ziwe fidia kwa ajili yake) kwenye kifua chake ama tumboni. Bila ya kupanga na kuamua, ye ye alighani:

“Kwa jina la Mwenyizi Mungu, na pamoja na Mwenyezi Mungu na juu ya dini ya Mtume wa Mwenyezi Mungu.”

Kisha akanyanya kichwa chake kuelekea juu mbinguni na akasema: “Wanamuua mtu ambaye ndiye mtoto pekee wa binti ya Mtume Wako.”

Kisha aka ukamata ule mshale uliokuwa umepenya kupitia kwenye kifua chake hadi mgongoni kwake na aka uchomoa kupitia mgongoni kwake huku damu ikimwagika kwa wingi.

(Nafas al-Mahmum)

SHAHADA YA KUCHOMA MOYO YA IMAM (A.S.)

Katika hili tukio la kuchomoa mshale, Imam (a.s.) alikomba kila tone la damu lililokuwa limebakia pamoja na nguvu zake zote. Maadui waliacha mapigano na hakuna aliyethubutu kumsogelea Imam (a.s.) kumpa ye ye pigo la mwisho.

Shimr (*laanatu-llahi alayhi*) aliwakemea askari wake: “Mama zenu wawalilieni ninyi! kwa nini mnasubiri? Muuweni mtu huyo (akimaanisha Imam a.s.)

Askari hao walimzingira na kuanza kumshambulia Imam huyo anayefariki. Askari mmoja alimpiga kwenye mkono wake wa kushoto wakati askari mwingine akipiga kwenye bega lake. Sinan ibn Anas alijitokeza mbele na kwa ukatili kabisa akasukumiza mkuki

wake kwenye uvungu wa koo la Imam (a.s.) kisha akauchomoa na kuuchoma kwenye kifua chake Imam (a.s.). Kwa namna fulani Imam (a.s.) alimudu kwa taabu kubwa mno kubakia amesimama mpaka Sinan ibn Anas (*laanatu-llahi alayhi*) alipomchoma mshale kwenye koo lake. Imam (a.s.) alianguka chini na kisha baada muda kidogo alijitahidi kukaa na kuuchomoa mshale huo kutoka shingoni kwake. Kichwa chake, ndevu na kifua vilikuwa vimefunikwa kwa damu yake.

“Namna hii ndivyo nitakavyokutana na Mola Wangu nikiwa nimegubikwa na damu yangu mwenyewe, na nikiwa nimenyimwa haki yangu.” Alisema al-Imam Husein (a.s.).

Hilal ibn Nafii’, kamanda mmojawapo wa maadui anaelezea:

“Niliangalia kwenye medani ya vita na nikamkuta Husein akifurukuta na kugeuka kutoka upande mmoja hadi mwingine wakati roho yake ilipokuwa inatoka kwenye viungo vyake. Aling’ara sana wakati huu. Uzuri na ushwari uliotokeza kutoka kwake ulinizuia mimi kufikiria kumuua. Kamwe sijawahi kuona mtu ambaye ameuliwa kikatili kiasi hicho na akawa anapendeza hivyo kama yeye.”

Katika muda huu Imam (a.s.) aliomba kutu ya maji. Ambapo adui mmoja aliyekuwa amemsimamia karibu yake akasema: “Wewe hautayaonja maji mpaka utakapopewa yale maji yanayochoma ya Jahannam.”

“Laa sivyo, mimi nitatangulia kwa babu yangu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na kunywa kutoka kwenye chemchemi ya Peponi na kwake mimi nitatoa malalamiko yangu juu ya vitendo vyenu.”

Maneno hayo ya Imam (a.s.) hayakuwa na athari yoyote kwao watu hawa. Kana kwamba nyoyo zao zimekuwa ngumu mno na dalili zote za huruma zilikuwa zimeondolewa kutoka kwao.

Umar ibn Sa'd aligeukia upande wake wa kulia na akamwambia askari mmoja: "Mmalize kabisa al-Husein." Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Sinan ibn Anas alimuelekeza Khawli: "Nenda ukamkate kichwa al-Husein." Khawli alisonga kuelekea kwa Imam Husein (a.s.), lakini akaanza kutetemeka na akarejea kwenye nafasi yake ya mwanzo alipokuwa.

Mwenyezi Mungu akukate mikono yako! Kwa nini unatetemeka?" Shimr alimuza. Halafu yeye Shimr (*laanatu-llahi alayhi*) mwenyewe akaenda kwa Imam (a.s.) na akamkata kichwa chake huku akisema: "Ingawa hata hivyo ninajua kwamba wewe ni mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu na mbora wa watu kupitia baba yako na mama yako, na kiongozi wa watu, bado mimi nitakikata kichwa chako." Shimr alikikabidhi kichwa kile kilichobarikiwa cha Imam (a.s.) ili akipeleke kwa Umar ibn Sa'd – laana juu yao wote.

Mtumishi wa kike wa familia ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikimbilia mahali ambapo Imam (a.s.) alikuwa ameuliwa na akaambiwa: "Ewe mtumishi wa Allah, bwana wako ameuliwa." Mtumishi huyo alirejea kwenye mahema huku akilia na kuguta kwa sauti: "Wamemuua al-Husein, wamemuua al-Husein!"

Wanawake walitoka nje ya mahema na wakalia sana kwa sauti, wakipiga mayowe yasiyodhibitika kwa kifo cha Imam al-Husein (a.s.).

(*A'yan al-Shi'ah*)

IMAM (A.S.) ANAOMBAA MAJI

Kwa mujibu wa riwaya moja, wakati Shimr alipoweka sime yake kwenye shingo yenye kuungua joto ya Imam (a.s.), Imam mtukufu (a.s.) alimgeukia na kwa pumzi zake zinazoishia akasema:

“Kama unataka kuniua mimi basi nipaatie kutu ya maji.”

Kwa ombi hili Shimr (*laanatu-llahi alayhi*) akajibu akasema: “Wallahi! Wewe hutapata hata tone la maji hadi utakapokionja kifo kutu baada ya kutu.”

(*Kibrit al-Ahmar*)

Kwa mujibu wa riwanya nyingine, wakati Umar ibn Sa'd alipowaamuru askari wake: “Nendeni mkammlize yule bwana,” Shimr alikwenda kwa Imam (a.s.), akakaa kwenye kifua chake (a.s.) na akakamata zile ndevu zake zilizokuwa zimeLOWA damu na kisha kwa ukatili kabisa akakikata kichwa chake (a.s.) kwa mapigo kumi na mbili ya kisu chake.

(*Maqtal al-Husayn al-Muqarram*)

MSIBA WA DHUL-JANAH – YULE FARASI MWAMINIFU WA IMAM (A.S.)

Pale Imam (a.s.) alipodondoka ardhini, Dhul Janah, yule farasi wake alianza kumzunguka akiyakinga mapigo ya maadui yasimfike wakati huo akiwa anatoa milio na kubweka.

Umar ibn Sa'd alikemea: “Msimamisheni vurugu zake farasi huyo na mumlete kwangu kwani huyo ndiye mbora wa farasi wote wa Mtume!” Kundi la askari likamzingira lakini farasi huyo akaanza kuwapiga mateke na akawaua askari wa maadui wapatao arobaini.

Baada ya kuona hivyo, Umar ibn Sa'd aliwapigia kelele: “Mwacheni. Ngoja tuone ni nini atakachofanya farasi huyu.”

Wakati farasi huyo alipoachwa huru alikwenda kwenye ule

mwili wa Imam (a.s.) uliojaa damu na akaweka kishungi chake juu ya Imam (a.s.) mpaka kikapata rangi ya damu yake hiyo. Farasi huyo alikuwa akiunusa mwili wa Imam (a.s.) na kutoa mlion wa sauti kubwa.

Imam Muhammad ibn Ali al-Baqir (a.s.) anasimulia kwamba farasi huyo katika milion wake alikuwa akikemea maneno: “Watu madhalimu wa Ummah wamemuua mwana wa Mtume wao!”

Halafu farasi huyo aligeukia kwenye mahema akienda shoti kuyaelekea huku akitoa milio kwa namna ambayo ilijaza angahewa. Bibi Zainab (s.a.) alipoisikia milio hiyo ya farasi alimeukia Bibi Ummu Kulthum na kusema: “Huyo ni farasi wa kaka yangu al-Husein (a.s.) akielekea huku kwenye mahema. Anaweza akawa ameleta maji kiasi.”

Ummu Kulthum (s.a.) alitoka mbio kwenye hema na akamuona farasi huyo asiye na mpandaji wake. Akapiga mikono yake juu ya kichwa chake na akachana ushungi wake na huku akiguta: “Wallahi al-Husein ameuawa!” Bibi Zainab alianza kulia na kumuomboleza Imam (a.s.) pale alipovisikia vilio vya Ummu Kulthum.

(Ma'ali al-Sibtayn)

Katika Ziyarat al-Nahiyah, Imam wa Kumi na Mbili, al-Mahdi (a.t.f.s.) amemhutubia Imam Husein (a.s.) na akasema:

“Farasi wako alikimbilia kwenye mahema akilia na kubweka. Na pale wanawake walipomuona farasi wako huyo amechanganyikiwa, na wakayaangalia matandiko yako yanepinduliwa na kukunjwa, walitupilia mbali (kwa huzuni) mitandio yao, nywele zao zikatawanyika wazi, wakipiga nyuso zao makofii huku zikiwa zimefunuliwa wazi, wakiom-

boleza. Wakiwa wamedhalilishwa baada ya kuwa wenye hadhi. Wakikimbilia pale mahali ambapo ulikuwa umeangukia na kumuona Shimr amekaa juu ya kifua chako akiuweka wazi upanga wake tayari kwa kulifunua koo lako.”

SAKINAH; PALE ANAPOMUONA DHUL-JANAH

Kwa mujibu wa riwaya nyingine, pale zile sauti za farasi anayekuja ziliposikika ndani ya mahema, Bibi Zainab alimwambia Sakinah (amani iwe juu yao wote): “Sakinah baba yako amerudi na maji. Mwendee ukanywe hayo maji!” Sakinah alitoka mbio nje ya hema na akaiona hali ya Dhul-Janah. Alilia na kulalamika: “Oh, ewe Muhammad! Oh, huzuni ya kuondokewa! Oh, ewe Husein! Oh, ewe babu yangu! Oh, ewe Fatimah! Ewe Dhul-Janah! Ni nini kimemfika baba yangu? Umemuacha wapi muombezi wa watu? Yuko wapi Nuru ya macho ya Mtukufu Mtume (s.a.w.w.)?”

Alisoma beti fulani kadhaa pale kwenye farasi huyo:

“Ewe farasi, umemuacha baba yangu mionganii mwa maadui?
Umemuacha kati ya mchanga unaochoma na damu wakati wanaujeruhi mwili wake?

Rejea, ewe farasi na ukamrudishe baba yangu hapa. Na kama utarejea naye hapa,
Basi itakuwa kubwa sana hadhi yako kwetu sisi.”

(Tadhkirat al-Shuhada)

Imesimuliwa katika kitabu *Masa'ib al-Ma'sumin* kwamba: Wakati Dhul Janah aliporejea kwenye yale mahema na wanawake

wakakimbia wakipiga mayowe na kupiga makofi nyuso zao, kila mmoja wao aliongea na farasi huyo. Mmojawao alisema: “Ewe farasi, kwa nini hukumrudisha al-Husein hapa?” Ambapo mwingine kati yao alisema: “Kwa nini umemuacha Imam (a.s.) mionganoni mwa maadui?” Bibi Zainab (s.a.) aliguta: “Ah, uso wake umefunikwa na damu ya kaka yangu!” Bibi Sakinah (s.a.) aliuliza: “Je, baba yangu alipewa funda ya maji au aliuawa akiwa na kiu yenye kuchoma?”

(Masa’ib al-Ma’sumin)

Kwa mujibu wa riwaya nyinginez, farasi huyo alipigapiga kwa nguvu sana kichwa chake juu ya ardhi karibu na mahema hayo mpaka akafa.

(Nafas al-Mahmum)

Na kwa kulingana na riwaya nyingine, farasi huyo akiwa amechanganyikiwa na kuhofia sana alikimbia kutoka hapo kwenye mahema mpaka kule mto Furati ambako alitumbukia humo na kupotea kabisa.

(Tadhkirat al-Shuhada)

BAADHI YA MISIBA ISIYOVUMILIKI ILI-YOMPATA IMAM (A.S.) ILE SIKU YA KUPATA SHAHADA YAKE

1. Wakati ambapo Imam (a.s.) hakuweza kuendelea kupambana, alisimama kwa taabu sana pale mahali ambapo alikuja kuuliwa baadaye. Askari wa adui walikuwa wakimsogelea kisha wakir-

udi nyuma wakikataa kuhusika na kumuua yeye. Katika wasaa huu, Malik ibn Yusr alikwenda karibu naye akamtupia matusi na kisha akapiga kwenye kichwa chake kitukufu kwa upanga wake. Pigo hilo la upanga lilivunja helimeti yake vipande vi-wili ulipokuwa ukipenya kwenye kichwa kitukufu hicho. Damu ilifoka kutoka kichwani kwa Imam na kuangukia usoni mwake (a.s.). Imam aliiufuta damu hiyo na akafunga kipande cha nguo kwenye jeraha hilo.

(Luhuf)

2. Baada ya kuuliwa kwa Imam (a.s.), Umar ibn Sa'd (*laanatullahi alayhi*) aliwaita watu wake na kuwauliza: “Ni nani kati yenu watakaochukua jukumu la kukanyaga kifua na mwili wa Husein kwa kwato za farasi wao?”

Watu kumi walichukua jukumu la kutekeleza jinai hiyo mbaya ya kikatili. Waliwaswaga farasi wao juu ya ule mwili uliokatwa kichwa wa Imam mtukuka (a.s.) na wakavunja kila fupa katika kifua na mwili wake mtukufu. Baada ya hili, watu hao kumi wakaja kwa ibn Ziyad kudai zawadi zao. Usayd ibn Malik akamwambia ibn Ziyad: “Sisi ndio wale tulioopanda juu ya farasi wenye nguvu na kupondaponda mifupa katika kifua na mwili wa Husein.”

“Na ninyi ni nani? Ibn Ziyad akawauliza wale wengine. Wakamjibu: “Sisi ndio tuliuokanyaga mwili wake mpaka ukawa laini kama mkate uliopondwa.”

Ibn Ziyad akaagiza zawadi ndogo itolewe kwao. Abu Umar Zahid anasimulia: “Hawa kumi wote walizaliwa kwenye zinaa. Mukhtar al-Thaqafi katika mapinduzi yake ya kulipiza kisasi damu ya al-Husein (a.s.) alifanya mikono na miguu ya watu

kumi hawa kupigiliwa misumari na akafanya farasi wawakanyage kwenye migongo yao mpaka wakafariki.”

(*Luhuf*)

3. Katika siku ya Ashura, wakati Imam (a.s.) alipoingia kwenye mto Furati na akataka kunywa maji kutoka humo, Husein ibn Numayr (*laanatu-llahi alayhi*) alimrushia mshale ambaa ulim-choma kwenye koo lake. Imam (a.s.) aliuchomoa mshale huo na akaweka mikono yake chini ya koo lake akiikinga damu hiyo na kuirusha kuelekea angani huku akisema kumwambia Husein ibn Numayr: “Mwenyezi Mungu asiikate kiu yako.” Halafu Imam (a.s.) akaambiwa kwamba mahema yake yali-kuwa yanaporwa, kama ilivyoelezwa hapo kabla, na kuzuiwa asiyanywe maji hayo.

Wakati Imam (a.s.) aliporudi kule kwenye mahema wanawake na watoto waliokuwa na kiu walitoka nje wakidhani kwamba ameleta maji. Lakini walipoiona shingo yake, kifua na mikono imeloa damu, walilia na kupiga mayowe huku wakipiga nyuso zao kwa huzuni.

Kabla Imam (a.s.) hajaenda kwenye mto Furati, mmoja wa watoto alimfuata na kusema: “Ewe baba! Mimi nina kiu.” Hapo Imam (a.s.) alimjibu: “Ewe mtoto, ivumilie kidogo tu na mimi nitakwenda kuleta maji.” Pale sasa aliporejea, mtoto yule alimkimbilia Imam (a.s.) na kumuuliza: “Ewe baba yangu! Je, umeniletea maji? Imam (a.s.) alilia na kusema maneno haya: “Enyi Shi’ah wangu! Nikumbukeni mimi wakati mtakapokuwa mnakunywa maji matamu.” Halafu Imam akaomba kipande cha nguo ambacho alikifunga kwenye shingo yake na akawaaga wale wanawake na watoto kwa mara nyingine tena. Alijaribu

sana kufika kwenye maji mara kadhaa lakini akawa anazuiwa na maadui. Kiu ya watoto wake wachanga ilikuwa ikimlazimisha kwenda kule mtoni.

(*Ma'ali al-Sibtayan*)

4. Imam Muhammad al-Baqir (amanu iwe juu yake) amesema kwamba walimuua Imam al-Husein (a.s.) katika njia ya kikatili ambayo kwamba Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alikuwa amewakataza watu kuwaulia wanyama wa porini.

“Aliuawa kwa panga, mikuki, mawe na fimbo. Na baada ya kumuua yeye, waliupondaponda mwili wake chini ya kwato za farasi wao.”

(*Kibrit al-Ahmar*)

FAHARASA YA VYANZO VILIVYOTUMIWA NA MWANDISHI

Akthir al-Ibadat fi Asrar al-Shahadah – pia kinajulikana kama *Asrar al-Shahadah*

Iqa' ibn Abid ibn Ramadhan al-Shayrawani al-Darbandi al-Ha'iri.

A 'lam al-Wara – pia kinajulikana kama *A 'lam al-Huda*

Sheikh Abu Ali al-Fadhl ibn al-Hasan ibn al-Fadhl al-Tabrasi

Al-Amali – kinajulikana pia kama *al-Majalis*

al-Sheikh as-Saduq Abu Ja'far Muhammad ibn Ali ibn Babawi al-Qummi

Anwar al-Shahadah

Hasan ibn Ali al-Yazdi al-Ha'iri

A 'yan al-Shi 'ah

Sayyid Muhsin Amin

Bihar al-Anwar

Allamah Majlisi

Al-Dam 'at al-Sakibah fi Musibat al-Ratibah

Muhammad Baqir ibn al-Karim al-Bahbahani al-Najafi

Din wa Tamaddun – kinacho julikana pia kama *Islam wa al-Falsafah*

Mufid al-Malja'i al-Khalkhali

Fursan al-Hayjan

Dhabih Allah ibn Muhammad Ali al-Mahalati

Ithbatal-Wasiyyah

Abu al-Hasan Ali ibn al-Husayn ibn Ali al-Mas'udi

Kamil al-Baha'i

Sheikh Imad al-Din al-Hasan ibn Ali al-Tabari

Al-Kamil fi al-Tarikh

Iz al-Din Abi al-Hasan al-Shaybani, anaye julikana kama ibn al-Athiir

Kibrit al-Ahmar fi Shara 'it Ahl al-Minbar

Muhammad Baqir al-Birjandi

Kitab al-Irshad

Al-Shaykh al-Mufid

Al-Luhuf ‘ala Qatala al-Tafuf

Abu al-Qasim Ali ibn Musa ibn Tawus al-Hilli

Ma’ali al-Sibtayn

Muhammad Mahdi ibn abd al-Hadi al-Mazandarani al-Ha’iri

Maqatil al-Talibiyin

Abu al-Faraj al-Isfahani

Maqtal al-Awalim

Sheikh Abdu Allah ibn Nur al-Bahrani

Maqtal al-Hussayn

Abu Mikhnaf Lut ibn Yahya

Maqtal al-Hussayn

Abd al-Razzaq al-Muqarram

Maqtal al-Hussayn

Khawarizmi

Masa’ib al-Abrar

Shah Mirza al-Salmasi

Massa’il al-Ma’sumin

Mawla Abd al-Khaliq al-Yazdi

Minhaj al-Dumu’

.....
Muntaha al-Amal

Sheikh Abbas al-Qummi

Muntakhab al-Tawarikh

Muhammad Yusuf ibn Rahmat Allah

Muntakhab al-Turayhi

Shaykh Fakhr la-Din ibn Muhammad Ali ibn Ahmad ibn Turayh
al-Najafi

Muthir al-Ahzan

Shaykh Sharif ibn Abd al-Husayn ibn Muhammad Hasan

Nafas al-Mahmuum

Shaykh Abbas Qummi

Nahj al-Shahadah

.....

Nasikh al-Tawarikh

Mirza Muhammad Taqi al-Kashani

Rayhan al-Shari'ah

.....

Riyahin al-Shari'ah

.....

Sharh Nahjul-Balaghah

Ibn Abi al-Hadid al-Mu'tazilah

Tarikh al-Tabari

Abu Ja'far Muhammad ibn Jarir al-Tabari

Tadhkirat al-Shuhada'

Hakim Amanat Ali

Unwan al-Kalam

Muhammad Baqir al-Fisharki al-Isfahani

Waqa'i wa al-Hawadith

.....

Ziyarat al-Nahiyah

Sayyid Ibn Tawus

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala

16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)

37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana
39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipyta
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu

58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah

78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgongwa
97. Sadaka yenyе kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali

99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenyé Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kumsalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqlain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne

120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili

161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na

Ramadhani)

182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwenendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo

202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Mwanachuoni wa Kishia (*Al-Muraja 'aat*)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Upotoshaji dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura
211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Kuvunja Hoja Iliyotumika Kutetea Uimamu wa Abu Bakr
216. Mfumo wa Wilaya
217. Ndoa ya Mutaa
218. Vipi Tutaishinda Hofu?

KOPI NNE ZIFUATAZO MSIBA WA DHUL-JANAH ZIMETAFSIRIWA

KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique